

KUMSWALIA MTUME NI UFUNGUO WA UTATUZI WA MATATIZO

الصلوات مفتاح حل المشكلات

(Hadithi na visa vya kweli juu ya
fadhlila za kumswalia
Mtukufu Mtume Muhammad (saww)
na Kizazi chake kitukufu (as)

Kimeandikwa na:
Ali Khamsah al-Qazwini
(Maarufu kwa jina la al-Hakim al-Hindi)

Kimetarjumiwa na:
Abdul Karim Juma Nkusui

ترجمة

الصلوات مفتاح حل المشكلات

تأليف

على خمسه اي القزويني (المعروف بالحكيم الهندي)

من اللغة العربية الى اللغة السواحلية

© Haki ya kunakili imehifadhiwa na:
Al-Itrah Foundation

ISBN No: 978 - 9987 –512 – 28 – 7

Kimeandikwa na:
Ali Khamsah al-Qazwini
(Maarufu kwa jina la al-Hakim al-Hindi)

Kimetarjumiwa na:
Abdul Karim Juma Nkusui

Kimepangwa katika Kompyuta na:
Al-Itrah Foundation

Toleo la kwanza: Machi, 2014
Nakala: 1000

Kimetolewa na kuchapishwa na:
Alitrah Foundation
S.L.P. - 19701, Dar es Salaam, Tanzania
Simu: +255 22 2110640 / 2127555
Barua Pepe: alitrah@yahoo.com
Tovuti: www.ibn-tv-com
Katika mtandao: www.alitrah.info

YALIYOMO

Neno la Mchapishaji	1
Neno kwa msomaji mpendwa.....	3
Utangulizi.....	6
Maneno katika kumswalia Mtume Muhammad (s.a.w.w) na Ali zake (a.s.).....	9
Kumswalia Mtume Muhammad (s.a.w.w) na Aali zake	9
Dua katika mapokezi ya Ahlul-Baiti (a.s.)	12
Miongoni mwa maana za swala	14
Dondoo kutoka katika maisha ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w)	17
Swala ya Mwenyezi Mungu kwa Nabii (s.a.w.w.)	18
Kuhesabu thawabu za kumswalia mtume na Aali zake	18
Malipo ya kumswalia mtume ndani ya kitabu	19
Mwenye kunyimwa harufu ya pepo.....	20
Radhi za mola na utakaso wa amali.....	20
Swala iliyo sawa na swala elfu kumi	21
Kulipa deni kuitia kumswalia Mtume (s.a.w.w) na Aali zake	22
Mgonjwa apona kuitia kumswalia Mtume Muhammad na Aali zake	23

Madhambi yafutwa kupitia kumswalia	24
Mtume Muhammad na Aali zake	24
Madhambi hucheleweshwa kuandikwa	24
Kusamehewa dhambi	24
Kusamehewa dhambi za miaka thamanini.....	25
Kusamehewa dhambi kadiri ziwavyo	25
Inatia uzito katika mizani.....	26
Rehema za Mwenyezi Mungu kwa mwenye kumswalia Nabii	26
Mabaya kumi hufutwa kwa baraka za swala moja	26
Kumswalia Nabii ni kinga dhidi ya moto	27
Kubashiriwa pepo	27
Malipo ya mashahidi sabini na wawili.....	28
Maana ya dhikri	28
Siri iliyopelekea wana wa Israel kuondolewa mateso	28
Sababu ya kujibiwa Dua	30
Swala iliyo sawa na hija sabini	31
Hukidhi haja za dunia na akhera.....	31
Madhambi hupukutika kwa kumswalia nabii na Aali zake	32
Msisitizo juu ya kumswalia muhammadi na Aali zake.....	32
Swala ya mtume huondoa ufakiri	32

Swala ya Mtume (s.a.w.w) hutajirisha	33
Inasaidia kuwa na kumbukumbu	33
Ni dawa ya kutibu ufkiriri	34
Bishara kwa mwenye kumswalia nabii na Aali zake	34
Kunusa manukato kwa kumswalia Mtume Muhammad (s.a.w.w) na Aali zake (a.s).....	35
Kumswalia Mtume Muhammad (s.a.w.w) na Aali zake baina ya dhuhri na la asri	36
Mwenye shauku ya kumdiriki Al-Qaim (af).....	36
Sharti la kujibiwa Dua	36
Huondoa kizuizi kinachozuia Dua kujibiwa	37
Kumwiga Imam Ridhaa (a.s)	37
Kumuona Nabii (saww) katika ndoto	37
Siri ya kumuona Nabii (saww) katika ndoto	37
Furaha ya Nabii kwa kumswalia yeye	38
Malaika aliyeamriwa kumfikishia Nabii (saww) swala	38
Mtu ambaye nabii anatajwa kwake na wala asimswalie	39
Matokeo ya kutokujali	39
Malipo ya asiyemswalia Mtume (saww)	39
Msikosee njia ya kuelekea peponi	40
Swala kigutu.....	40

Nyakati za kumswalia Mtume (saww).....	40
Sunnah ya kumswalia Nabii (saww) siku ya Ijumaa	41
Amani baina ya Ijumaa	41
Amani ya mwaka mzima	41
Hakuna swala bila ya kumswalia Muhammad na Aali zake	42
Nuru ya kumswalia muhammadi na Aali zake (a.s.)	42
Amali bora zaidi katika siku ya Iijumaa	43
Swala ya Shaabaniyyah, inayosomwa kila siku ndani ya mwezi wa Shabani	43
Orodha ya herufi za majina ya maasumina kwa ajili ya kukhitimishia.....	46
Kukhitimisha kumswalia Mtume Muhammad (s.a.w.w) na Aali Muhammad (as).....	47
Adabu za kuzingatiwa wakati wa kukhitimisha swala ya Mtume (saww)	48
Aina za kukhitimisha swala za Mtume (saww)	50
Njia ya kukhitimisha	51
Khitma arobaini	53
Kwa ajili ya kuondoa adhabu ya kaburi	68
Amali zenye manufaa zaidi kaburini	69
Miongoni mwa faida za kumswalia Muhammadi (saww) na Aali zake (as)	69
Kumswalia Mtume Muhammad (s.a.w.w) na Aali zake (as)	71

Kunalingana na tasbihi na tahlili.....	71
Nyakati ambazo inapasa humo kumswalia Mtume (saww).....	72
Kumswalia Mtume Muhammad (s.a.w.w) na aali zake ukiwa macho na wakati wa kulala	74
Kujikomboa kutoka kwenye dhambi kupitia kumswalia Mtume Muhammad (s.a.w.w) na Aali zake (as)	75
Kuondoa masikitiko kwa kumswalia Mtume (saww).....	78
Kujikinga na moto wa jahannam kwa kumswalia mtume (saww).....	78
Vitendo bora zaidi katika kaaba	78
Utajo wa moyoni na ulimini	79
Kumhudhurisha Nabii (saww)	79
Riwaya kutoka kwa Salman Al-Farisiy.....	79
Riwaya kutoka kwa masheikh wanaozingatiwa	80
Swala inayolingana na kukhitimisha Qur'ani mara 12,000.....	81
Shufaa ya manabii elfu moja.....	81
Kujibiwa Dua	82
Kwa nini mahari ya sunnah yamekuwa ni dirhamu 500?	82
Kisa cha ng'ombe wa Bani Israil	83
Arshi yanyanya kwa kumswalia Mtume Muhammad (s.a.w.w) na Aali zake (a.s.)	88

Kuondoa huzuni na kutakasika na dhambi	93
Sababu ya kusahau na tiba yake.....	94
Kisa cha mtu anayemswalia mtume (saww) daima	94
Busu la Nabii (saww).....	97
Miongoni mwa baraka za kumswalia Mtume Muhammad (s.a.w.w) na Aali zake (as)	98
Bahari yenyenye mawimbi	99
Ni kinga ya usengenyaji.....	100
Tajiri na masikini	100
Adhabu ya kaburi.....	102
Harufu nzuri	103
Kuzuia hatari.....	104
Kumswalia Mtume na pete iliyopotea	104
Swala ya mwisho	105
Kupoteza kitu muhimu.....	106
Karama za Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) kaburini	106
Swala ya Mtume (saww) inaokoa dhidi ya adhabu ya kaburi	107
Amani kutokana na uchungu, wakati wa kutoka roho	108
Swala ya usiku wa kuamkia Ijumaa na ya mchana wa ijumaa.....	109
Mtu atakayekuwa karibu mno na Nabii (saww) siku ya kiyama.....	109

Kupita katika sirat.....	109
Nuru siku ya kiyama	110
Chini ya kivuli cha arshi ya Mwenyezi Mungu mtukufu	110
Kumfukuza shetani kwa swala ya Mtume (saww)	110
Nuru katika sirat.....	113
Anawajibika kupata uwombezi.....	113
Maana ya swala ya Mwenyezi Mungu, ya Malaika, na ya waumini kwa Mtume (saww).....	113
Kinga dhidi ya moto wa Jahannam.....	114
Kuozeshwa hurulaini	114
Kumswalia muhammadi na Aali zake (a.s.) kila wanapotajwa Manabii (as)	115
Rafiki wa Muhammad (s.a.w.w.) katika pepo za juu	115
Amali ya mkesha wa mwezi saba Rajabu.....	116
Amali ya usiku wa nusu ya Shaban	116
Fadhila za swala ya Mtume na Aali zake (a.s.).....	118
Malipo ya mwenye kuacha kumswalia Mtume (saw).....	120
Bahati nzuri	121
Wasia wa awali katika vikao vya kidini.....	125

NENO LA MCHAPISHAJI

Kitabu ulichonacho mikononi mwako asili yake ni cha lugha ya Kiarabu kwa jina la, *al-al-Salawaatu Miftah hal-il Mushkilaat* kilichoandikwa naAli Khamsah al-Qazwini ambaye anajulikana zaidi kwa jina la, al-Hakim al-Hindi. Sisi tumekiita, *Kumswalia Mtume ni Ufunguo wa Utatuzi wa Matatizo*. Kitabu hiki kinahusu umuhimu na ubora wa kumswalia Mtume Muhammad (saww) na faida zake.

Iliposhuka aya 56 Sura al-Ahzaab isemayo: “*Hakika Mwenyezi Mungu na malaika Wake wanamswalia Nabii. Enyi ambao mmeamini! Mswalieni na mumsalimu kwa salamu,*” masahaba walimuuliza Mtume (s.a.w.w): “Tutakuswalie vipi?” Mtume (s.a.w.w) akasema: “Semeni: ‘*Allahumma swalli ‘ala Muhammad wa ‘ala Aali Muhammad.* Wala msiniswalie swala kigutu (iliyokatika).” Masahaba wakauliza: “Swala kigutu ni ipi, Ewe Mjumbe wa Allah?” Mtume akajibu: “Ni kusema: ‘*Allahumma swalli ‘ala Muhammad*’, kisha mnanyamaza, bali ninyi semeni: ‘*Allahumma swalli ‘ala Muhammad wa ‘ala Aali Muhammad.*’”

Mwandishi wa kitabu hiki amekusanya hadithi nyingi zinazohusu ubora, fadhila na faida za kumswalia Mtume (s.a.w.w) pamoja na matukio ya kihistoria yanayounga mkono kauli hii kutoka kwenye vyanzo mbalimbali vya Sunni na Shia.

Sisi kama wachapishaji, tunakichapisha kitabu hiki kama kilivyo kwa wasomaji wetu na kuwashauri wasome yaliyomo humo, wayafanyie kazi na kuyazingatia na kufaidika na hazina iliyomo ndani yake.

Hii ni moja katika kazi kubwa zilizofanywa na Taasisi ya Al-Itrah katika kuwashudumia kielimu wasomaji wake wazungumzaji wa

Kiswahili. Na kwa maana hiyo hiyo, imeamua kukichapisha kitabu hiki chenye manufaa makubwa kwa lugha ya Kiswahili kwa lengo lake lile lile la kuwahudumia Waislamu, hususan wanaozungumza lugha ya Kiswahili.

Hivyo, tunaamini kwamba wasomaji wetu watanufaika vya kutosha kutokana na kitabu hiki, kwa vile ni chenye manufaa sana, hususan wakati huu wa maendeleo makubwa ya elimu katika nyanja zote, ambapo uwongo, ngano za kale na upotoshaji wa historia ni vitu ambavyo havina nafasi tena katika akili za watu.

Tunamshukuru mwandishi wa kitabu hiki Ali Khamsah al-Qazwini, maarufu kwa jina la al-Hakim al-Hindi, kwa kazi kubwa aliyoifanya kwa ajili ya Umma huu wa Waislamu. Allah ‘Azza wa Jallah amlipe kila la kheri na amuingize Peponi kwa salama na amani insha’Allah. Halikadhalika tunamshukuru mdugu yetu Abdul-Karim Juma Nkusui kwa kukitarjumi kwa Kiswahili kitabu hiki, insha’Allah na ye ye Allah ‘Azza wa Jallah amlipe kila la kheri hapa duniani na huko Akhera pia, bila kuwasahau wale wote waliochangia kwa namna mmoja au nytingine mpaka kufanikisha kuchapishwa kwake. Allah Mwenye kujazi awalipe wote malipo mema hapa duniani na huko Akhera pia.

**Mchapishaji
Al-Itrah Foundation.**

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu.

DUA WAKATI WA KUSOMA

“Eee Mwenyezi Mungu nitoe katika giza la dhana na unikirimu kwa nuru ya ufahamu,Eee Mwenyezi Mungu tufungulie milango ya rehema Zako na tusambazie hazina ya elimu Yako kwa rehema Zako ewe Mwingi wa rehema kushinda wote wenye kurehemu. Eee!Mwenyezi Mungu: Jaalia mwisho wa mambo yetu uwe mwema.”

NENO KWA MSOMAJI MPENDWA

A salamu alaikum, nataraji kuwa ni mzima.

Sijui wewe ni nani? Na uko katika nchi gani? Lakini na-kulingania kwa moyo wenye ikhilasi na roho nyeupe kwa ajili ya kusambaza kheri na baraka katika nyanja ya kila muumini, umshukuru Mwenyezi Mungu kwa taufiki yake kwako, kwa kumjua mbora wa viumbe Muhammad na Aali zake watukufu na kujitahidi kujufaida za kuwaswalia. Nataraji kwamba kitabu hiki kilichopo mikoni mwako ni dalili na mwongozo wa utatuzi wa matatizo yote ya kidunia na ya kiakhera na usinisahau katika dua zako njema.

Je, unajua ni mashirika mangapi na taasisi ngapi ambazo zimenuua nakala ya kitabu hiki na zikakitoa zawadi kwa wenye uhu-

sianao nao, kwa wateja wao na kwa wafanyakazi wao? Hakika ni malipo makubwa yalioje watakayoyapata hawa katika juhudzi zao?

Hakika kutoa kwako kitabu hiki zawadi kwa familia yako au marafiki zako itasaidia kujaza mafanikio na taufiki katika maisha yao, na utaongeza juhudzi zao zenyenye manufaa. Ikiwa wewe ni kati ya wenye kutafuta maendeleo na mageuzi ya kimaanawi basi nakuusia kusoma kitabu hiki. Na ikiwa ni kati ya wale wanaotaka majina yao kubaki hai na kuhifadhiwa katika nyoyo za marafiki na pia uhusiano wao wa kijamii kuimarika na kuwa na uwezo mkubwa huku ukitoa huduma kubwa kupitia kwao basi ni juu yako kusoma na kusambaza kitabu hiki.

Ndugu yangu msomaji! Tumia kila fursa, mnasaba, Idi na ziara kutoa zawadi ya kitabu hiki kizuri na jua kwamba kitabu hiki kizuri kina uwezo wa kubadilisha maisha ya mtu na jamii. Na kama unam-jua mtu anayekabiliwa na matatizo ya kiroho na kifkra na anatafuta kwa jitihada utulivu na raha ya kimawazo basi mpe zawadi ya kitabu hiki.

Enyi akina mama watukufu na enyi akina baba na walezi watukufu; kama mna khofu juu ya mustakabala wa watoto wenu basi jitahidi-dini kuwafahamisha vitabu vya Kiislam vitukufu, hakika vinadhamini kwao mafanikio ya dunia na akhera. Enyi walimu watukufu, enyi wenye jukumu la kuongoza vijana, kuwalea na kunyanyua mustawa wao na mnatekeleza jukumu la Manabii (as), wausieni wanafunzi wenu kusoma vitabu vya Kiislam vyenye manufaa, hakika vitawasakieni kutekeleza kazi yenu ya kufikisha ujumbe. Wasilianeni nasi ili tuwatumie vitabu vyenye manufaa katika nyanja za kijamii na kimaadili.

Enyi akina kaka na akina dada watukufu tumeni kwetu maswali yenu na matatizo yenu ya kijamii, ya kitabia na ya kidini, vivyo

hivyo maswali na matatizo ya wale wanaowahusu, nasi kwa nafasi yetu tutayapeleka kwa waliobobe na wajuzi wenye kuwajibika kwa lengo la kujibiwa, kisha tutayatuma kwenu na kupata kutoka kwetu majibu yenyne manufaa mazuri inshaallah.

Anwani yetu:

Tehran Iran,

S.L.P. 88/13445,

AliKhamsaiy al-Qaz'winiy (al-Hakim al-Hindiy),

Mobile: +98 9121099667.

UTANGULIZI

Sifa zote njema ni za Mwenyezi Mungu Mola wa viumbe, rehema za Mwenyezi Mungu zimwendee bwana wetu na Nabii wetu kipenzi cha nyoyo zetu Muhammad (saww) na Aali zake Maasumina, hususan al-Hujjah ibn al-Hasan (aj). Eee Mwenyezi Mungu mteremshie rehema al-Mustafaa Muhammad na Ali al-Murtadhaa na Batuli az-Zahraa na wajukuu wawili Hasan na Husein. Mteremshie rehema Imam Zainul-Abidiyn Ali, al-Baqir Muhammad, as-Sadiq Ja'far, al-Kadhim Musa, na ar-Ridhaa Ali, at-Taqiy Muhammad, an-Naqiy Ali, na Hasan az-Zakiy al-Askariy. Na mteremshie rehema Imam al-Hadi al-Mahdi, ambaye ni Imam wa zama hizi, Khalifa wa Mwenyezi Mungu, Hoja yenyeye nguvu, na Bwana wa wanadamu na majini. Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yao wote.

Kati ya Sunnah tukufu za Mwenyezi Mungu ni kumswalia Muhammad na Aali zake, nao ni utajo bora zaidi kwa ajili ya kukidhiwa haja, kuponya wagonjwa, kuondoa maradhi na huzuni. Muislamu hutekeleza utajo huu mtukufu kila siku kwa uchache mara tisa kwa siku– katika Swala zake za kila siku -na hiyo ni katika tashahudi yake anaposema: “ Eee Mwenyezi Mungu mteremshie rehema Muhammad na kizazi cha Muhammad.” Na inafaa kwake kutaja utajo huu daima ikiwa anataka kuwa mionganoni mwa wenyewe kusalimika katika dunia na akhera, na kuwa katika kundi linalokubaliwa dua inshaallah.

Amesema Amirul-Muuminina (as): “Mja anapoomba na asimtaje Nabii (saww) dua yake inaelea juu ya kichwa chake, anapomswalia Nabii (saww) dua yake inanyanyuliwa juu.”¹

¹ *Mustadrakul-Wasail* cha Nuriy aliyefariki 1320 A. H chapa ya Muasasatu Aali Bait Qum 1408 A. H Juz. 5 Uk. 234, Mlango wa 34 (*Istihabaabi Swalaati Alaa Muhammad wa Aalihi*, Hadith 2, tasalsul 5745).

Hakika sisi katika kitabu hiki – ambacho kiko mikononi mwako na kwa kutaja baadhi ya hadith zenyenye nuru zilizopokewa kutoka kwa Ahlul-Bait (as), na kwa kufaidika kutokana na tafsiri ya baadhi ya Aya za Qur'an tukufu zenyenye mafungamano, na kwa kueleza baadhi ya visa vya kweli ambavyo vimewatokea baadhi ya watu wenye kudumu katika kumswalia Mtume (saww) na Aali zake- tunakusudia kubainisha nafasi ya utajo huu mtukufu na kile unachowezekukifanya kati ya maajabu ili Swala hiyo ya kumswalia Mtume na Aali zake tuifanye kuwa ni kigezo katika kutawasali kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, ili tuweze kutatua matatizo yetu magumu kupitia Swala-hiyo na ili tufarijike kwa kupokea majibu yenyenye kuondoa matafizoyetutote kwa baraka za kumswalia Muhammad na Aali zake.

Inanifurahikia mimi kutaja msukumo ambao umenifanya mimi kuanza kutunga kitabu hiki na ambacho kilikuwa na athari kubwa katika kubadili mwelekeo wa maisha yangu, nayo ni kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufualinijaalia kushiriki katika moja ya mikeshaya Ijumaa mwaka 1978 katika moja ya vikao vilivyokuwa vinaandalialiwa katika khitima ya kumswalia Muhammad na Aali zake, kwa kuandalialiwa na Sayyid Mtukufu Marhum al- Haji Fakhar Tehrani maarufu kwa jina la Fakhir Abaduz, yaani Sayyid Fakhariy al- 'Abbaaiy, na wakati huo huo nilikuwa na haja muhimu sana iliyoshughulisha fikra zangu, moyo wangu na uwepo wangu, nikatawasali katika kikao hicho –nikiwa mkweli mwenye kuitakidi nikiwa nimeazimia kudumukwa Maasumina kumi na nne, na sikukaa isipokuwa wiki moja tu – yaani usiku wa Ijumaa iliyofuata –nikawa nimefanikiwa katika haja yangu. Na kwakweli kukidhiwa haja yangu kwa wepesi huu kuliacha mshangao mkubwa kwangu binafsi hususan na ilikuwa ni nje ya Iran.

Na tangu wakati huo, mimi niko katika yale niliyoazimia, nayo ni kudumu katika kumswalia Mtume na katika utiifu, na si-

jaacha kuhudhuria katika vikao vya khitima tukufu ya kumswalia Mtume, basi milango ya kimaada na kimaanawi imeanza kufunguka mbele yangu zaidi na zaidi, kila ninavyozidi kujali kuhudhuria na kushindana. Na fadhila ya yote hayo baada ya Mwenyezi Mungu inarejea kwa aliyenitia moyo na aliyenishika mkono, al- Haji Fakhir Tehraniy ambaye alinihimiza katika kutafuta maarifa ya wigo wa utukufu na hadhi ya kitabu hiki kitukufu.

Kama ambavyo sisahau neema za Mwenyezi Mungu kwa wingi wa ndugu waumini walioshiriki katika vikao hivi, mmoja wao sikumoja alikuwa mgonjwa sana akawa anatawasali kwa khitima hii tukufu na baada ya muda mfupi yakatatuka matatizo yake kwa baraka na uangalizi wa wenye utajo huu, Muhammad na Aali zake, rehema za Mwenyezi Mungu ziwashukie wote.

Ndugu yenu mwenye kutambua fadhila za Mwenyezi Mungu, Mtume Wake (saww) na Aali zake (as) katika kutunga kitabu hiki, ana vitabu vingine vingi viko njiani kusambazwa, nitavitoa zawadi kwa Maasumina kumi na wanenye (as) kimoja baada ya kingine.

Na wakushukuriwa ni Mwenyezi Mungu, kwani mwanzo wa utunzi huo ulikuwa ni kitabu hiki *Hilul-Mushkilaati Bibarakati Swalawaati Alaa Muhammad wa Aalihi*, nacho kinakusanya matukio mengi yaliyowatokea baadhi ya waumini katika nyakati mbalimbali. Namuomba Mwenyezi Mungu Muweza kwa baraka za kumswalia Muhammad na Aali zake watukufu anikubalie bidhaa hii yenye mchanganyiko na amali hii chache, na anikunjulie kifua changu, anifanyie wepesi mambo yangu, aufungue mfundo wa ulimi wangu ili kauli yangu ifahamike kwa mapenzi ya Muhammad (saww) na kizazi cha Muhammad, huenda dua zao zitakuwa msaada kwangu, na naomba msaada na taufiki kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu.

**Mwenye kuwataja na kuwatumikia Ahlul-Bait,
Mwenye kumzuru Imam Husein (as),
Ali Khamsaiy al-Qaz'winiy,
Maarufu kwa jina la al-Hakim al-Hindiy.**

MANENO KATIKA KUMSWALIA MUHAMMADI (S.A.W.W.) NA AALI ZAKE (A.S.)

Miongoni mwa mambo mujarabu katika kutatua mambo muhimu, na katika njia mahususi ni kupata taufiki ya kumswalia Muhammad na Aali zake, kuandika maandishi yafuatayo na kuyanakshi katika karatasi ya rangi ya njano, na kuwa nayo wakati wote, nayo ni njia mujarabu isiyo na shaka inshaallah. Pia inasemekana kwamba maandishi haya ni katika majina ya Mwenyezi Mungu Mtukufu.²

Kumswalia Muhammad na Aali zake:

- Ni zawadi bora ya Mwenyezi Mungu kwa mwanadamu.
- Ni kati ya zawadi za peponi.
- Ni utakaso wa roho.
- Inafanya kinywa kuwa kizuri.
- Ni nuru katika Sirat.
- Ni uombezi kwa mwanadamu.
- Ni utajo wa Mwenyezi Mungu.
- Inapelekea Swala kukamilika.

² *Kauhar Shab Charagh*, cha Kifurusi Uk. 7

- Inapelekea dua kukamilika na kujibowi.
- Inapelekea mwanadamu kuwa karibu na Mwenyezi Mungu.
- Ni sababu ya kumuona Nabii (saww) katika ndoto.
- Ni kinga dhidi ya moto.
- Ni kiburudisho katika barzakh na Siku ya Kiyama.
- Ni kibali cha kupita katika Sirat kwenda peponi.
- Inamhakikishia mwanadamu uokovu katika ulimwengu tatu.
- Kwa Mwenyezi Mungu ni rehema, kwa Malaika ni utakaso kutokana na dhambi, na kwa watu ni dua.
- Ni bora zaidi na amali tukufu zaidi Siku ya Kiyama.
- Ni kitu kizito zaidi katika mizani.
- Ni amali inayopendwa zaidi.
- Inazima moto.
- Ni pambo la Swala.
- Inaondoa huzuni.
- Inafukuzia mbali ufakiri na madhambi.
- Ni dawa bora zaidi ya kiroho.³

Ni uzuri ulioje mtu kuwa mionganini mwa watu wenye kumswalia Muhammad na Aali zake! Na ni uzuri ulioje muumini kupamba mazingira ya kijamii na mazingira ya kazi yake kwa manukato ya kumswalia Muhammad na Aali zake!

³ Kama ambavyo tutasherehesha hayo yote na kutaja rejea zake katika kitabu hiki inshaallah.

- Kwa kumswalia Mtume na Aali zake ondoeni kwenu huzuni na majonzi.
- Kwa kumswalia Mtume na Aali zake mara moja iongezee nafsi yako nuru katika pepo.
- Kwa kumswalia Mtume na Aali zake mara moja takasika kutokana na dhambi zako zote na anza maisha upya.
- Kwa kumswalia Muhammad na Aali zake mara moja pata thawabu za mashahidi sabini na wawili.
- Na kwa kumswalia Muhammad na Aali zake mara moja sajili mema kumi katika daftari laamali zako.

DUA KATIKA MAPOKEZI YA AHLUL-BAITI (A.S.)

Imepokewa kutoka kwa Imam al-Baqir (as) kwamba amesema: “Ibada ndogo kabisa ni dua.”⁴

Basi muombeni Mwenyezi Mungu na itikieni wito wake ili mfaulu na muepukane na adhabu yake. Dua ni ibada, hivyo msii-ache kwa sababu ni njia bora zaidi ya kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu mtukufu. Na wala msijizue kuomba dua kwa udogo wa haja hakika mwenye kukidhi haja ndogo na kubwa ni mmoja, wala msi-choke kuomba hakika dua ina daraja kubwa mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Imepokewa kutoka kwa Imam as-Sadiq (as) kwamba amesema: “Asiyejiweza zaidi kati ya watu ni yule mwenye kushindwa kuomba, na bakhili zaidi kati ya watu ni yule mwenye kufanya ubakhili katika salamu.”⁵

Hakika majibu yamefichikana katika maombi kama ilivyofichikana mvua katika mawingu, na kama ambavyo mvua ni neema katika wakati wake vivyo hivyo majibu, na hivyo inapasa usikate tamaa Mwenyezi Mungu anapochelewa kujibu dua yako. Na katika maana hii ameashiria Imam al-Hujjah (a.s) katika dua yake: “Na huenda yaliyocheleweshwa kwangu ni bora kwangu kwa kuwa Wewe Ndiye wajua hatima ya mambo.”⁶

⁴ *Wasailu Shi'ah* cha Hurrul-Aamiliy aliyefariki 1104 A. H, chapa ya Muasasatu Aali Bait, Qum ya Mwaka 1409 A. H Juz.7, Uk. 30, Mlango wa 3 katika milango ya dua, hadith ya 8625.

⁵ *Wasailu Shi'ah* cha Hurrul-Aamiliy aliyefariki 1104 A.H chapa ya Muasasatu Aali Bait, Qum ya 1409 A.H. Juz. 7, uk. 28 mlango wa pili katika milango ya dua Hadith ya. 8616

⁶ *Mafatihul-Jinan* cha Shiekh Abbasiy al-Qummiy dua ya *Ifitaah* ya Imam al-Hujjah (aj).

Njooni enyi wapendwa tufanye dua kuwa ni sehemu ya maisha yetu ili tupate fadhila, uangalizi na huruma ya Mwenyezi Mungu, na kila mmoja wetu anapoona kwamba amefanikiwa kuomba basi ajue kwamba maana ya hilo ni kwamba milango ya rehema za Mwenyezi Mungu imefunguka mbele yake, dua yake ikikubaliwa basi ni pongozi kwake na isipojibwa basi ajue kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu atamlipa mambo matatu badala ya hayo:-

1. Mwenyezi Mungu atamlimbikizia neema atakazompa wakati wake ukifika.
2. Mwenyezi Mungu atamwepushia shari na balaa.
3. Ataijaalia dua yake kuwa ni kafara ya madhambi yake.

Hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa yaliyo katika nyoyo, ni Mwenye kusikia Mwenye kuona yuko karibu mno na sisi kuliko mshipa wa moyo, ni Mjuzi wa haja zetu tunazoziomba Kwake.

- Hakika nyakati bora zaidi kwa dua ni kabla ya kuchomoza jua na kabla ya kuzama kwake.
- Inapasa pasiwepo na kizuizi cha jambo lolote dhidi ya dua.
- Muombe Mwenyezi Mungu haja zako, hakika Yeye ni Muweza wa kuzikidhi Naye ndio amekuamuru hilo. Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: “**Niombeni nitakujibuni.**”⁷
- Omba haja zako kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu na wala usijipe njia ya kukata tamaa katika nafsi yako. Amesema Mwenyezi Mungu: “**Msikate tamaa na rehema za Mwenyezi Mungu.**”⁸

⁷ Suratu Ghaafir aya 60

⁸ Suratu Zumar aya ya 53

Imam Amirul-Muuminina (as) awe ni kigezo chako kwani ali-kuwa ni mwingi wa kuomba dua, naye (as) ndiye aliyesema: “Dua ni kinga kutokana na kila balaa.”⁹

Na ili ufile kwenye kusudio na lengo kuu usiache kuomba bali endelea kuomba katika njia za mlango wa Mwenyezi Mungu Mtukufu hadi ufunguliwe.

“Mimi sina hila zaidi ya kubisha hodi katika mlango Wako, nikikataliwa ni mlango upi nitabisha hodi”?

MIONGONI MWA MAANA ZA SWALA

Swala: Katika lugha ina maana ya dua, na neno hili limetumika katika Swala za kila siku kwa kuwa zinajumuisha pia dua, bali neno Swala katika jamii limetumika kwa kumaanisha moja kati ya mambو mawili:-

Kwanza: Dua maalum ambayo inamadhumuni ya kuomba cheo na kuzidi kuwa karibu na Nabii Muhammad (saww). Ama maana ya pili ni Swala ya kisharia ambayo ina rukuu na sijda, na kati ya Swala hizo ni Swala za kila siku.

Inaaminiwa kwamba neno Swala limenyambuliwa kutoka katika neno *Taswiliyatū* lenye maana ya kufuata, kwani Swala inafuata sharia tukufu. Na kwa ibara nyingine ya kina zaidi: Ni kumfuata Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Na baadhi wamesema: Hakika neno Swala limetokana na neno “*Swilatu*” yaani mafungamano ya mwenye kupenda kwa anayempenda. Swala ya kweli ni ile ambayo inampamba mwenye kuswali

⁹ *Wasailu Shi'ah* cha Hurru al- Aamili aliyefariki 1104 A. H chapa ya Muaasastu Aali Bait Qum 1409 A. H Juz, 5 uk: 91 mlango wa *istihbab istiswihaab al- aqiq fiy Du'a* Hadith ya 6014

wakati wa kuitekeleza kwa adabu ya hali ya juu na anawasiliana na Muumba Mtukufu peke yake.

Swala ni sababu ya ukuruba wa mja kwa Mungu Wake na kumswalia Muhammad na Aali zake ni sababu ya mafungamano ya mwenye kupenda kwa ampendaye, na mwenye kumpenda Muhammad na Aali zake (as) anafungamana nao mafungamano ya kweli na anaambatana na matawi ya mti wao kwa mafungamano ya milele.

Kama ambavyo baadhi wametaja maana tano ambazo zimenyambuliwa kutoka katika Aya tukufu za Mwenyezi Mungu: “**Yeye ni ambaye anawateremshieni rehema.**”¹⁰ Na kauli Yake (swt): “**Hao wanateremkiwa na rehema za Mola Wao.**”¹¹ Na kauli Yake (swt): “**Hakika Mwenyezi Mungu anamteremshia rehema na Malaika Wake wanamtakia rehema Nabii...**”¹²

Na maana hizi tano ni:-

Rehema, maghfira, sifa, utakaso na karama.

Baadhi ya maulamaa wamesema: “Hakika neno Swala limeundwa na herufi nne kama ifuatavyo:-

Swaad: ambayo imetokana na **Swamad** (Mwenye kukusudiwa), nalo ni katika majina ya Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Laam: ambayo imetokana na **Al-Latwif** (Mpole), nalo ni kati ya majina ya Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Waaw: ambayo imetokana na **al-Waahid** (Mmoja wa pekee), nalo ni kati ya majina ya Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Haau: ambayo imetokana na **al-Haadiy** (Mwenye kuongoza), nalo ni kati ya majina ya Mwenyezi Mungu Mtukufu.

¹⁰ Suratul- Ahzab aya ya 43

¹¹ Suratul- Baqara: 157

¹² Suratul- Ahzab: 56

Na baadhi yao wamesema: “Hakika Swala inamaana ya kujisal-imisha, nayo ni mja kuisalimisha nafsi yake na jambo lake kwa yule alijejaaliwa na Mwenyezi Mungu kuwa kiongozi wake na khalifa wa Nabii Wake.

Ama **Muhammad** inamaanisha anayesifiwa sana. Ni haki Muhammad asifiwe sana kwa kila sifa na kwa ajili hiyo Mwenyezi Mungu amemfanya kuwa ni makhususi kwa jina hili.

Na baadhi yao wamesema: **Muhammad** na **Ahmad** ni majina ambayo yamenyambuliwa kutoka katika neno *al-Hamiyd* na *al-Mahmuud*, na *al-Hamiyd* inamaana ya mwenye kusifiwa kwa wingi, na Mwenyezi Mungu Mtukufu ndiye Mwenye kusifu na Mwenye kusifiwa zaidi. Na amemfanya Nabii Wake Mtukufu kuwa ni mahussusi kwa majina haya matukufu yote mawili **Muhammad** na **Ahmad**, hivyo yeye (saww) katika daraja la kumsifu Mwenyezi Mungu Mtukufu ni **Ahmad**, yaani ni mwenye kusifu kwa wingi kumshinda kila mtu. Na katika daraja la kusifiwa yeye ni **Muhammad**, yaani yeye (saww) ni mwenye kusifiwa zaidi kuliko yeyote.

Sasa hivi tumekwishajua utukufu wa Nabii (saww) basi tueleze kwa muhtasari dondoor kutoka katika maisha yake matukufu.

DONDOD KUTOKA KATIKA MAISHA YA MTUKUFU MTUME (S.A.W.W.)

1. Jina lake ni Muhammad, Ahmad, Mahmud.
2. Cheo chake: Mwisho wa Manabii na Mitume.
3. Lakabu zake: al-Mustafaa, Habibullah, Rasullullah, na ana lakabu zaidi ya mia moja.
4. Jina lake la heshima: Ni Abul-Qasim, Abu Ibrahim, Abu Zahraa, na ana majina ya heshima zaidi ya tisa.
5. Jina la baba yake: Ni Abdullah.
6. Jina la mama yake: Ni Amina.
7. Tarehe ya kuzaliwa kwake: 17 Rabiul-Awwal, mwaka wa Tembo.
8. Sehemu aliyozaliwa: Makka tukufu.
9. Wakati wa kuzaliwa: Mapambazuko ya alfajiri.
10. Siku ya kuzaliwa: Ijumaa.
11. Tarehe ya kuo: 10 Rabiul-Awwal na umri wake wakati huo ulikuwa ni miaka 25 na umri wa mke wake Khadija ni miaka 40, watoto wake ni Qasim, Abdullah, Ibrahim, Zainab, Ummu Kuluthum, Ruqayyah na Fatimah.
12. Umri wake mtukufu ni miaka 63.
13. Muda wa utume wake ni miaka 23.
14. Tarehe ya kufa kwake shahidi ni 28 Safar kabla ya kuzama juu siku ya Jumatatu.

15. Sababu ya kufa shahidi: Alikula nyama ya mbuzi yenze sumu.
16. Aliyemuuwa: Mwanamke katika wanawake wa Kiyahudi wa Khaibari.
17. Mahala alipozikwa: Madina tukufu.
18. Nasaba yake kwa upande wa baba yake: Muhammad bin Abdullah bin Abdul-Mutalib bin Hashim bin Abdi Manafi, ambaye nasaba yake inafika kwa Ismail bin Ibrahim (as). Ama kwa upande wa mama yake ni Amina binti Wahhab bin Naufal bin Zahraa bin Kilaab.

SWALA YA MWENYEZI MUNGU KWA NABII (S.A.W.W.)

Amesema Mwenyezi Mungu (swt): “**Hakika Mwenyezi Mungu na Malaika wake wanamswalia Nabii enyi mliaoamini mswalieni na msalimieni na mtakieni amani.**”¹³

Hakika cheo cha bwana wetu Muhammad (saww) ni kitukufu na ni daraja la juu, hakika Mwenyezi Mungu na malaika wake wanamswalia na sisi tuliomwamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake pia tunamswalia pamoja nao.

KUHESABU THAWABU ZA KUMSWALIA MTUME NA AALI ZAKE

Imepokewa kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) kwamba amesema:

¹³ Suaratul- Ahzab: 56

“Nilipelekwa usiku wa miraji hadi mbinguni, nilimuona Malai-ka ana mikono elfu moja kila mkono una vidole elfu moja, naye anahesabu kwa vidole hivyo, nikamwambia Jibril, Malaika huyu ni nani na nini anakihesabu? Akasema: ‘Malaika huyu nimwangalizi wa matone ya mvua anajua ni matone mangapi yameteremka toka mbinguni kwenda ardhini.’ Nikamwambia Malaika: Wewe unajua tangu Mwenyezi Mungu ameumba du-nia ni matone mangapi yameteremka toka mbinguni kwenda ardhini? Akasema: ‘Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, naapa kwa ambaye amekutuma kwa haki kwa viumbe Vyake, mimi ninajua ni matone mangapi yameteremka toka mbinguni kwen-da ardhini, najua kwa ufanuzi ni matone mangapi yameshuka nchi kavu na matone mangapi yameteremka baharini, ni matone mangapi yameteremka katika majumba na matone mangapi yameteremka katika bustani, na matone mangapi yameteremka katika ardhi ya chumvi na matone mangapi yameteremka katika makaburi.’ Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akastaajabu kuhifadhi na kukumbuka kwake hesabu yake. Akasema: ‘Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungui la kuna hesabu nisiyoiweza kui-hifadhi pamoja na kumbukumbu niliyonayo, mikono na vidole nilivyonyavyo!’ Akasema ni hesabu gani hiyo? Akasema: ‘Kau-mu katika umma wako wanahudhuria kikao na linapotajwa jina lako na wanakuswalia, mimi siwezi kuhesabu thawabu zao.”¹⁴

MALIPO YA KUMSWALIA MTUME NDANI YA KITABU

Imepokewa kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) kwamba amesema:

¹⁴ *Mustadrakul-Wasa'il* cha Nuriy aliyefariki 1320H chapa ya Muasasatu Aali Bait Qum 1408 A. H Jz. 5, uk: 355 mlango wa *Wujubu swalat alaa Nabiyi (saww)* kulama dhukra wa wujuba swalatu alaa *Aalihi ma'a swalatu alaihi* Hadith ya. 8 katika mtiririko ni ya 6072

“Mwenye kuniswalia katika kitabu Malaika hawataacha ku-muombea maghfira maadamu tu jina langu lipo katika kitabu hicho.”¹⁵

MWENYE KUNYIMWA HARUFU YA PEPO

Kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) kwamba amesema:

“Mwenye kuniswalia bila kuwaswalia Ahali zangu hatopata harufu ya pepo na hakika harufu yake inapatikana katika umbali wa mwendo wa miaka mia tano.”¹⁶

RADHI ZA MOLA NA UTAKASO WA AMALI

Imepokewa kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) kwamba amesema:

“Kuniswalia kwenu mimi ni kuzipasisha dua zenu, ni kumridhisha Mola wenu na ni utakaso wa amali zenu.”¹⁷

¹⁵ *Biharul-Anwaar* cha Allammah al-Majilisiy aliyefariki 1110 chapa ya Muasasatu al-Wafaai Qum Beirut 1404 A. H. Juz. 91, uk: 71 Hadith ya 65 mlango wa 29 *Fadhil swalat alaa Nabiyyi (saww) wa Aalihi*

¹⁶ *Wasailu Shi'ah* cha Hurrul-Aamly chapa ya Muasasati Aali bait Qum 1309 A. H. Jz. 7, uk: 203 Hadith 9117 mlango wa 142 *Wujubu swalati alaa Nabiyyi (saww) wa wujubu swalati alaa Aalihi ma'a swalati alaihi*

¹⁷ *Jamaalul- Usubu'i* cha Sayid Ibnu Twawusi aliyefariki 664 A. H kimesambazwa na Daru Ridhaaa Qum uk: 241 yametajwa tunayoyapokea juu ya fadhil swalati alaa Nabyyi (saww)

SWALA ILIYO SAWA NA SWALA ELFU KUMI

Alikuja mtu kwa Sultan Mahamud Sabakatikiyn na akamwambia: "Ni muda mrefu nilikuwa natamani kumuona Nabii katika ulimwengu wa ndoto na kumweleza matatizo yangu lakini sikupata bahati hiyo hadi usiku uliopita ambapo nilipata utukufu huu, nikamzuru na nikashuhudia uzuri wake na ukamilifu wake katika ulimwengu wa ndoto na nikamwambia: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) hakika mimi ninadaiwa dirhamu elfu kumi na siwezi kuzilipa na naogopa kunifika mauti na deni hili likawa katika dhima yangu. Akaniambia (saww): 'Nenda kwa Mahamud Sabakatikiyn na uchukue kiasi hicho.' Nikamwambia: Naogopa kwamba hatoniamini na atanitaka dalili. Akasema (saww): 'Mwambie dalili ni kwamba wewe unamswalia Mtume mwanzo wa usiku mara elfu thalathini na katika mwisho wake mara elfu thalathini.'

Sultani Mahamud aliposikia ndoto hii alilia na akaisadikisha, na akampa kiasi hicho na dirahamu 1000 zingine. Waliohudhuria wakastaajabu na wakasema: 'Ewe Sultani vipi unasadikisha maneno ya huyu mtu na sisi tulikuwa pamoja na wewe mwanzo wa usiku na mwisho wake na hatujakuona unashughulika na uradi na lau yejote akidumu katika utajo huu usiku na mchana asingeweza kufikisha elfu sitini!'

Sultani Mahmud akasema: 'Nimesikia kutoka kwa Maulamaa kwamba kuna Swala ya Nabii ambayo mwenye kumswalia mara moja ni kana kwamba amemswalia mara elfu kumi na mimi nimekariri Swala hii mara tatu mwanzo wa usiku na katika mwisho wake mara tatu na huyu mtu ni mkweli katika mazungumzo yake na Swala hiyo ni hii:-

اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى سَيِّدِنَا وَنَبِيِّنَا مُحَمَّدٍ وَآلِهِ مَا اخْتَلَفَ الْمُلْوَانِ
وَتَعَاقَبَ الْعَصْرَانِ وَكَرِّ الْجَدِيدَانِ وَاسْتَقْبِلْ الْفَرْقَادَانِ وَبَلِّغْ
رُوحَهُ وَارْوَحْ أهْلِ بَيْتِهِ مِنْيَ التَّحِيَّةِ وَ السَّلَامِ.¹⁸

“Ewe Mwenyezi Mungu mswalie Muhammad na Aali Muhammad kadiri mchana na usiku upishanavyo, kadiri asubuhi na jioni zipishanavyo, na kadiri urejeavyo tena usiku na mchana, na kadiri zichomozavyo tena nyota. Na ifikishie roho yake na roho za watu wa nyumbani kwake, maamkizi na salamu kutoka kwangu.”

KULIPA DENI KUPITIA KUMSWALIA MTUME NA AALI ZAKE

Mmoja kati ya wale wenyekujinyima dunia alikuwa anadaiwa dirham mia tano, akamuona Nabii (saww) katika ndoto, Nabii (saww) akamwambia:

“Nenda kwa Abu Hasan al-Kisaiy – na alikuwa nikati ya watu mashuhuri huko Nisaburina kila mwaka alikuwa anawavika nguo mafakiri elfu kumi-na mwambie: Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) anakusalimu na anasema, lipa deni la mtu huyu, na akikutaka dalili inayothibitisha ukweli wako mwambie: Dalili ni kwamba wewe unamswalia mara mia moja kila usiku na imeshapita kwako mikesha miwili bila wewe kumswalia.’

Mchamungu huyu alikwenda kwa Abu Hasan al-Kisaiy na akamweleza ndoto yake lakini hakumjali. Mchamungu huyu

¹⁸ *Khutumu wa adhikaar shifaai – cha Kifurusi - uk: 316*

akasema: Na dalili yangu ni kadhaa wakadhaa. Al-Kisaiy aka-poromoka kutoka kwenye kiti na akasujudu kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu na akasema: ‘Hii ni siri baina yangu na Mwenyezi Mungu Mtukufu, haijui yejote na hakika imeafikiana, hakika mimi nimesahau utajo huu mtukufu tangu usiku wa siku mibili.’ Kisha akaamuru mtu huyu apewe dirihamu 2,500 na akasema: ‘Ama elfu ya kwanza ni kwa ajili ya bishara ambayo ameniletea kutoka kwa Nabii (saww), na ama elfu ya pili ni kwa ajili ya hatua zake za kuja kwetu, na ama mia tano ni kwa ajili ya kutii amri ya Nabii (saww).’ Kisha akamwambia mchamungu huyo, ‘kila utakapokuwa na haja basi utujie.’”¹⁹

MGONJWA APONA KUPITIA KUMSWALIA MUHAMMADI NA AALI ZAKE

Mwanamke alitaka ponyo kwa mtoto wake kipofu na kiziwi kutoka kwa Nabii (saww). Akamwambia nenda na uniswalie kwa wingi. Mwanamke akarejea katika nyumba yake huku akimswalia Muhammad (saww) na Aali zake (a.s.) kwa kila hatua anayotembea. Alipofika katika nyumba yake akamuona mtoto wake yuko salama na ameshapona. Akarejea kwa Nabii (saww) na akampa habari ya kupona kwa mtoto wake. Jibril akateremka kwa Nabii (saww) na akamwambia: “Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema: Kama alivypo-ponya mtoto huyu kwa baraka za kukuswalia wewe na Aali zako vivyo hivyo nitasamehe Siku ya Kiyama madhambi ya umma wako kwa baraka za kukuswalia wewe na Aali zako.”²⁰

¹⁹ *Kaakh nashinaan* cha Kifurusi

²⁰ *Kaakh nashinaan* cha Kifurusi

MADHAMBI YAFUTWA KUPITIA KUMSWALIA MUHAMMADI NA AALI ZAKE

Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww): “Mwenye kuniswalia mara moja haitobaki hata chembe katika madhambi yake.”²¹

MADHAMBI HUCHELEWESHWA KUANDIKWA

Imepokewa kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) kwamba amesema:

“Haniswalii yejote mara moja na akawasikilizisha Swala hiyo Malaika wenye kumchunga isipokuwa hawatomwandikia dhambi kwa muda wa siku tatu.”²²

KUSAMEHEWA DHAMBI

Imepokewa kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) kwamba amesema:

“Mwenye kuniswalia kila siku mara tatu na kila usiku mara tatu kwa ajili yakunipenda na kuwa na shauku na mimi ni haki ya Mwenyezi Mungu Mtukufu kumsamehe dhambi za usiku huo na siku hiyo.”²³

²¹ *Jaami 'ul-Akhbaar*, Taaj Diyn Shi'iriy chapa ya Dar Ridhaa Qum 1405 A. H fasil ya 28 fiy swalati alaa Nabiyyi (saww) uk: 59

²² *Jaami 'ul-Akhbaar*, Taaj Diyn Shi'iriy chapa ya Dar Ridhaa Qum 1405 A. H fasil ya 28 fiy swalati alaa Nabiyyi (saww) uk: 59

²³ *Mustadrakul-Wasa 'il cha Nuriy* chapa ya Muasasati Aali Bait Qum 1408 A. H. Jz. 5, uk: 331 malngo wa 31 *Istihbabil- ikithaaari min swalati alaa Muhammad wa Aalihi* (saww) Hadith no 6) ya 6015 katika mtirirko

KUSAMEHEWA DHAMBI ZA MIAKA THAMANINI

Imepokewa kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) kwamba amesema:

“Mwenye kuniswalia siku ya Ijumaa mara mia moja atasame-hewa dhambi za miaka themanini.”²⁴

KUSAMEHEWA DHAMBI KADIRI ZIWAVYO

Imepokewa kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) kwamba amesema:

“Hakuna yejote katika umma wangu anayenitaja na kuniswalia isipokuwa Mwenyezi Mungu atamsamehe madhambi yake hata kama ni mfano wa mchanga wa A’liji.”²⁵

²⁴ *Mustadrakul-Wasail* cha Nuriy chapa ya Muasasati Aali Bait Qum 1408 H juz 6 uk: 72 malngo wa 35 *Istihabil- ikithaari min swalati alaa Muhammadwa Aali Muhammad (saww) fiy lailatil- Jumu’ati wa yaumihi* Hadith namba 8 ya 6467 katika mtirirko.

²⁵ *Irishadul-Qulub* cha Dailamiyaliyefariki 841 A. H. chapa ya Daru Sharifu RidhaaQum 1413 A. H. Jz. 1, uk: 190 mlango wa 52 *Fiy Hadith muntakhabah*. Na inasemekana kwamba Ramlu Aaliji ni milima iliyoquatana katika urefu wake huko Dahanaai karibu na Yamaamatii na ni chini ya Najid

INATIA UZITO KATIKA MIZANI

Imepokewa kutoka kwa Nabii (saww) kwamba amesema:

“Mimi nitakuwa katika mizani Siku ya Kiyama, basi ambaye mabaya yake yatakuwa mazito kuliko mema yake nitakuja na Swala yangu ili niongeze uzito katika mema yake.”²⁶

REHEMA ZA MWENYEZI MUNGU KWA MWENYE KUMSWALIA NABII

Imepokewa kutoka kwa Imam as-Sadiq (as) kwamba amesema:

“Anapotajwa Nabii (saww) basi mswalieni kwa wingi hakika mwenye kumswalia Nabii mara moja Mwenyezi Mungu anam-rehemu mara elfu moja katika safu elfu moja za Malaika, na hakitabaki kitu katika alivyoumba Mwenyezi Mungu isipokuwa kitamuombea rehema mja kwa ajili ya Mwenyezi Mungu kumteremshia rehema na Malaika kumuombea rehema.”²⁷

MABAYA KUMI HUFUTWA KWA BARAKA ZA SWALA MOJA

Imepokewa Kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) kwamba amesema:

²⁶ Wasailu Shi'ah cha Hurrul-Aamly chapa ya Muasasati Aali Bait Qum 1309 A. H. Jz, 7, uk: 195 Hadith 9097 mlango wa 34 istihbab ikithaari min swalaati alaa Muhammad wa Aalihi (saww) wa ikhitiyariha alaa maa siwaaha

²⁷ Al-Kaafy cha Thiqatul-Islaaam al-Kullainy aliyefariki 329 A. H chapa ya Darul-Kutubi al-Islamiyati Tehran 1365H Jz. 2, uk: 492 mlango wa Swalati alaa Nabiyyi Muhammad wa Ahli-Baytih (saww), Hadith ya 6.

“Mwenye kuniswalia mara moja Mwenyezi Mungu anamteremshia rehema za kuniswalia mara kumi na atasamehewa makosa kumi na atanyanyuliwa daraja kumi.”²⁸

KUMSWALIA NABII NI KINGA DHIDI YA MOTO

Imepokewa kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) kwamba amesema:

“Mwenye kuniswalia mara moja Mwenyezi Mungu anamteremshia rehema mara kumi, na mwenye kuniswalia mara kumi Mwenyezi Mungu anamteremshia rehema mara mia moja, na mwenye kuniswalia mara mia moja Mwenyezi Mungu anamteremshia rehema mara elfu moja, na mwenye kuniswalia mara elfu moja Mwenyezi Mungu hatomwadhibu kwa moto abadani.”²⁹

KUBASHIRIWA PEPO

Imepokewa kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) kwamba amesema:

“Mwenye kuniswalia siku ya Ijumaa mara mia moja atakuja siku ya Kiyama na usoni mwake kuna nuru, na mwenye kuniswalia siku ya Ijumaa mara elfu moja hatokufa hadi aone makazi yake peponi.”³⁰

²⁸ *Mustadrakul-Wasaili* cha Nuriy chapa ya Muasasati Aalil-Bayt Qum 1408 A. H juz 5 uk: 337 mlango wa 31 Hadith ya. 33 ya 6042 katika mtiririko

²⁹ *Mustadrakul-Wasaili* cha Nuriy chapa ya Muasasati Aalil-Bayt Qum 1408H juz 5 uk: 351 mlango wa 34 Hadith ya 1 ya 6064 katika mtiririko

³⁰ *Mustadrakul-Wasaili* Jz. 6, uk: 72 mlango wa 35 Hadith namba 7 ya 6466 katika mtiririko

MALIPO YA MASHAHIDI SABINI NA WAWILI

Imepokewa kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) kwamba amesema:

“Mwenye kusema Allahumma swali alaa Muhammad wa Aali Muhammad, Mwenyezi Mungu anampa malipo ya mashahidi sabini na wawili, na anatoka katika dhambi zake kama vile siku aliyozaliwa na mama yake.”³¹

MAANA YA DHIKRI

Kutoka kwa Ubaidullah bin Abdillah bin Dahqaan amesema:

“Niliingia kwa Abul Hasan Ridhaa (as) akaniambia: Nini maana ya kauli yake (swt): “**Akalitaja jina la Mola Wake na kuswali:**” (**Sura A’alaat: 18.**) Nikasema: Kila anapotaja jina la Mola Wake anasimama na kuswali. Akaniambia. ‘Mwenyezi Mungu amekalifisha haya bila kuvuka mpaka.’ Nikasema. Niwe fidia kwako basi ni nini maana yake? Akasema: ‘Kila anapotaja jina la Mola Wake anamswalia Muhammad (saww) na Aali zake.’”³²

SIRI ILIYOPELEKEA WANA WA ISRAIL KUONDOLEWA MATESO

Imepokewa kutoka kwa Imam Abu Muhammad al-Askariy (as) katika kauli yake (swt):

“Na vile tulipokuokoeni kwa watu wa Firaun waliokupeni ad-habu mbaya” Akasema (as): “Na ilikuwa mionganini mwa ad-

³¹ *Mustadrakul-Wasaili* Jz. 5, uk: 335 mlango wa 31 Hadith ya 18 ya 602 katika mtiririko

³² *Al-Kafiy* cha Kullainiy chapya Darul-Kutubil-Islamiyatii Tehran 1365 A. H. Jz. 2, uk: 494 mlango wa swalati alaa Nabiyyi Muhammad (saww) wa Ahali Baithi Hadith namba 11

habu yao kali ni kwamba Firaun alikuwa anawapa kazi ya kujenga kwa udongo na kwa kuwa alikuwa anaogopa wasikimbie kazi aliamuru wafungwe minyororo, na walikuwa wanasonba udongo huo wakiwa katika minyororo hadi juu napaa, na kuna wakati mmoja wao anaanguka na kufa au kulemaa bila kuwajali, hadi alipompelekea Musa (as) wahyi awaambie wasianze kazi isipokuwa kwa kumswalia Muhammad na Aali zake wema ili wafanyiwe tahafifu, hivyo wakawa wanafanya hivyo na wanafanyiwa tahafifu. Na akamwamuru kila anayeanguka na kulemaa kati ya waliosahau kumswalia Muhammad na Aali zake wema aseme hivyo katika nafsi yake akiweza, yaani amswalie Muhammad na Aali zake au wamsomee ikiwa hawezi, naye atasimama bila kusimamishwa, wakafanya hivyo basi wakasalimika.”

Na katika kauli yake (swt): “**Wakiwachinja wana wenu wa kiume,**” akasema:

“Na hiyo ni alipoambiwa Firaun kwamba atazaliwa mtoto katika Bani Israil na ataangamia katika mikono yake, akaamuru kuchinjwa watoto wao wa kiume, hivyo kila mmoja kati yao alikuwa anaweka wakunga yeche binafsi ili asijulikane, ukitimia ujauzito wake humtupa mtoto wake jangwani au katika pango la mlima au sehemu isiyojulikana, na humswalia Mtume Muhammad na Aali zake mara kumi, na hapo Mwenyezi Mungu humletea Malaika ambaye humlea na hutoa maziwa katika vidole na mtoto hunyonya, na katika vidole hutoka pia chakula laini ambacho mtotohula, hadi Bani Israil wakakua, na waliosalimika na kukua ni wengi zaidi kuliko waliouliwa.”

Na (as) katika kauli yake (swt): “**Na wanawaacha hai wanawake wenu**” akasema:

“Wanawataka na wanawafanya vijakazi, wakapiga kelele kwa Musa (as) wakasema: Wanawafanya mabaya mabinti zetu na

dada zetu, Mwenyezi Mungu akawaamuru mabinti hao kila wanapopatwa na tatizo hilo wamswalie Muhammad na Aali zake wema basi walikuwa wanazuia wanaume hao ama kwa kupewa kazi au kwa kuugua au kwa kuzimia au kwa huruma kati ya huruma yake, na hakuudhiwa kati yao mwanamke bali Mwenyezi Mungu Mtukufu alizuia hayo kwao kwa kumswalia Muhammad na Aali zake wema. Kisha Mwenyezi Mungu Mtukufu akasema: “**Hayo kwenu**” katika kuwanusuru huko ambako amekunusuruni kutoka kwao Mola wenu “**balaa**” neema “**adhimu kutoka kwa Mola wenu**” kubwa. Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu “**Enyi bani Israil kumbukeni**” wakati balaa inaondolewa kwa waliowatangulia na inapungua kwa kumswalia Muhammad na Aali zake wema, je hamjui kwamba nyinyi mtakapomuna na kumwamini itakuwa ni neema bora kwenu, na ni fadhila ya Mwenyezi Mungu Mtukufu kwenu.”³³

SABABU YA KUJIBIWA DUA

Amesema Imam as-Sadiq (as):

“Mwenye kuwa na haja kwa Mwenyezi Mungu basi na aanze kwa kumswalia Muhammad na Aali zake kisha aombe haja yake kisha amalizie kwa kumswalia Muhammad na Aali zake, hakika Mwenyezi Mungu ni Mtukufu mno hawezi kukubali sehemu mbili: ya mwanzo na ya mwisho, kisha aache kukubali katikati yake, ambapo Swala ya Mtume haina kizuizi.”³⁴

³³ *Mutadrakul-Wasail* cha ya Muasasti Aalil-Bait, Qum 1408 A. H. Jz. 5, uk: 339 mlango wa 31 Hadith ya 35 namba 7045 katika mffululizo

³⁴ *Al-Kafiy* ya Kullainiy chapa ya Darul-Kutubil-Islamiyati, Tehran 1365 A. H. Jz 2, uk: 494 malango wa *swalati alaa Nabiyyi Muhammad wa Ahali baitihi (saww)*, Hadith ya 16

SWALA ILIYO SAWA NA HIJA SABINI

Kutoka kwa Abu Baswiri amesema:

“Nilimsikia Abu Abdillah (as) anasema: Kumswalia Muhammad na Aali zake baina ya Dhuhri na Laasiri ni sawa na Hija sabini.”³⁵

KUKIDHI HAJA ZA DUNIA NA AKHERA

Imepokewa kutoka kwa Imam as-Sadiq (as) kwamba amesema: “Mwenye kusema mara moja baada ya Alfajiri na baada ya Swala ya Magharibi kabla ya kunyanya miguu yake au kabla ya kuongea na yejote:

إِنَّ اللَّهَ وَمَلَائِكَتَهُ يُصَلُّونَ عَلَى النَّبِيِّ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا صَلُوْرٌ
عَلَيْهِ وَسَلَّمُوا تَسْلِيمًا
اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدِ النَّبِيِّ وَ عَلَى ذُرِّيَّتِهِ وَ عَلَى أَهْلِ بَيْتِهِ

“Hakika Mwenyezi Mungu na malaika Wake wanamswalia Nabii. Enyi ambao mmeamini! Mswalieni na mumsalimu kwa salamu. Ewe Mwenyezi Mungu mswalie Muhammad Nabii, na dhuria wake na watu wa nyumbani kwake.”

³⁵ Wasailu Shi'ah ya Hurrul-Aamiliy chapa ya Muasasti Aalil-Baiti, Qum, 1409A. H. Jz. 7, uk: 400 Hadith ya 9686 mlango wa 48 (Maa yustahabu an yugraa wa yuqaalu aqiybul-Jumuati wal- Asri)

Mwenyezi Mungu atamkidhia haja mia moja, sabini kati yake ni za Akhera na thelathinini za duniani.³⁶

MADHAMBI HUPUKUTIKA KWA KUMSWALIA NABII NA AALI ZAKE

Kutoka kwa Imam Ridhaa (as) kwamba amesema:

“Asiyeweza kafara ya dhambi zake basi amswalie Muhammad na Aali zake kwa wingi, kwani inapukutisha kabisa madhambi.”³⁷

MSISITIZO JUU YA KUMSWALIA MUHAMMADI NA AALI ZAKE

Amepokea Alhaji Nuriy kutoka kwa Alhaji Sheikh Ahmad bin Sheikh Zainu Diyn, amesema:

“Nilibahatika kukutana na Imam Zainul-Abidin (as) katika ulimwengu wa ndoto, siku moja nikamuuliza: Bwana wangu nini nifanye ili niwe kati ya wenye kukumbuka daima kaburi na Kiyama? Bwana wangu nini nifanye ili nifanikiwe kutubu na kutekeleza amali njema na ili niimarishe nyumba yangu ya Akhera? Akasema (as): ‘Ukitaka kupata taufiki na mafanikio jilazimishe daima kusema: Allahumma Swali Alaa Muhammad wa Aali Muhammad.’”³⁸

³⁶ *Mustadrakul-Wasail* chapa ya Muasasati Aalil-Bait Qum, 1408A. H. Jz: 5, uk: 100 mlango wa 26 (*Nubdhatu mimmaa yustahabu an yuzaada fiy taaqiybil- Magharibwal- Ishaai*) Hadith ya 6 ya 5436 katika mtiririko

³⁷ *Mustadrakul-Wasail* chapa ya Muasasati Aalil-Bait Qum, 1408 A. H. Jz: 7, uk: 195 mlango wa 34 Hadith 9390 katika mtiririko

³⁸ *Daru Salaam* uk: 123

SWALA YA MTUME HUONDOA UFAKIRI

Imepokewa kutoka kwa Nabii (saww) kwamba:

“Kumswalia Muhammad na Aali zake kunaondoa ufkiri.”³⁹

SWALA YA MTUME HUTAJIRISHA

Kati ya siri za Swala ya Mtume (s.a.w.w.) ni kwamba ikisomwa kwa ajili ya Akhera msomaji wake anapata daraja nyingi za kiroho na akizisoma kwa ajili ya dunia anapata utajiri. Ama namna yake ni kusoma mara 10 asubuhi na mara 10 jioni. Ama kuhitimisha kwake ni mara 99, na haya ni matamko yake:

اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى سَيِّدِنَا وَحْبِبِنَا وَشَفِيعِنَا مُحَمَّدٍ، حَمَّا الرَّحْمَةِ
وَمِيمِ الْمُلْكِ وَدَالِ الدَّوَامِ ، السَّيِّدِ الْكَامِلِ الْفَاتِحِ. الْخَاتِمِ كُلَّمَا
ذَكَرَكَ وَذِكْرُهُ الْذَّاكِرُونَ ، وَ كُلَّمَا سَهَا وَغَفَلَ عَنْ ذِكْرِكَ
وَذِكْرِهِ الْغَافِلُونَ، صَلَّاةً دَائِمَةً بَدَوَ امِكَ بَاقِيَةً بِبَقَائِكَ لَا مُنْتَهَى
لَهَا دُونَ ذَلِكَ وَعَلَى اللَّهِ وَأَصْحَابِهِ كَذَلِكَ إِنَّكَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ
قَدِيرٌ وَبِالإِجَابَةِ جَدِيرٌ⁴⁰

³⁹ Dastanahaaiy swalawaati – cha kifursi – yaani kisa cha swalawaati uk: 97

⁴⁰ Athaaru wabarakaatu swalawaati cha Kifursi uk: 44

INASAIIDIA KUWA NA KUMBUKUMBU

Imepokewa kutoka kwa Nabii (saww) kuwa alisema:

“Hakika kumswalia Muhammad na Aali zake kunasaidia kuwa na kumbukumbu.”

NI DAWA YA KUTIBU UFAKIRI

Kutoka kwa Sahli bin Sa’ad as-Sa’adiy amesema:

“Alikuja mwanaume mionganini mwa Answari kwa Nabii (saww), akamshitakia ufakiri na dhiki ya maisha, Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akamwambia ukiingia nyumbani kwako salimia ikiwa humo kuna yejote na kama hakuna yejote humo basi niswalie na soma Surat Ikhlasi mara moja. Mwanaume huyo akafanya hivyo, basi Mwenyezi Mungu akamkun-julia riziki na akampanulia hadi akawakunjulia na jirani zake.”⁴¹

BISHARA KWA MWENYE KUMSWALIA NABII NA AALI ZAKE

Kutoka kwa Abdullah bin Sanaan kutoka kwa Abu Abdillahi as-Sadiq (as) amesema:

“Nabii (saww) siku moja alimwambia Ali (as): Ewe Ali je, ni-kubashirie? Akasema: ‘Ndio, naapa kwa baba yangu na mama yangu hakika wewe hujaacha kuwa ni mbashiri kwa kila kheri.’ Akasema (saww): Amenipa habari Jibril punde tu kwa kuniam-

⁴¹ Mustadrakul-Wasail chapa ya Muasasati Aalil-Bayt Qum, 1408AH. Jz: 4, uk: 289 mlan-go wa 24 (*Istihbab ikithaari min qiraatil- Ikhlaswi ...*) Hadith ya 10 ya 4712 katika mtiririko

bia yale yanayostaajabisha! Ali akasema: ‘Ni habari ipi amekupa ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu?’ Akasema: Amenipa habari kwamba mtu katika umma wangu akiniswalia na akafuatilizia Swala yangu kwa kuwaswalia Ahlul-Baiti wangu anafunguliwa milango ya mbinguni, na Malaika wanamtakia rehema sabini, na kwamba kama yeye ni mwenye dhambi na makosabasi yatapukutika kwake madhambi kama yanavyopukutika majani kutoka kwenye mti. Mwenyezi Mungu Mtukufuatasema: ‘Labaika na wema ni wako ewe mia Wangu. Enyi Malaika wangu nyinyi mnamtakia rehema mara sabini na mimi namteremshia rehema mia saba.’ Na akiniswalia na wala asifuatilizie kwa kuwaswalia Ahlul-Baiti wangu basi kutakuwa na vizuizi sabini baina yake na mbingu, na Mwenyezi Mungu atamwambia: ‘Huitikiwi wala hunawema ewe mia Wangu, enyi malaika Wangu msinyanyue dua yake ila akiambatanishwa Nabi Wangu na kizazi chake.’ Haitaacha kuwa ni yenyе kuzuiliwa hadi niambatanishwe na Ahlul-Baiti wangu.”⁴²

KUNUSA MANUKATO KWA KUMSWALIA MUHAMMADI (SAWW) NA AALI ZAKE (A.S.)

Kutoka kwa Malik al-Juhaniy amesema:

“Nilimpatia Abu Abdillah manukato, akayachukua akayanusa na akayaweka baina ya macho yake kisha akasema: ‘Mwenye kupokea manukato na akayanusa na akayaweka baina ya macho yake kisha akasema: Allahumma Swal Alaa Muhammad Wa Aali Muhammad hayatoanguka ardhini hadi asamehewe.’”⁴³

⁴² *Mustadrakul-Wasail* chapa ya Muasasati Aalil-Bayt Qum, 1408 A. H Jz: 5, uk: 354 mlango wa 35 Hadith ya 1 ya 6065 katika mtiririko

⁴³ *Wasailu Shi'ah* cha Hurrul-Aamiliy chapa ya Muasasati Aalil-Bayt Qum, Jz. 2, uk: 171 mlango 114 (*Istihbab taqbiyl al- ward wa rayaahiy ... wa swalati alaa Muhammad wa Aali Muhammad*, Hadith, ya 1849 ka katika mtiririko)

KUMSWALIA MUHAMMADI (SAWW) NA AALI ZAKE BAINA YA DHUHRI NA LAASRI

Imepokewa kutoka kwa Imam as-Sadiq (as) kwamba amesema:

“Mwenye kumswalia Muhammad na Aali zake baina ya Dhuhri na Laasiri inakuwa ni sawa na rakaa sabini.”⁴⁴

MWENYE SHAUKU YA KUMDIRIKI AL-QAIM (AF)

Imepokewa kutoka kwa Imam as-Sadiq (as) kwamba amesema: “Mwenye kusema baada ya Swala ya Alfajri na baada ya Swala ya Dhuhri:

اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَآلِ مُحَمَّدٍ وَعجلْ فِرْجَهُمْ

Hatakuwa mpaka amdiriki Mwakilishi wa Aali Muhammadi (a.s.)⁴⁵

SHARTI LA KUJIBIWA DUA

Imepokewa kutoka kwa Imam Amirul-Muuminina (as) kwamba amesema:

“Kila dua inazuiliwa hadi aswaliwe Muhammad na kizazi cha Muhammad.”⁴⁶

⁴⁴ *Mustadrakul-Wasail* chapa ya Muasasati Aalil-Bayt Qum, 1408 A. H Jz: 6, uk: 97 mlango wa 40 (*Maa yustahabu an yuqraa wa yuqaalu fiy aqiybl- Jumuati wal- Asri*) Hadith ya 16 ya 6520 katika mtiririko

⁴⁵ Rejea ya juu Jz. 5, uk: 96 mlango wa 24 Hadith ya 5 ya 5426 katika mtiririko

⁴⁶ *Biharul-Anwar* cha Allammah al-Majilisi chapa ya Muasasatil-Wafaai Beirut 1404AH. Jz. 27, uk: 260 mlango wa 15 (*Aswalaati alaihim swalawatullahi alaihim*) Hadith ya 15

KUONDOA KIZUIZI KINACHOZUIA DUA KUJIBIWA

Imepokewa kutoka kwa Imam a-Sadiq (as) kwamba amesema:

“Hakuna dua isipokuwa baina yake na baina ya mbingu kuna kizuizi hadi aswaliwe Muhammad na kizazi cha Muhammad,(a.s) na anapofanya hivyo dua inapenya kizuizi na kuingia na asipofanya hivyo dua hainyanyuliwi.”⁴⁷

KUMWIGA IMAM RIDHAA (A.S.)

Kutoka kwa Rajaa Dhahak amesema kuwa:

“Hakika Imam Ridhaa (as) alikuwa anaanza katika dua yake kwa kumswalia Muhammad na Aali zake na anazidisha katika hilo katika Swala na kwingineko.”⁴⁸

KUMUONA NABII (SAWW) KATIKA NDOTO

Amesema al-Kafa’amiy katika sharhi ya kitabu *al-Mis’baha*; Imekuja katika kitabu cha *Khuwaswil-Qur’an*:

“Mwenye kusoma usiku wa Ijumaa baada ya Swala ya usiku Surat al-Kawthar mara elfu moja kisha akamswalia Muhammad na Aali zake mara elfu moja hakika atamuona katika ndoto.”⁴⁹

⁴⁷ *Mustadrakul-Wasail* chapa ya Muasasati Aalil-Bayt Qum 1408A. H Jz: 5, uk: 225 mlango wa 34, Hadith ya 5, ya 5748 katika mtiririko

⁴⁸ *Uyunul-Akhbar Ridhaa (as)* cha Sheikh Suduuq chapa ya Darul-Aalaam kwa usambazaji 1378 A. H. Jz. 2, uk: 182 mlango wa 44 *fity dhikri akhilaaqihi al- kariyamati*

⁴⁹ *Daru Salaam* Jz 3 uk:6

SIRI YA KUMUONA NABII (SAWW) KATIKA NDOTO

Imekuja katika kitabu *Jadhibul-Qulub* cha Abdil-Haqad-Dahlawiy: “Kuna njia moja tu ya kumuona Nabii (saww) katika ndoto, nayo ni kudumu katika kumswalia yeze (saww) na Aali zake huku ukiwa na tohara, utamswalia kwa kusema:

اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَآلِهِ كَمَا تُحِبُّ وَتُرْضِي⁵⁰

FURAHA YA NABII KWA KUMSWALIA YEYE

Alionwa mmoja kati ya waja wachamungu siku moja amekaa katika kona akishiriki katika moja ya vikao vya muhadhara, wahudhuriaji wakastaajabu na baadhi wakamuuliza sababu ya kuhudhuria kwake, akasema: Nilimuona Nabii (saww) katika ndoto akaniamuru kuhudhuria majilisi ya khatibu huyu na akasema: “Hakika yeze ananiswalia kwa wingi na mimi niko radhi naye.”⁵¹

MALAIKA ALIYE AMRIWA KUMFIKISHIA NABII (SAWW) SWALA

Imepokewa kutoka kwa Imam as-Sadiq (as) kwamba amesema:

“Mwenyezi Mungu amemuweka Malaika anayeyitwa Dhihlil katika kaburi la Nabii (saww), mmoja wenu anapomswalia na kumsalimia anamwambia ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu fulani amekusalimia na amekuswalia. Akasema basi Nabii anajibu salamu.”⁵²

⁵⁰ *Daru Salaam* Jz. 3, uk: 7

⁵¹ *Athaaru wa barakaatu swalawati – cha Kifurusi – uk: 87*

⁵² *Mustadrakul-Wasail* chapa ya Muasasati Aalil-Bayt Qum 1408 A. H. Jz: 5, uk: 330 mlango wa 31 Hadith ya 5 ya 6014 katika mtiririko

MTU AMBAYE NABII ANATAJWA KWAKE NA WALA ASIMSWALIE

Imepokewa kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) kwamba amesema:

“Ambaye natajwa kwake na wala asinwalie ataingia motoni, na Mwenyezi Mungu amuweke mbali.”⁵³

MATOKEO YA KUTOKUJALI

Imepokewa kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) kwamba amesema:

“Imedhalilika pua ya mtu ambaye ninayetajwa mbele yake na wala asinwalie.”⁵⁴

MALIPO YA ASIYEMSWALIA MTUME (SAWW)

Kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) amesema kwamba:

“Mtu ambaye nitatajwa mbele yake na akaniswalia na wala asi-samehewe basi Mwenyezi Mungu amuweke mbali.” Ikasemwa: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu vipi anakuswalia na wala asisamehewe? Akasema: “Hakika mja anaponiswalia na

⁵³ Rejea ya juu juz 6 uk: 408 mlango wa 10 (*Wujubu swalati alaa Muhammad wa Aalihii*) Hadith ya 8299

⁵⁴ *Biharul-Anuwar* chapa ya Muasasatil-Wafaai Beirut 1404 A. H. Jz. 94 uk: 80 mlango wa 56 *fadhailu shahari Shaaban wa swiyaamihii* Hadith 47

asiwaswalie Aali zangu Swala hiyo inageuzwa na anapigwa nayo usoni mwake, na akiniswalia na akawaswalia Aali zangu anasamehewa.”⁵⁵

MSIKOSEE NJIA YA KUELEKEA PEPONI

Imepokewa kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) kwamba amesema:

“Yeyote ambaye nitatajwa mbele yake na akasahau kuniswalia basi ajue kuwa anapotezwanja ya kuelekea peponi.”⁵⁶

SWALA KIGUTU

Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww):

“Msiniswalie Swala kigutu.” Akaambiwa ni ipi Swala kigutu? Akasema: “Nikusema: ‘Allahumma Swali Alaa Muhammad’na mkanyamaza. Bali semeni: ‘Allahumma Swali Alaa Muhammad wa Aali Muhammad.’”⁵⁷

NYAKATI ZA KUMSWALIA MTUME (SAWW)

Imepokewa kutoka kwa Imam as-Sadiq (as) kwamba amesema:

“Hakika inapoingia siku ya Ijumaa huteremka Malaika kutoka mbinguni kwa idadi ya chembe ndogo, na katika mikono huwa wamebeba kalamu za dhahabu na karatasi za fedha, hawaandiki hadi usiku wa Jumamosi isipokuwa thawabu tu za kumswalia Muhammad na Aali zake (as), basi mswalieni kwa wingi.”⁵⁸

⁵⁵ *Wasailu-Shi'ah*, Jz. 7, uk: 203, Hadith 9117 katika mtiririko.

⁵⁶ Al Kafiy juz 2 uk: 495 Malango waAswalatu alaa Nabiyyi wa Ahali baitihi Hadith 19

⁵⁷ *Al-Hadaaiqu Nnaadhiratu*, Jz, 8.uk: 365

⁵⁸ *Al-Kafiy* cha Kullainiy chapa ya Darul-Kutubil-Isalamiyat Tehran 1365 Jz. 3, uk: 416 mlango wa *Fadhilu yaumil- Jumauati walaiatalihi* Hadith ya 13

SUNNAH YA KUMSWALIA NABII (SAWW) SIKU YA IJUMAA

Imepokewa kutoka kwa Imam as-Sadiq (as) kwamba amesema:

“Hakika ni Sunnah kumswalia Muhammad na Ahlul-Baiti wake kila siku ya Ijumaa mara elfu moja, na katika siku zingine mara mia moja.”⁵⁹

AMANI BAINA YA IJUMAA

Imepokewa kutoka kwa Imam Ja’far bin Muhammad kutoka kwa baba zake (as) amesema:

“Mwenye kusema mara tatu baada ya Dhuhri ya siku ya Ijumaa:

اللَّهُمَّ اجْعِلْ صَلَوَاتَ مَلَائِكَتِكَ وَرَسُلِكَ عَلَىٰ مُحَمَّدٍ
وَآلِ مُحَمَّدٍ وَعَجْلَ فَرْجَ آلِ مُحَمَّدٍ

basi itakuwa ni amani kwake baina ya Ijumaa mbili.”⁶⁰

AMANI YA MWAKA MZIMA

Imepokewa kutoka kwa Imam as-Sadiq (as) kwamba amesema:

“Mwenye kusema siku ya Ijumaa baada ya Swala ya Subhi:

⁵⁹ Rejea iliyotangulia

⁶⁰ *Mustadrakul-Wasail* chapa ya Muasasati Aalil-Bayti 1408 A. H. Jz. 6, uk: 97 mlango 4 Hadith 40 ya 6521 katika mtiririko

اللهم اجعل صلواتك و صلوات ملائكتك و حمله عرشك
و جميع خلقك و سمائك و ارضك و انبيائك و رسليك على
محمد و آل محمد.

hatoandikiwa dhambi mwaka mzima.^{”⁶¹}

HAKUNA SWALA BILA YA KUMSWALIA MUHAMMAD NA AALI ZAKE

Imepokewa kutoka kwa Imam as-Sadiq (as) kwamba amesema:

“Mwenye kuswali na wala asiniswalie na akaacha hayo kwa makusudi basi hana Swala. Hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu ameanza kwa Swala yangu kabla ya Swala Yake, amesema: Hakika amefaulu aliyejitatasa na akataja jina la Mola Wake kisha akaswali.”^{”⁶²}

NURU YA KUMSWALIA MUHAMMADI NA AALI ZAKE (A.S.)

Imepokewa kutoka kwa Imamas-Sadiq (as) kwamba amesema:

“Sadaka ya usiku wa kuamkia Ijumaa na siku yake ina thawabu elfu moja, na Swala ya kumswalia Muhammad na Aali zake

⁶¹ Biharul-Anuwar chapa ya Muasastil-Wafai Beirut 1404 Jz 86 uk: 354 malngo wa Aamalu yaumil- Jumuati

⁶² Tahadhibul-Ahkami, cha Sheikh Tusi chapa ya Najaf ul-Ashraf Darul kutubil-Islamiyat Tehran 1365, Jz. 2, uk: 159 mlango 9 Tafswil maa taqadama dhikruhu fiy swalati Hadith ya 83

usiku wa kuamkia Ijumaa ina mema elfu moja, na Mwenyezi Mungu hufuta humo makosa elfu moja, na hunyanyua humo daraja elfu moja, na hakika mwenye kumswalia Muhammad na Aali zake usiku wa kuamkia Ijumaa nuru yake inaangaza mbin-guni hadi siku kitakaposimama Kiyama.”⁶³

AMALI BORA ZAIDI KATIKA SIKU YA IJUMAA

Aliulizwa Imam as-Sadiq (as) kuhusu amali bora zaidi siku ya Ijumaa, akasema:

“Sijui amali bora zaidi kuliko kumswalia Muhammad na Aali zake.”⁶⁴

SWALA YA SHAABANIYYAH, INAYOSOMWA KILA SIKU NDANI YA MWEZI WA SHABANI

Katika kitabu *Mis’bahul-Mujtahid* imepokewa kutoka kwa Mujahid kutoka kwa baba yake amesema: Ali bin Husein (as) alikuwa anaomba baada ya kupetuka jua katika siku za Shaban na katika nusu yake na anamswalia Nabii kwa Swala hii:

اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَآلِ مُحَمَّدٍ، شَجَرَةَ النُّبُوَّةِ، وَمَوْضِعِ الرِّسَالَةِ، وَمُخْتَلِفِ الْمَلَائِكَةِ، وَمَعْدِنِ الْعِلْمِ، وَأَهْلِ بَيْتِ الْوَحْىِ،

⁶³ Wasailu shi’ah chapa ya Muasasati Aalil-Bayt Qum 1409 A. H. Jz. 7, uk: 413 mlango 55 (*Istihbab swadagati yaumul-Jumuati* Hadith ya 9729)

⁶⁴ Tawailul-Ayaati al-dhahirati, uk: 454 Suratul-Ahzab - wa maa fiyha minal-Ayaati

اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَآلِ مُحَمَّدٍ الْفُلُكِ الْجَارِيَةِ فِي الْجَحِّ
 الْغَامِرَةِ، يَأْمُنُ مَنْ رَكِبَهَا، وَيَغْرِقُ مَنْ تَرَكَهَا، الْمُتَقَدِّمُ لَهُمْ
 مَارِقُ، وَالْمُتَاخِرُ عَنْهُمْ زَاهِقُ، وَاللَّازِمُ لَهُمْ لَاحِقُ، اللَّهُمَّ صَلِّ
 عَلَى مُحَمَّدٍ وَآلِ مُحَمَّدٍ، الْكَهْفِ الْحَصِينِ، وَغِيَاثِ الْمُضْطَرِّ
 الْمُسْتَكِينِ، وَمَلْجَأِ الْهَارِبِينَ، وَعِصْمَةِ الْمُعْتَصِمِينَ، اللَّهُمَّ
 صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَآلِ مُحَمَّدٍ صَلَاةً كَثِيرَةً، تَكُونُ لَهُمْ رِضاً
 وَلِحَقٌّ مُحَمَّدٍ وَآلِ مُحَمَّدٍ أَدَاءً وَقَضَاءً، بِحَوْلِ مِنْكَ وَقُوَّةِ يَا رَبِّ
 الْعَالَمِينَ، اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَآلِ مُحَمَّدٍ، الطَّيِّبِينَ الْأَبْرَارِ
 الْأَخْيَارِ، الَّذِينَ أَوْجَبْتَ حُقُوقَهُمْ، وَفَرَضْتَ طَاعَتَهُمْ وَلَا يَتَّهِمُونَ،
 اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَآلِ مُحَمَّدٍ، وَاعْمِرْ قَلْبِي بِطَاعَتِكَ،
 وَلَا تُخْزِنِي بِمَعْصِيَتِكَ، وَارْزُقْنِي مُواسَةً مَنْ قَتَرْتَ عَلَيْهِ مِنْ
 رِزْقِكَ بِمَا وَسَعْتَ عَلَيَّ مِنْ فَضْلِكَ، وَنَشَرْتَ عَلَيَّ مِنْ عَدْلِكَ،
 وَأَحْبَيْتَنِي تَحْتَ ظِلِّكَ، وَهَذَا شَهْرُ نَبِيِّكَ سَيِّدِ رُسُلِكَ، شَعْبَانُ
 الَّذِي حَفَّتَهُ مِنْكَ بِالرَّحْمَةِ وَالرَّضْوَانِ، الَّذِي كَانَ رَسُولُ اللهِ
 صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ يَدْأُبُ فِي صِيَامِهِ وَقِيَامِهِ فِي لَيَالِيهِ

وَأيَّامِهِ بُخُواً لَكَ فِي إِكْرَامِهِ وَإِعْظَامِهِ إِلَى مَحْلٍ حِمَامِهِ،
اللَّهُمَّ فَاغْنِنَا عَلَى الْأَسْتِنَانِ بِسُنْتِهِ فِيهِ، وَنَذِلِ الشَّفَاعَةَ لَدَيْهِ،
اللَّهُمَّ وَاجْعِلْهُ لِي شَفِيعاً مُشَفَّعاً وَطَرِيقَاً إِلَيْكَ مَهِيئاً، وَاجْعَلْنِي
لَهُ مُتَبَّعاً حَتَّى الْقَالَ يَوْمَ الْقِيَامَةِ عَنِي راضِياً، وَعَنْ ذُنُوبِي
غاضِياً، قَدْ أَوْجَبْتَ لِي مِنْكَ الرَّحْمَةَ وَالرَّضْوَانَ، وَأَنْزَلْتَنِي
دارَ الْقُرْارِ وَمَحْلَ الْأُخْيَارِ.

“Ewe Mwenyezi Mungu! Msalie Muhammadi na Aali Muhammadi, mti wa unabii, maweko ya utume, mapishano ya malaika, mgodi wa elimu na watu wa nyumba ya wahyi. Ewe Mwenyezi Mungu msalie Muhammadi na Aali Muhammadi, meli itembeayo ndani ya bahari kuu, husalimika yule mwenye kuipanda na hughariki yule mwenye kuiacha. Hupotea yule mwenye kuwatangulia, huhiliki yule mwenye kubakia nyuma mbali nao, na hupata heshima yao yule mwenye kuandamana nao. Ewe Mwenyezi Mungu msalie Muhammadi na Aali Muhammadi ambao ni ngome imara, msaada kwa mwenye shinda aliye mnyonge, kimbilio la wenyekukimbia na ni ulinzi wa wenyekushikamana nao. Ewe Mwenyezi Mungu msalie Muhammadi na Aali Muhammadi sala nyingi watakazokuwa radhi nazo, na zitaka-zokuwa utekelezaji na ulipaji wa haki zao, kwa nguvu na uwezo toka Kwako ewe Mola Mlezi wa viumbe vyote. Ewe Mwenyezi Mungu msalie Muhammadi na Aali Muhammadi wazuri, was-afi na wema, ambao umewajibisha haki zao na umefaradhisha kuwatii na kuwapenda. Ewe Mwenyezi Mungu msalie Muhammadi na Aali Muhammadi na amirisha moyo wangu kwa kukutii Wewe na wala usinifedheheshe kwa kukuasi Wewe, na

niruzuku moyo wa kumhurumia yule uliyembania riziki Yako, nimhurumie kuititia fadhila Zako ulizonipanulia, uadilifu Wako ulioueneza juu yangu na uhai ulionipa chini ya kivuli Chako. Huu ni mwezi wa Nabii Wako bwana wa Mitume Wako, Shabani ambayo umeijaza rehema na radhi kutoka Kwako, ambayo Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) alikuwa akiitumia kwa kufunga mchana na kuamka kufanya ibada usiku kwa ajili ya kukutii Wewe katika kuiheshimu (Shabani) na kuitkuza mpaka alipoondoka katika dunia hii. Ewe Mwenyezi Mungu! Tusaidie kufuata mwenendo wake humu na kupata uombezi wake. Ewe Mwenyezi Mungu! Na mfanye mwombezi wangu mwenye kukubaliwa na njia yangu rahisi ya kukufikia Wewe, na nijaalie niwe mfuasi wake mpaka nikutane Nawe Siku ya Kiyama na hali umeniridhia na dhambi zangu umezipuuza, baada ya kuni-pa rehema na radhi kutoka Kwako na kunifikisha katika makazi ya kudumu na mahala pa watu wema.”⁶⁵

ORODHA YA HERUFI ZA MAJINA YA MAASUMINA KWA AJILI YA KUKHITIM- ISHIA

Jina tukufu la Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) ni Muhammad:
92

Jina tukufu la Amirul-Muumina ni Ali (as): 110

Jina tukufu la Bibi Zahraa (as) ni Fatma: 135

Jina tukufu la mjukuu al-Mujtabaa (as) ni Hasan: 118

Jina tukufu la bwana wa Mashahidi (as) ni Husein: 128

Jina tukufu la Zainul-Abidn (as) ni Ali: 110

⁶⁵ Wasailu Shi'ah chapa ya Muasasti Aalil-Bayt Qum 1409 A. H. Jz. 10, uk: 492 mlango 28 (*Istihbab swaum Sha'aban kullahu au ba'adhu*), Miswibahu al-mutahjid cha Tusiy Muasasatil-fiqihi shi'ah Beirut 1411A. H. *Maa yuqalu fiy kulli Shaabani* uk: 28

- Jina tukufu la Imam al-Baqir (as) ni Muhammad: 92
Jina tukufu la Imam as-Sadiq (as) ni Ja'far: 353
Jina tukufu la Imam al-Kadhim (as) ni Musa: 116
Jina tukufu la Imam Ridhaa (as) ni Ali: 110
Jina tukufu la Imam al-Jawad (as) ni Muhammad: 92
Jina tukufu la Imam al-Hadi (as) ni Ali: 110
Jina tukufu la Imam al-Askariy (as) ni Hasan: 118
Jina tukufu la Imam al-Muntadhar (as) ni Mahdi: 59.⁶⁶

KUKHITIMISHA KUMSWALIA MUHAMMAD (SAWW) NA AALI MUHAMMAD (AS)

Miongoni mwa khitma walizopendelekeza Maimam na kuzipa umuhimu mkubwa ni khitma ya kumswalia Muhammad na Aali zake (a.s.), kwani hakuna mgonjwa aliyetawasali kwayo kwa Mwenyezi Mungu isipokuwa Mwenyezi Mungu alimponya ugonjwa wake. Na katika kitabu *Jamiul-Akhbar* imeandikwa kuwa hakika Nabii (saww) amesema: “Mwenye kuniswalia mara moja Mwenyezi Mungu humfungulia mlango wa afya.”⁶⁷

Imepokewa kutoka kwa Imam as-Sadiq (as) kwamba amesema:

“Mwenye kumswalia Nabii na kizazi chake na Ahlul-Bait wake Mwenyezi Mungu anamkidhia haja mia moja, sabini kati ya hizo ni za Akhera na thelathini ni za kidunia.”⁶⁸

⁶⁶ Atharu wa Barakatu Swalawati, uk: 123

⁶⁷ *Jamiul-Akhbar*, Taaji Diyn Shaiyriy chapa ya Daru Ridhaa Qum, 1405 A. H. uk: 59 al-faswil 28 fty swalati alaa Nabiyyi wa aalihii

⁶⁸ *Mustadrakul-Wasail* chapa ya Muasasti Aalil-Bayt Qum, 1408 A. H. Jz. 5, uk: 100 mlang'o 26 Hadith 6 ya 5436 katika mtiririko

ADABU ZA KUZINGATIWA WAKATI WA KUKHITIMISHA SWALA YA MTUME (SAWW)

1. **Twahara:** Hakika kati ya masharti ya kukubaliwa dua, nyiradi na khitma ya Swala ya kumswalia Mtume ni twahara ya mwili na roho.
2. **Kutotamani yaliyopo mikononi mwa watu:** Kati ya masharti ya kujibiwa dua ni kutomtegemea asiyekuwa Mwenyezi Mungu kiasi kwamba mwenye kufanya uradi awe ni mwenye kuambatana naye peke Yake, na kwa ajili hiyo imepokewa kutoka kwa Imam as-Sadiq (as) kwamba amesema: “Kutotamani yaliyopo katika mikono ya watu ni utukufu kwa muumini katika dini yake.”⁶⁹
3. **Yakini:** Na kati ya masharti ya kujibiwa dua ni muombaji awe mwenye kukumbuka na mwenye yakini kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu ni Muweza wa yote anayoyataka.
4. **Dua ya mwenye kughariki:** Na katika mashrti ya kujibiwa dua vilevile ni dua ya muombaji iwe kama vile dua ya mwenye kughariki, ambaye haoni njia ya kunusurika isipokuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, kwani imepokewa kwamba Mwenyezi Mungu alimwambia Isa bin Mariam (as): “Ewe Isa niombe dua ya mwenye kughariki mwenye huzuni ambaye hana wa kumnusuru.”⁷⁰
5. **Kumsifu Mwenyezi Mungu:** Inapasa kwa muombaji aanze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu na kumsifu; Imepokewa

⁶⁹ *Al-Kafiy cha Kullainiy chapa ya Darul-Kutubil-Islamiyati Tehran, 1365 Jz. 2, uk: 148*
mlango wa al-Istighnai an-Naasi Hadith 4

⁷⁰ *Biharul-Anuwar chapa ya Muasasatil-Wafai Beirut 1404 A. H. Jz. 90, uk: 341 Hadith 65*
mlango wa 20 – Raghabatu warahabtu watadharu ‘u Hadith 12

kutoka kwa Imam as-Sadiq (as) kwamba amesema: “Anapotaka mmoja wenu kumuomba Mola wake kitu kati ya haja zake za kidunia au za akhera basi ajilazimishe kwa kuanza kuomba kwa kumsifu Mwenyezi Mungu Mtukufu na kumshukuru na kumswalia Nabii (saww) kisha amuombe Mwenyezi Mungu haja zake.”⁷¹

6. **Kukiri dhambi na kuomba msamaha:** Hakika katika dhambi kuna ambayo yafanya moyo kuwa mweusi na inazuia dua. Muombe Mwenyezi Mungu msamaha kwayo, na uchache wa kuomba msamaha ni kusema: ‘Namuomba Mwenyezi Mungu msamaha na ninatubia kwake.’ mara sabini.
7. **Kuitakasa nafsi na kuuhudhurisha moyo:** Ukitakasa moyo wako kutohana na najisi na kila kinachoambatana nao miongoni mwa matamanio ya kinafsi na ukauhudhurisha moyo, itapatikana kwako hali kamili ya kuhudhuria katika makusudio. Imepokewa kutoka kwa Imam Zainul-Abidin (as) kwamba amesema: “Haikubaliwi katika Swala ya mja isipokuwa kile alichohudhurisha moyo humo.”⁷²
8. **Nia ya moyoni:** Hakika kati ya adabu muhimu za nyuradi, takhitimu na tawasuli ni nia ya moyoni ambayo isipopatikana hakika utajo wa kweli hautopatikana, kuna faida gani kuushughulisha ulimi kwa utajo wakati moyo umeghafilika nao kwa mambo mengine. Na hapa inapasa kujitahidi kuhakikisha nia ya moyoni inapatikana wakati wa uradi, tawasuli na dua; Vivyo hivyo katika kumswalia Mtume (saww) kama ilivyopokewa kutoka kwa Maimam (as).

⁷¹ *Al-Kafiy cha Kullainiy* chapa ya Darul-Kutubil-Islamiyat Tehran, 1365 A. H. Jz. 2 uk: 484 malango wa *Thanai qabla du'ai* Hadith 1

⁷² *Mustadrakul-Wasail* chapa ya Muasasti Aalil-Bayt Qum, 1408 A. H. Jz. 3, uk: 56 mlango 16 (*Taukiyd istihbab al-mudaawamati ala nawaafil*) Hadith ya 2 no 3008

9. **Wakati:** Kila baadhi ya nyuradi na Swala zinapopangwa kwa namna maalum vivyo hivyo hupangiwa wakati maalum, mfano baina ya mapambazuko au baada ya Swala ya Alfajir au baada ya Maghribi au baada ya Laasiri, siku ya Alhamisi au siku na usiku wa Ijumaa, vivyo hivyo kulingana na miezi inayofaa na yenye ubora zaidi.
10. **Kuhesabu:** Hakika kuchagua idadi katika kusoma uradi au takhitim inazingatiwa kuwa ni katika hukumu muhimu ambazo inapasa kuziangalia, yaani ni lazima kuzihusisha na idadi hiyo ambayo wametamka na wameiainisha Maasumina (as) kama ilivyopokewa katika kumswalia Muhammad na Aali zake katika sehemu zingine: mara tatu, na sehemu zingine mara kumi au mara mia moja au mara elfu moja.”⁷³

AINA ZA KUKHITIMISHA SWALA ZA MTUME (SAWW)

Mwenye kutaka kujua namna ya kukhitimisha Swala ya kumswalia Muhammad na kizazi cha Muhammad ni lazima aanze kulingana na hali zifuatazo:

1. Kumswalia mara 14 yaani kwa idadi ya herufi za Swala zenyewe.
2. Kumswalia kwa hesabu ya idadi ya jumla ya Abjadiya ya Swala zenyewe, yaani mara 557.

⁷³ Hususan masharti kumi yaliyotangulia tazama: *Biharul-Anwar* chapa ya Muatasatil-Wafai Beirut, 1404 A. H. Jz. 91, uk: 71 mlango wa 29; na Jz. 27, uk: 260 mlango wa 15; na Jz. 86, uk: 354 mlango wa 4, *Al-Jawahir saniiyyati* mlango wa 10 Hadith 17, *Al-Kafiy* Jz. 2, uk: 491- 495 mlango wa *Swalatu alaa Muhammad wa Ahli baitihi*, *Thawabul- Aamali wa Iqaabul- Aamali* cha sheikh Suduqu uk: 153 – 159, *Jamiul-Akhbar*, *Tuju Diyni* uk: 58-65, faswil ya 28, *Risalatu nuur alaa nur* uk: 53 *Jamalul-Usubu*’i cha Asad bin Tausi uk: 183.

3. Kumswalia kwa hesabu ya idadi ya jumla ya herufi za mmoja wa Maasumina (as), na tumeshatangulia kutaja hesabu hiyo katika kitabu hiki. Mfano ukitaka kutoa zawadi thawabu za Swala zako kwa Imam Husein (as) inapasa kumswalia Muhammad na Aali zake mara 128, yaani kwa idadi ya jumla ya idadi ya herufi za jina la Imam Husein (as).
4. Ikiwa khitma ni kwa ajili ya kuomba haja na kuondoa ugonjwa na huzuni hapa hakuna idadi maalum na hivyo inapasa idadi iwe mara 92, yaani kwa idadi ya jumla ya herufi za jina la Nabii (saww) au mara 110 yaani kwa idadi ya jumla ya herufi za jina la Imam Amirul-Muuminina (as).
5. Na ikiwa ni haja binafsi basi ni bora kuchagua idadi ya jumla ya idadi ya herufi za jina la mtu mwenyewe, na ikiwa anataka apeleke thawabu zake kwa wafu wake basi jumla ya idadi ya herufi za jina la marehemu.⁷⁴

NJIA YA KUKHITIMISHA

1. Mtu anuie, kwa mfano: Nitakapokidhiwa haja yangu fulani nitamswalia Muhammad na Aali zake mara 14,000 na kila elfu moja kati yake ni zawadi kwa mmoja wa Ma'asumina kumi na nne (as), atakapokidhiwa haja yake ni lazima atekeleze.
2. Mtu amswalie Muhammad na Aali zake kila siku mara elfu moja na kutoa zawadi thawabu zake kwa mmoja wa Maasumina kumi na nne (as) hakika atapata haja yake ndani ya muda huo au baada yake.
3. Mtu amswalie Muhammad na Aali zake kila siku mara elfu moja kwa muda wa mwezi moja hakika atakidhiwa haja yake inshallah baada ya kumalizika mwezi.

⁷⁴Atharu wabarakaatu swalawat uk: 114- 115

4. Imejaribiwa kwa ajili ya kukidhi haja na kulipa deni kuanzia usiku wa Ijumaa kwa muda wa wiki mbili kwa namna ifuatayo: Mwenye kufanya uradi afanye amali hii baada ya usiku wa manane na aoge katika usiku wa kwanza:

Katika usiku wa kwanza: Usiku wa Ijumaa anasema mara elfu moja: “Allahumma Swali Alaa Muhammad Wa Aali Muhammad”

Katika usiku wa pili: Usiku wa Jumamosi anasema mara elfu moja: “Allahumma Swali Alaa Ali Amirul-Muuminina”

Katika usiku wa tatu: Usikuwa Jumapili anasema mara elfu moja: “Allahumma Swali Alaa Fatmatiz Zahraa.”

Katika usiku wa nne: Usiku wa Jumatatu anasema Mara elfu moja: “Allahumma Swali Alaaal-Hasan.”

Katika usiku watano: Usiku wa Jumanne anasema mara elfu moja: “Allahumma Swali Alaa al-Husein.”

Katika usiku wa sita: Usiku wa Jumatano anasema mara elfu moja: “Allahumma Swali Alaa Ali binHusein.”

Katika usikuwa saba: Usiku wa Alhamisi anasema mara elfu moja: “Allahumma Swali Alaa Muhammad bin Ali.”

Katika usikuwa nane: Usiku wa Ijumaa anasema mara elfu moja: “Allahumma Swali Alaa Ja’far bin Muhammad.”

Katika usiku wa tisa: Usiku wa Jumamosi anasema mara elfu moja: “Allahumma Swali Alaa Musa bin Ja’far.”

Katika usiku wa kumi usiku wa Jumamosi anasema mara elfu moja: “Allahumma Swali Alaa Ali bin Musa.”

Katika usiku wa kumi na moja usiku wa Jumapili anasema mara elfu moja: “Allahumma Swali Alaa Muhammad bin Ali.”

Katika usiku wa kumi na mbili usikuwa Jumatatu anasema mara elfu moja: “Allahumma Swali Alaa Ali bin Muhammad.”

Katika usiku wa kumi na tatu usiku wa Jumanne anasema mara elfu moja: “Allahumma Swali Alaal Hasan bin Ali.”

Katika usiku wa kumi nanne usiku wa Jumatano anasema mara elfu moja: “Allahumma Swali Alaa Hujjat bin Hasan.”

Katika usiku wa kumi na tano usiku wa Ijumaa anasema mara elfu moja: “Allahumma Swali Alaa Abbas Shahid.”⁷⁵

KHITMA AROBAINI

Katika faslu hii tunaashiria khitma arobaini ambazo tumezichambua kutoka katika rejea za Kiislamu. Inapendeza kufanya khitma hizi katika hali ya twahara pamoja na kuhudhurisha moyo.⁷⁶

1. Utasoma Bismillahi Rahmani Rahimi mara 786, yaani kwa idadi ya Maasumina kwa idadi ya herufi za Bismillahi. Kisha unamswalia Muhammad na kizazi cha Muhammad mara 132, hakika utakapofanya hivyo utakidhiwa haja yako inshallah.⁷⁷

⁷⁵ *Athar wa barakaatu Swalawaatu* uk: 117

⁷⁶ Hadiyatun khudaa cha Kifurusi 134

⁷⁷ Sirul-Mustatir uk: 63

2. Kwa ajili ya kupata utukufu mswalie Muhammad na Aali zake mara kumi kila siku⁷⁸
3. Imepokewa kutoka kwa Imam as-Sadiq (as) kwamba amesema:

“Mwenye kusema mara moja baada ya Swala ya Alfajir na baada ya Swala ya Maghrib kabla ya kunyanyuka miguu yake au kuzungumza na yejote:

إِنَّ اللَّهَ وَمَلَائِكَتَهُ يُصَلُّونَ عَلَى النَّبِيِّ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا صَلُوْا
عَلَيْهِ وَسَلِّمُوا تَسْلِيمًا
اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدِ النَّبِيِّ وَ عَلَى ذُرِّيَّتِهِ وَ عَلَى أَهْلِ بَيْتِهِ

“Hakika Mwenyezi Mungu na malaika Wake wanamswalia Nabii. Enyi ambao mmeamini! Mswalieni na mumsalimu kwa salamu. Ewe Mwenyezi Mungu mswalie Muhammad Nabii, na dhuria wake na watu wa nyumbani kwake.”

Mwenyezi Mungu anamkidhia haja mia moja, sabini kati ya hizo ni za akhera na thelethini ni za duniani.”⁷⁹

4. Kati ya khitma zilizomujarabu ambazo zina athari kubwa katika kukidhi haja, ni khitma ya kumswalia Muhammad na Aali zake, nayo ni mujarabu kwa ajili ya kukidhi haja, kuondoa balaa, kunuurika kutohana na maumivu na taabu na kufikia makusudio

⁷⁸ Athar wa barakaatu Swalawaatu uk:116

⁷⁹ Mustadrakul-Wasail cha Nuriy chapa ya Muasasti Aalil-Bayt Qum 1408H Jz: 5, uk: 100 mlango 26 (Nubdhatu mimmaa yustahabu an yuzaada fiy taaqiybil-Maghrib wall-Ishaa) Hadith ya 6, na ya 5436 katika mtirirko.

na maombi, nayo ni kumswalia Muhammad na Aali zake mara 14,000 kwa namna ifuatayo:

Kwanza unatawadha unaweka manukato katika mdomo wako kwa maji ya waridi, kisha unasoma Swala za hazina ya siri mara tatu, na baada yake unamswalia Muhammad na Aali zake mara 14,000 kwa nia ya Maasumina kumi na nne kwa taratibu, yaani unatoa kila thawabu elfu moja kwa Maasum kwa kuanzia na Nabii (saww) na kumalizia na al- Huffajt (as).

Ama Swala ya hazina ya siri ni hii:

اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى سَيِّدِنَا وَحَبِيبِنَا وَشَفِيعِنَا مُحَمَّدٍ، حَمَّاء الرَّحْمَةِ وَمِيمِ
الْمُلْكِ وَدَائِلِ الدَّوَامِ ، السَّيِّدِ الْكَامِلِ الْفَاتِحِ . الْخَاتِمِ كُلُّمَا ذَكَرَكَ
وَذَكْرُهُ الذَّاكِرُونَ ، وَكُلُّمَا سَهَا وَغَلَّ عَنْ ذِكْرِكَ وَذَكْرِهِ الْغَافِلُونَ ،
صَلَاةً دَائِمَةً بَدَأْتِكَ بِقِيَةً لَبِقَائِكَ لَا مُنْتَهَى لَهَا دُونَ ذَلِكَ وَعَلَى اللَّهِ
وَأَصْحَابِهِ كَذَلِكَ إِنَّكَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ وَبِالإِجَابَةِ جَدِيرٌ⁸⁰

5. Imepokewa kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) kwamba amesema: “Mwenye kuniswalia mara mia moja anaki-dhiwa haja mia moja.”⁸¹
6. Kwa ajili ya kuponya wagonjwa waliokatiwatamaa kupona kwao na ambao wamerejeshwa na matabibu, inapasa kumswalia Muhammad na Aali zake kwa wingi. Na ni bora zaidi kumswalia hivi:

⁸⁰ Athaaru wabarakaatu Swalawaati cha kifursi uk: 44

⁸¹ Sunanu Tirimidhiy Jz. 1, uk: 303

اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَآلِ مُحَمَّدٍ كَمَا بَارَكْتَ عَلَى إِبْرَاهِيمَ.⁸²

7. Kwa ajili ya kundoa ufakiri na umasikini imepokewa kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) kwamba amesema:
“Zidisheni utajo wa Mwenyezi Mungu Mtukufu na kumswalia mimi.”⁸³
8. Kwa ajili ya kutibu usahafulifu, imepokewa kutoka kwa Imam Hasan al-Mujtabaa (as) kwamba ameusia kumswalia Muhammad na Aali Muhammad.”⁸⁴
9. Imepokewa kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) kwamba alisema mwenye kumswalia kila asubuhi mara kumi na kila jioni mara kumi hakika yeye (saww) atahudhuria katika kila haja yake.⁸⁵
10. Imepokewa kutoka kwa Imam as-Saadiq (as) kwamba amesema: “Mwenye kusema: ‘Yaa Rabbi Swali Alaa Muhammad wa Aali Muhammad’ mara mia moja atakidhiwa haja mia moja.”⁸⁶
11. Imepokewa kutoka kwa Imam al-Baqir (as) kwamba amesema:
“Mwenye kusema baada ya Alasiri siku ya Ijumaa:

⁸² *Sharhu fadhlil swalawaati*, uk: 102

⁸³ *Jalaal-afhaam*, uk: 52

⁸⁴ *Wasailu Shi'ah* chapa ya Muasasti Aalil–Bait Qum, 1409 A. H Jz. 7, uk: 198 mlango 37 Hadith ya 9106 katika mtirirko

⁸⁵ *Sharhu fadhlil swalawaati*, uk: 127

⁸⁶ *Al-Kafiy* cha Kullainiy chapa ya Darul-Kutubil Islamiyati Teheran 1365 A. H Jz: 2, uk: 393 Hadith 9 mlango wa *Swalatualaa Nabiyyi wa Ahli-Baitihi*

اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَآلِ مُحَمَّدٍ الْأَوْصِيَاءِ الرَّاضِيِّينَ
الْمَرْضِيِّينَ بِأَفْضَلِ صَلْوَاتِكَ وَبَارِكْ عَلَيْهِمْ بِأَفْضَلِ بَرَكَاتِكَ
وَالسَّلَامُ عَلَيْهِمْ وَعَلَى أَرْوَاحِهِمْ وَاجْسَادِهِمْ وَرَحْمَةُ اللهِ وَبَرَكَاتِهِ

Mwenyezi Mungu atamkidhia haja elfu moja.”⁸⁷

12. Imepokewa kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) kwamba amesema: “Mwenye kuswali rakaa mbili usiku wa Ijumaa katika kila rakaa asome Sura al-Ikhilasi mara 50, akimaliza aseme:

اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى النَّبِيِّ الْعَرَبِيِّ وَآلِهِ.

yanaondoka matatizo yake.⁸⁸

13. Swalaifuatayo ni katika hazina ya siri za Aali Muhammad (saww), na imepokewa kutoka kwa Imam Ridhaa (as) kwamba amesema: “Mwenye kumswalia Nabii kwa Swala hii hupukutisha dhambi zake, husamehewa makosa yake, hudumu furaha yake, hujibiwa maombi yake, hupewa maombi yake na hukunjuliwa riziki yake, husaidiwa dhidi ya adui yake, huandaliwa sababu za aina za kheri na hujaaliwa kuwa katika marafiki wa Nabii wake katika pepo za juu. Ataisoma mara tatu asubuhi na mara tatu jioni:

⁸⁷ Al-Mahaasin cha al-Bariqiy chapa ya Darul-Kutubil-Islamiyyati Qum 1423H Jz. 1, uk: 59 Hadithi 96

⁸⁸ Hadiyatul Khudaa cha Kifursi, uk: 137

اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَآلِهِ فِي الْأَوَّلِينَ وَصَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَآلِهِ
 فِي الْآخِرِينَ وَصَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَآلِهِ فِي الْمَلَائِكَةِ الْأَعْلَى وَصَلِّ
 عَلَى مُحَمَّدٍ وَآلِهِ فِي النَّبِيِّنَ وَالْمُرْسَلِينَ اللَّهُمَّ أَعْطِ مُحَمَّدًا وَآلَهُ
 الْوَسِيلَةَ وَالْفَضِيلَةَ وَالشَّرَفَ وَالرِّفْعَةَ وَالدَّرَجَةَ الْكَبِيرَةَ اللَّهُمَّ
 إِنِّي آمَنْتُ بِمُحَمَّدٍ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَلَمْ أَرَهُ فَلَا تَحْرِمْنِي فِي
 الْقِيمَةِ رُؤْيَايَتِهِ وَارْزُقْنِي صُحبَتَهُ وَتَوَفَّنِي عَلَى مِلَّتِهِ وَاسْقِنِي مِنْ
 حَوْضِهِ مَثْرَبًا رَوِيًّا سَائِغاً هَنِيئًا لَا أَظْمَاءُ بَعْدَهُ أَبَدًا إِنَّكَ عَلَى
 كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ اللَّهُمَّ كَمَا آمَنْتُ بِمُحَمَّدٍ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ
 وَلَمْ أَرَهُ فَعَرَفْنِي فِي الْجَنَانِ وَجْهُهُ اللَّهُمَّ أَبْلِغْ رُوحَ مُحَمَّدٍ عَنِي
 صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ تَحِيَّةً كَثِيرَةً وَسَلَامًا⁸⁹

14. Inapofika theluthi moja ya usiku wa Ijumaa swali rakaa mbili za haja ukimaliza mswalie Mtume Muhammad (saww) na Aali Muhammad kisha sema: Bismillahi Rahmani Rahim, namswalie Muhammad na Aali Muhammad mara mia moja. Endelea na amali hii mfululizo kwa mikesha mitatu ya Ijumaa; utakidhiwa haja zako inshaallah.”⁹⁰

⁸⁹ *Tahdhiybul-Ahkaami* cha Sheikh Tusiy, Khurasan 460 A. H, Najaf al-Ashraf chapa ya Darul-Kutubil-Islamiyyati Teheran 1365 A. H, Sharhi ya Jz, 3. uk: 86 Hadith ya 15, *Dua fiy ziyaadati tamaamil-miati rakaati*

⁹⁰ *Mi'rajul-muumin* uk: 20

15. Khitma hii ni maarufu kwa jina la Swala ya ushindi, husomwa asubuhi siku arobaini baada ya Swala ya Alfajiri, kwa Swala hii vitafunguka kwako vizuizi na utanusurika kwa adui yako:

الصلوة والسلام عليك يا رسول الله ، الصلوة والسلام عليك
يا حبيب الله ، الصلوة والسلام عليك يا خليل الله ، الصلوة
والسلام عليك يا صفي الله، الصلوة والسلام عليك يا نجي الله
، الصلوة والسلام عليك يا خير خلق الله ، الصلوة والسلام
عليك يا من اختاره الله ، الصلوة والسلام عليك يا من زينه الله
، الصلوة والسلام عليك يا من ارسله الله ، الصلوة والسلام
عليك يا من شرفه الله ، الصلوة والسلام عليك يا من عظمه
الله ، الصلوة والسلام عليك يا من من كرمه الله ، الصلوة
والسلام عليك يا سيد المرسلين ، الصلوة والسلام عليك يا
امام المتقين ، الصلوة والسلام عليك يا خاتم النبيين ، الصلوة
والسلام عليك يا شفيع المذنبين ، الصلوة والسلام عليك يا
رسول رب العالمين ، الصلوة والسلام عليك يا سيد الأولين
، الصلوة والسلام عليك يا سيد الآخرين ، الصلوة والسلام

عليك يا قائد المرسلين ، الصلاة والسلام عليك يا شفيع الأمة ،
 الصلاة والسلام عليك يا عظيم الهمة ، الصلاة والسلام عليك
 يا حامل لواء الحمد ، الصلاة والسلام عليك يا صاحب المقام
 المحمود ، الصلاة والسلام عليك يا ساقي الحوض المورود ،
 الصلاة والسلام عليك يا أكثر الناس تبعاً يوم القيمة ، الصلاة
 والسلام عليك يا سيد ولد آدم ، الصلاة والسلام عليك يا
 أكرم الأولين والآخرين ، الصلاة والسلام عليك يا بشير ،
 الصلاة والسلام عليك يا نذير ، الصلاة والسلام عليك يا
 داعي الله بإذنه السراج المنير ، الصلاة والسلام عليك يا
 نبي التوبة ، الصلاة والسلام عليك يانبي الرحمة ، الصلاة
 والسلام عليك يا مقفى ، الصلاة والسلام عليك يا عاقب ،
 الصلاة والسلام عليك يا حاضر ، الصلاة والسلام عليك يا
 مختار ، الصلاة والسلام عليك يا ماحي ، الصلاة والسلام
 عليك يا أحمد ، الصلاة والسلام عليك يا محمد ، صلوات الله
 وملائكته ورسله وحملة عرشه وجميع خلقه عليك وعلى آلك
 وأصحابك ورحمة الله وبركاته .⁹¹

⁹¹ *Tafsiru nur thaqalain*, Jz: 4, uk; 302

16. Kila mwenye kusimama kwenye kaburi la Nabii (saww) na kusoma kauli yake (swt):

إِنَّ اللَّهَ وَمَلَائِكَتَهُ يُصَلُّونَ عَلَى النَّبِيِّ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا صَلُوْا
عَلَيْهِ وَسَلِّمُوا تَسْلِيمًا

kisha akasema: ‘*Swalallahu Alaika Yaa Rasulullahi*’ mara 70 atakidhiwa haja yake. Na kwa kuwa bahati tukufu yakumzuru Mtume (saww) kwa karibu sio rahisi kwa kila muumini, inawezezeka kwa mwenye haja kuchora kaburi lake (saww) katika ardhi au katika karatasi kisha analiweka mbele yake na kukariri uradi uliotajwa juu. Na sheikh Abbas al-Qummiy ameashiria juu ya hili katika mlango wa ziara ya Nabii (saww).

17. Na katika hadithi kutoka kwa Nabii (saww) ni kwamba mwenye kumswalia yeye na Aali zake baada ya Dhuhri mara mia moja, Mwenyezi Mungu atampa mambo matatu: Kwanza hatokuwa ni mwenye kudaiwa, na akidaiwa Mwenyezi Mungu atamlipia deni lake. Pili anahifadhi imani yake, na tatu: Siku ya Kiyama Mwenyezi Mungu hatomuuliza juu ya yale aliyomneemesha duniani.⁹²
18. Sheikh Bahaiy anasema: “Ikiwa mtu ni mwenye haja muhimu basi na atoke na kwenda jangwani, achore mistari minne na mstari mmoja baina ya mistari hiyo mine, na ajalie kuwa hilo ni kaburi la Nabii (saww) kisha alinyooshee kidole kwa kusema mara kumi na mbili: “*Swalallahu Alaika Yaa Rasulullahi*” haki-ka atakidhiwa haja yake inshaallah.”⁹³

⁹² Athar Barakaatu Swalawaati, uk: 119

⁹³ Athar Barakaatu Swalawaati, uk: 116

19. Ikiingia siku ya Jumatatu okota changarawe 74 jangwani, thelethini na saba kwa mkono wako wa kulia na thelethini na saba kwa mkono wa kushoto, kisha wekakwenye mkono wa kushoto yale yaliyokusanywa na mkono wa kulia, na weka kwenye mkono wa kulia yale yaliyokusanywa na mkono wa kushoto, kisha swali rakaa mbili za haja na baada ya salamu na kumaliza Swala, isomee kila changarawe moja ya mkusanyiko uliowekwa upande wa kulia: “as-Swalatu Alaa Muhammad wa Aali Muhammad” mara kumi isipokuwa changarawe ya mwisho, yenyewe utaisomea mara sita, na jumla yake katika changarawe zote itakuwa ni mara 366, na utafanya vivyo hivyo kwa changarawe zilizoko upande mwingine. Kisha nyanyua mikono yako kwa kuomba dua na omba haja yako kwa Mwen-ezi Mungu kisha tupa changarawe za kwanza katika maji yenyе kutiririka na fukia changarawe za kundi la pili ardhini. Amali hii ni mujarabu na haijaonekana kwenda kinyume na matalario.⁹⁴
20. Kwa kuondoa huzuni, matatizo na kupanuka riziki soma yafuatayo:

Siku ya Jumamosi: “Allahumma Swali Alaa Muhammad wa Aali Muhammad” mara elfu moja.

Siku ya Jumapili: “Yaa Rabbal-Alamina” mara elfu moja.

Siku ya Jumatatu: “Yaa Dhal- Jalali Wal-Ikraam” mara elfu moja.

Siku ya Jumanne: “Yaa Qaadhiyal- Hajaati” mara elfumoja.

Siku ya Jumatano: “Yaa Arhama Raahimina” mara elfu moja.

Siku ya Alhamisi: “Yaa Hayyu YaaQayuum” mara elfu moja.

⁹⁴ Hadiyatuh Khudaa uk: 143

Siku ya Ijumaa: “Yaa Laa Ilaaха Illallahu al-Malikul-Haqul-Mubiin.” Mara elfu moja.⁹⁵

21. Katika kila siku ya Ijumaa na vilevile siku ya Iddil-Fitri sema mara elfu moja:

يَادِئُمُ الْفَضْلَ عَلَى الْبَرِّيَّةِ، يَابْسِطُ الْيَدِينَ بِالْعَطِيَّةِ، يَا صَاحِبَ
الْمَوَاهِبِ السُّنْنِيَّةِ، صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَآلِهِ خَيْرِ الْوَرَى سَجِيَّةَ،
وَأَغْفِرْ لَنَا يَا ذَا الْعَلَى فِي هَذِهِ الْعَشِيَّةِ⁹⁶

22. Kutawasali kwa Nabii Mtukufu (saww): “Elekea kibla na hali ni mwenye udhu, hudhurisha moyo wako na mswalie Muhammad na Aali zake mara elfu moja na endelea na hali hii kwa muda wa siku 92 kisha omnia haja yako.”⁹⁷
23. Endelea kwa muda wa siku arobaini katika kumswalia Muhammad na Aali zake, kila siku mara 557, sambamba na kuwajibika kwa kutimiza wajibu wa kisheria na kuacha maasi, kisha omnia haja yako.⁹⁸
24. Mswalie Mtume Muhammad na Aali zake kwa idadi ya jumla ya herufi za moja wa Maasumina kumi na nne, na kwa muda wa siku arobaini, kisha toa zawadi ya thawabu zake kwao (as).⁹⁹
25. Tawasali kwa bibi Zainabu al-Kubra (as), nayo ni kati ya tawasuli zenyenye baraka na kheri nyingi, njia ya kutawasali kwake

⁹⁵ Khutum wa adhikaari shifaai wadarmaan – cha kifurusi uk: 83

⁹⁶ Mafaatihul-Jinan cha Sheikh Abbasi al-Qummiy

⁹⁷ Hadiyatul-Khudaa, uk: 143

⁹⁸ Hadiyatul-Khudaa, uk: 143

⁹⁹ Athar Barakaatu Swalawaati uk: 118

(as) ni kumswalia Muhammad na Aali zake kwa muda wa siku 69 kila siku mara 69, kisha unazitoa zawadi kwake (as), na ni bora kutoa sadaka shilingi 79 katika njia ya Mwenyezi Mungu vilevile.¹⁰⁰

26. Kati ya khitma mujarabu ambazo baadhi ya ndugu wamezijaribu ni kumswalia Mtume Muhammad na Aali Muhammad mara 69 tangu kutokea kwa tatizo, na kuzitoa zawadi kwa bibi Zainabu (as) pamoja na kutoa shilingi 69 katika njia ya Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa nia yake.”¹⁰¹
27. Na kati ya khitma mujarabu ni kutoa zawadi ya kumswalia Muhammad na Aali Muhammad mara 133 katika uwanja wa kaburi la Abul-Fadhil Abbasi (as). Na pia imesemwa ni kufunga siku 133 kwa ajili ya khitma hii, pia imesemwa ni siku 40 na inasemekana ni siku 21.¹⁰²
28. Na kati ya khitma ambazo zinazingatiwa sana na watu wa maadili na tabia na wanaikimbilia wanapopatwa na matatizo: Ni kumswalia Muhammad na Aali Muhamamad mara 72,000 katika siku 72, na kuzitoa zawadi kwa roho tukufu za Mashahidi wa Karbalaa ambao walikufa kishahidi pamoja na Imam Husein (as).¹⁰³
29. Na kati ya mujarabati katika watu wa sira na maadili ni kumswalia Muhammad na Aali Muhammad mara 786, yaani kwa idadi ya jumla ya herufi za Bismillahi Rahamani Rahim, inafaa sana katika kupanua riziki na kujinasua kutokana na kutekwa.¹⁰⁴

¹⁰⁰ *Hadiyatul Khudaa*, uk: 146

¹⁰¹ *Hadiyatul Khudaa*, uk: 146

¹⁰² Athar Barakaatu Swalawaati uk: 121

¹⁰³ *Hadiyatul Khudaa*, uk: 146

¹⁰⁴ Athar Barakaatu Swalawaati, uk: 121

30. Na kati yakhitma zingine zinazopasa kuzingatiwa ni kutawasali kwa Sayyidi Shuhadaa Hamza bin Abdul-Muttalib (r.a), na hiyo ni kwa kumswalia Muhammad na Aali Muhammad kwa siku arobaini katika kila siku mara 60, na kisha kuzitoa zawadi kwa Hamza Ami wa Nabii (saww).¹⁰⁵
31. Na kati ya khitma mujarabu vilevile ni kutawasali kwa Mama wa Abul-Fadhil Abbasi (as), naye ni Fatima al-Kilabiyyah maarufu kwa jina la Ummul-Banina (r.a), hiyo ni kwa kumswalia Muhammad na Aali Muhammad kwa siku arobaini kila siku mara 135, kisha unatoa zawadi thawabu zake kwa roho yake tukufu.¹⁰⁶
32. Na kati ya khitma mujarabu nazinazopasa kuzingatiwa vilevile ni kutawasali kwa mjumbe wa Imam Husein (as), na hiyo ni kwa kumswalia Muhammad na Aali Muhammad siku arobaini kila siku mara 170, kisha anazitoa zawadi kwa Muslim bin Aqil (r.a).¹⁰⁷
33. Ilikuwa ni ada ya al-Arif al-Haj Sheikh Hasan Ali an-Nakhdiyy al-Isfahaaniy (r.m) katika kila usiku wa Ijumaa kusoma sura tukufu Yasin, kisha kumswalia Muhammad na Aali Muhammad mara 1100 na kuzitoa zawadi kwa roho za waumini katika bonde la Salaam Najaf tukufu, na wengi wameujaribu uradi huu kwa njia za kimaada na kimaanawi.¹⁰⁸
34. Unapopatwa na tatizo au huzuni hakika kutawasali kwa Nabii (saww) ni kimbilio bora na lenye kusaidia, na ili kutawasali kwake sema ndani ya siku arobaini kila siku mara 92 au mara 132:

¹⁰⁵ Athar Barakaatu Swalawaati, 122

¹⁰⁶ Athar Barakaatu Swalawaati 122

¹⁰⁷ Haditayatu Khudaa, uk: 148

¹⁰⁸ Athar barakaatu swalawaati, uk: 119

اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى نَبِيِّ الرَّحْمَةِ وَشَفِيعِ الْأُمَّةِ وَ كَافِرِ الْعُمَّةِ
مُحَمَّدٌ وَآلِهِ أَجْمَعِينَ.

kwani ni mujarabu sana.¹⁰⁹

35. Kati ya khitma mujarabu sana katika kutatua matatizo ya kimaada kwa watu wa maadili ni kusema kila siku:

لَا فَتَى إِلَّا عَلَى لَا سِيفٍ إِلَّا ذُو الْفَقَارِ

baada ya Swala ya Subhi mara 70, na kumswalia Nabii na Aali zake baada ya Swala ya Maghribi mara 110.¹¹⁰

36. Kati ya khitma mujarabu na inayopasa kuzingatiwa na am-bayo walikuwa wanaiusia sana wafuasi wa Ahlul-Bait baada ya kuona baraka zake za kimaada na kimaanawi ni kumswalia Muhammad na Aali Muhammad kila siku mara 3750 kwa muda wa siku arobaini, kisha kuzitoa zawadi thawabu zake kwa roho za waliokufa shahidi katika njia ya kumtawalisha Amirul-Muuminina (as) na kuwapa haki Ahlul-Bayt (as) tangu mwanzo wa Uislamu.¹¹¹
37. Kutawasali kwa Imam Ridhaa (as) kwa siku arobaini, na hiyo ni kwa kujitwaharisha kisha kuelekea kwa kuuhudhurisha moyo kwa Imam (as), kwa kuchunga adabu za dhikri na kusema: “*Allahumma Swali Alaa Ali bin Musa Ridhaaal-Murtadhaa (as)*” mara 110.¹¹²

¹⁰⁹ Athar Barakaatu Swalawaati 122

¹¹⁰ Athar Barakaatu Swalawaati 121

¹¹¹ Hadiyatul Khudaa, uk: 149

¹¹² Hadiyatul Khudaa, uk. 150

38. Kuswali rakaa mbili za haja kisha kumswalia Muhammad na Aali zake mara 116 na kuzitoa zawadi kwa Imam Musa bin Ja'far (as), na baada ya kumaliza unaweka shavu lako la kulia ardhini na kusema:

اللَّهُمَّ قَدْ عَلِمْتَ حَوَائِجِي فَصَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَآلِ مُحَمَّدٍ وَاقْضِهَا،

kisha unaweka shavu lako la kushoto ardhini na unasema:

اللَّهُمَّ قَدْ أَحْصَيْتَ ذُنُوبِي فَبِحَقِّ مُحَمَّدٍ وَآلِ مُحَمَّدٍ صَلِّ عَلَى
مُحَمَّدٍ وَآلِ مُحَمَّدٍ وَاغْفِرْهَا وَتَصَدَّقْ عَلَيَّ بِمَا أَنْتَ أَهْلُهُ،

kisha unaweka paji lako ardhini na kusema mara mia moja:

شَكْرًا شَكْرًا

kisha unaomba haja yako.¹¹³

39. Kutawasali kwa Abu Talib, Fatimat binti Asad na Khadija al-Kubra (as), nayo ni mujarabu mambo yanapokuwa magumu na kutatiza, na hiyo ni kusema kwa muda wa siku 11 katika kila siku mara 51: “*Allahumma Swali Alaa Muhammad wa Aali Muhammad*” kisha unazitoa zawadi kwao (r.a).¹¹⁴

¹¹³ Hadiyatul Khudaa uk: 150

¹¹⁴ Hadiyatul Khudaa, uk 137

40. Imepokewa kutoka kwa Imam Ridhaa (as) kwamba amesema:

“Mwenye kumswalia Muhammad na Aali Muhammad siku ya Ijumaa mara mia moja anakidhiwa haja 60, thelathini kati ya hizo ni za duniani na thelathini ni za akhera.”¹¹⁵

KWA AJILI YA KUONDOA ADHABU YA KABURI

Imepokewa kutoka kwa Nabii (saww) kwamba amesema:

“Mwenye kuswali rakaa mbili usiku wa Ijumaa katika kila rakaa akasoma Sura Ikhlas mara 50, na akasema katika mwisho wa Swala yake:

اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى النَّبِيِّ الْأَمِيِّ.

Mwenyezi Mungu atamsamehe yaliyotangulia katika madhambi yake na yanayokuja, na ni kana kwamba amesoma Qur’ani yote mara 12,000, na Mwenyezi Mungu atamuondolea njaa na kiu ya Siku ya Kiyama, na Mwenyezi Mungu atamuondolea matatizo na huzuni na atamlinda kutokana na Ibilisi na askari wake, na hatoandikiwa kosa kamwe, Mwenyezi Mungu atamfanyia tahafifu katika sakaratil-mauti, na akifa katika siku yake hiyo au usiku wake huo atakufa shahidi, na atamuondolea adhabu ya kaburi na hatomuomba Mwenyezi Mungu chochote isipokuwa atampa, na atazifanya Swala zake na Saumu zake kuwa ni nzito na atamjibu dua yake na Malaika wa mauti hatochukua roho yake hadi Ridhwan amjie na harufu ya pepo na kinywaji kutoka peponi.”¹¹⁶

¹¹⁵ Athar Barakaatu Swalawaati, uk: 128- 129

¹¹⁶ Mustadrakul-Wasail cha Nuru chapa ya Muasasati Aalil-Bayti Qum 1308 A. H. Jz: 6, uk: 81 mlango 37 wa (*Istihbab swalaaatil- magharibati layatil- jumu’ati*) Hadith na: 10 ya 6484 katika mtirirko

AMALI ZENYE MANUFAA ZAIDI KABURINI

Kutoka kwa Abul-Alqamah huria wa Bani Hashim amesema:

“Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alituswalisha Subhi kisha akatugeukia akasema: ‘Enyi masahaba zangu jana usiku nimemuona ami yangu Hamza bin Abdul-Muttalib na ndugu yangu Ja’far bin Abu Talib wakiwa na sahani ya zabibu mbi-vu mikononi mwao, wakazila kwa muda kisha zikageuka na kuwa zabibu kavu, nazo wakazila kwa muda, zabibu zikageuka na kuwa tende; Nikasogea kwao nikawaambia naapa kwa baba yangu, ni amali gani bora zaidi mliifanya? Wakasema: Tumekuta amali bora zaidi ni kukuswalia wewe, kutoa mali na kumpenda Ali bin Abu Talib (as).”¹¹⁷

MIONGONI MWA FAIDA ZA KUMSWALIA MUHAMMADI (S.A.W.W.) NA AALI ZAKE (A.S.)

1. Mwenye kusema siku ya Ijumaa:

رَبِّ صَلَّى عَلَى مُحَمَّدٍ النَّبِيِّ وَعَلَى أَهْلِ بَيْتِهِ

mara mia moja Mwenyezi Mungu atamkidhia haja mia moja.¹¹⁸

2. Kunyanya sauti kwa kumswalia Mtume kunaondoa unafiki; Imepokewa kutoka kwa Abu Abdillahi as-Sadiq (as) kwamba

¹¹⁷ Rejea iliyotangulia Jz. 7, uk: 250 mlango 45 (Taakudu istihaab saqiyil- Maai) Hadith 4 ya 8170 katika mtirirko

¹¹⁸ Wasailu Shi’ah chapa ya Muasasati Aalil-Bayt Qum 1409 A. H Jz: 7, uk: 387 mlango 34 Hadith 9654 na Sunnan Tirimidhiy, Jz: 1, uk: 303

amesema. Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww): “Nyanyueni sauti zenu kwa kuniswalia, hakika kunaondoa unafiki.”¹¹⁹

3. Kumswalia Muhammad na Aali zake ni sababu ya kutakasa amali; Imeshatangulia kauli ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww): “Kuniswalia kwenu kunapasisha dua zenu na ni kumridhisha Mola Wenu na ni utakaso wa amali zenu.”¹²⁰
4. Mwenye kumswalia Muhammad na Aali zake mara moja Mwenyezi Mungu anamfungulia mlango wa afya.¹²¹
5. Kumswalia Muhammad na Aali zake kunaondoa ufkiri.¹²²
6. Unaposahau kitu na ukataka kukikumbuka mswalie Muhammad na Aali zake.¹²³
7. Kumswalia Muhammad na Aali zake kunamshinda adui anayemnyemelea mwanadamu, yaani Ibilisi.¹²⁴
8. Mwenye kumswalia Nabii na Aali zake (as) Malaika wanamuombea rehema.¹²⁵
9. Mwenye kumswalia Nabii na Aali zake anakuwa ni mfano wa Malaika na anapata rehema ambayo wanaipata Malaika.¹²⁶

¹¹⁹ *Al-Kafiy* cha Kullainiy chapa ya Darul-Kutubil-Islamiyat Teheran 1365 A. H Jz: 2, uk: 493 mlango wa *Swalatu alaa Nabiyyi Muhammad wa Ahli Baitihi* Hadith

¹²⁰ *Jamalul-Usubu'i* cha Sayid Ibnu Tausi chapa ya Daru Ridhaa Qum uk: 241 ameeleza tunayoyapokea katika fadhila za kumswalia Nabii (saww)

¹²¹ *Jami'ul-Akhibaar*, Taajju Diyn Ashiiriy chapa ya Daru Ridhaa Qum 1405 uk: 59 fasilu ya 28 fiy swalaati alaa nabiyyi (saww)

¹²² *Jalaul-Afhaam* uk: 252

¹²³ *Jalaul-Afhaamuk*. 252

¹²⁴ *Sharhu fadhaaili swalawaati*, uk: 114

¹²⁵ *Mustadrakul-Wasail* cha Nuriy chapa ya Muasasati Aalil-bait Qum 1408 A. H. Jz: 5, uk: 363 mlango wa 31 Hadith 28 ya 6036 katika mtirirko

¹²⁶ *Rejea iliyo tangulia*

10. Kwa kumswalia Muhammad na Aali Muhammad mwanadamu anafikia cheo cha ukhalili kama alivyokifikia Ibrahim (as) kwa baraka za kumswalia Muhammad na Aali zake.¹²⁷
11. Watu wema zaidi na waliokaribu zaidi na Nabii (saww) Siku ya Kiyama ni wale waliokuwawanamswalia kwa wingi duniani.¹²⁸
12. Kunapelekea kupata uombezi wa Nabii (saww).¹²⁹
13. Ni kafara ya madhambi.¹³⁰
14. Imepokewa kutoka kwa Imam Amirul-Muuminina (as) kwamba amesema: “Kumswalia Nabii (as) kunapukutisha sana makosa kuliko maji yanavyozima moto.”¹³¹

KUMSWALIA MUHAMMADI (SAWW) NA AALI ZAKE (AS) KUNALINGANA NA TASBIHI NA TAHLILI

Imepokewa kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) kwamba amesema:

“Mwenyezi Mungu alipoumba Arshi aliumba Malaika elfu sabini na akawaambia: ‘Fanyeni tawafu katika arshi ya nuru na mnisabih mimi na bebeni arshi yangu.’ Wakatufu na wakasabih na wakataka kubeba arshi lakini hawakuweza, ndipo Mwenyezi Mungu akawaambia: ‘Fanyeni tawafu katika arshi ya nuru na isalieni nuru ya utukufu Wangu na mswalieni Muhammad kip-

¹²⁷ Ilalu Shara’iuu cha Sheikh Suduuq cha ya maktabatu Dawariy Qum uk: 24

¹²⁸ Makarimul-akhilaq cha Tusiy chapa ya Daru Sharif Ridhaa Qum 1412 A. H uk: 312

¹²⁹ Mustadrakul-wasail cha Nuriy chapa ya Muasasati Aalil-Bayt Qum 1408H Jz: 5, uk: 334 mlango wa 31 Hadith 15 namba 6024

¹³⁰ Wasail Shi’ah Jz: 7, uk: 194 mlango 34

¹³¹ *Thawabul-aamali wa iqaaibl-aamali* cha Sheikh Suduuq chapa ya Daru Ridhaa Qum 1406 A. H uk: 154

enzi Changu (saww).’Ndipo wakabeba arshi na wakatufu pembezoni mwake wakasema: ‘Mola Wetu ultiuamrisha tukusabihi na kukutukuza.’Mwenyezi Mungu akawaambia.‘Enyi Malaika Wangu mkimswalia kipenzi Changu Muhammad (saww) basi mtakuwa mmeshanabisahi, kunitkuza na kunifanyia tahlili Mimi.’”¹³²

NYAKATI AMBAZO INAPASA HUMO KUMSWALIA MTUME (SAWW)

1. Baada ya kusikia jina la Nabii (saww).
2. Wakati wa kuanza kufundisha, kutoa mawaiidha na baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu na kumtukuza.¹³³
3. Ni mustahabu wakati wa kukaa katika kipando kusema: Bismillahi Wabillahi wa Allahu Akbar Wa Swalallahu Alaa Muhammad Wa Aalihi Khairul-Bashari.¹³⁴
4. Wakati wa kutawadha.
5. Unapopita msikitini, unapoingia na kutoka humo.¹³⁵
6. Kabla hujaanza dhikri ya pamoja na ya peke yako.¹³⁶
7. Wakati wa kuanza kuandika na kutuma, wakati wa kuanza kula chakula na mwisho wake.¹³⁷
8. Katika khutuba ya ndoa baada ya kumshukuruna kumtukuza Mwenyezi Mungu.¹³⁸

¹³² *Mustadrakul-Wasaail* cha Nuriy chapa ya Muasasati Aalii-Bait Qum 1408 A. H. Jz: 5, uk: 341 mlango wa 31 Hadith 39 ya 6048 katika mtirirko

¹³³ Tafsiru-Ruuhul-bayaan, Jz: 7, uk: 231

¹³⁴ Tafsiru-Ruuhul-bayaan, Jz: 7, uk: 231

¹³⁵ Sharhu Ihqaaql-Haqqi Jz: 9, uk: 621 na 622

¹³⁶ Sharhu Ihqaaql-Haqqi Jz: 7, uk: 230

¹³⁷ Sharhu Swalawati, uk: 113

¹³⁸ Sharhu Ihqaaql-Haqqi Jz: 7, uk: 232

9. Karibu na kaburi la Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww).¹³⁹
10. Baada ya kumaliza Sa'i baina ya Swafa na Mar'wa katika Mash'ari tukufu.¹⁴⁰
11. Njiani wakati wakwenda Hija, mwenye kutaka kupanda mwiniuko atasoma takbir, na akielekea mteremko atamswalia Muhammad na Aali Muhammad.¹⁴¹
12. Baina ya kaburi la Nabii (saww) na mimbari yake.¹⁴²
13. Wakati unapovuma upepo na wakati wa kuchinja wanyama.¹⁴³
14. Wakati wa kuingia sokoni.¹⁴⁴
15. Unapostaajabu.¹⁴⁵
16. Unapotaka kufanya jambo.¹⁴⁶
17. Kabla ya dua na baada ya kumaliza.¹⁴⁷
18. Baada ya kupiga chafya.¹⁴⁸
19. Unaponusa harufu ya manukato, kunusa maua hususan maua ya waridi Muhammadiy.¹⁴⁹

¹³⁹ Sharhu Ihqaaql-Haqqi Jz: 7, uk: 237

¹⁴⁰ Sharhu Ihqaaql-Haqqi Jz: 7, uk: 237

¹⁴¹ Sharhu Ihqaaql-Haqqi Jz: 7, uk: 231

¹⁴² Sharhu Ihqaaql-Haqqi Jz: 7, uk: 231

¹⁴³ Sharhu Swalawat, uk: 113

¹⁴⁴ Sharhu Swalawat, uk: 113

¹⁴⁵ Sharhu Swalawat, uk: 113

¹⁴⁶ Sharhu swalawaati, uk: 113

¹⁴⁷ Sunanu Tirimidhiy Jz: 2, uk: 53

¹⁴⁸ Wasailu Shi'ah cha Hurrul-Aamiliy, chapa ya Muasasati Aalil-Bayt Qum 1409A. H. Jz: 7, uk: 203 mlango wa 42, Hadith ya 9118.

¹⁴⁹ Raudhatul-Wasail-Waadhiyna Jz: 2, uk: 328

20. Baada ya Swala za kila siku, na hiyo ni kwa kumswalia Muhammad na Aali zake mara kumi na nne na kutoa zawadi kwa Maasumina (as), kisha unamswalia Muhammad na Aali zake mara saba na kuzitoa zawadi kwa mawalii wa Mwenyezi Mungu. Hii ni Sunnah ya watu wa maadili.

KUMSWALIA MUHAMMADI NA AALI ZAKE UKIWA MACHO NA WAKATI WA KULALA

Nyakati hizi mbili, yaani kabla ya kulala na mwanzo mtu anapoamka kutoka usingizini, zinaumuhimu maalum; Hiyo ni kwa sababu ni mwanzo na mwisho wa maisha ya kila siku ya mwanadamu, ni dharura mwanadamu kuwa katika mwanzo wa shughuli zake za kila siku awe ni mwenye kumwelekeea Mwenyezi Mungu kikamilifu na si mwenye kughafilika Naye, ili awe katika amani dhidi ya vishawishi vya shetani na wasiwasi wa nafsi yenye kuamuru maovu, hali ni hiyohiyo wakati wa kulala, muda ambao unahesabiwa kuwa ni wakati wa kutafakari na kuchukua maamuzi ya maisha ya kesho. Ni wajibu kwa mwanadamu wakati wa mwelekeo huu wa kiroho aikinge nafsi yake kutokana na hatari na kila mikakati ya shetani au fikra za kinyama zinazomuweka mbali na njia ya Mwenyezi Mungu iliyonyooka na kumfanya kwenda mbio nyuma ya matamanio ya kishetani. Wachamungu na watu wa irfani walikuwa wanazipa umuhimu mkubwa nyakati hizi mbili na hiyo ni kwa kuhitimisha siku yao kabla ya kuzama kwenye usingizi kwa kumswalia Muhammad na Aali zake mara 14 au mara 3 kwa uchache, na walikuwa wanapoamka kutoka usingizini na kabla ya kuamka vitandani mwao wanakaa na wanaelekeea kwa Mwenyezi Mungu Mtukufuna wanamswalia Muhammad na Aali zake mara 14 na wanatoa zawadi kwa ma'asumina 14, kisha wanamswalia mara saba na wanatoa zawadi

kwa mawalii wa Mwenyezi Mungu, kisha wanaanza maisha yao kwa udhu kisha wanaendelea na kazi zao zingine.¹⁵⁰

KUJIKOMBOA KUTOKA KWENYE DHAMBI KUPITIA KUMSWALIA MUHAMMADI NA AALI ZAKE (A.S.)

Dhambi ni matunda ya mafungamano baina ya nafsi yenyе kuanmirsha maovu na shetani, naye humuweka mwanadamu mbali na uzio wa umaasumu na utakaso. Kufurahia madhambi kunampelekea mwanadamu kufanya madhambi zaidi, kukengeuka usafi na kufuata njia ya shetani, na hapo uwepo wake hujaa giza.

Chanzo cha uovu wote wa mwanadamu ni dhambi ambayo inaanza kama doa jeusi katika moyo wa mwanadamu, akitubia doa hilo linaondoka, ama akiendelea katika maasi doa hilo linaanza kukua kidogo kidogo hadi linafunika moyo wote, hivyo mwanadamu hatofaulu baada yake abadani, isipokuwa akipata rehema kutoka kwa Mola Wake. Na kwa sababu hii imekuja katika athari kwamba hakuna kitu kinachodhuru moyo kama dhambi.

Hakika maisha ya mwanadamu yanaambatana na moyo, moyo ndio ambao unaendesha mwili wa mwanadamu, na viungo vyote vimatedhalilishwa kwake na vitendo vyake vyote na harakati zake zinatokana na moyo. Na wakati uleule hakika sehemu nyingi ambazo zinawezekana kusababisha taabu kwa mwanadamu ni moyo, iwapo shetani akiufanya kuwa ni makazi, yaani sehemu ile ile ya kiungu ambayo inaambatana na utu wa mwanadamu na kumuwezesha kumshuhudia Malaika wa wahyi na kusikiliza maneno yake.

Hivyo wema wa mwanadamu na uovu wake umetegemezwa katika moyo, Mwenyezi Mungu amesema:

¹⁵⁰ Risalatu Mu'unisi Saalikiyna, uk: 18

إِلَّا مَنْ أَتَى اللَّهَ بِقَلْبٍ سَلِيمٍ

“Siku ambayo haitafaa mali wala watoto. Isipokuwa atakayeku-ja kwa Mwenyezi Mungu na moyo safi.”(26:89)

Kitu kimoja ambacho kinaweza kuporomosha moyo wa mwanadamu ni dhambi hivyo ni wajibu kujiepusha na dhambi na kupata msaada kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Hapa tunafahamu ni kwa nini wataalamu wa ugonjwa wa moyo wamezingatia kuwa ugonjwa wa moyo ni kati ya magonjwa magumu katika mwili wa mwanadamu; Hakika moyo ni kituo cha kuendesha mwili. Amesema Imam as-Sadiq (as): “Upofu mbaya zaidi ni upofu wa moyo.”¹⁵¹

Moyo ukipofuka mwanadamu anakuwa mbali kidogo kidogo na Mwenyezi Mungu na ukamilifu wa kibinadamu, na anatumbukia katika maporomoko ya matukio na anapetuka katika uanadamu wake. Na katika hali hii hii anatoa mwanya kwa shetani ambaye anamwenda mbio pamoja na moyo wenye kuamrisha maovu kuionyesha dhambi kuwa ni ndogo katika mtazamo wa mwanadamu, na hivyo anamtwala mwanadamu na anamzoeza kufanya madhambi, mwanadamu akizoea dhambi inakuwa ni vigumu kwake kuyaacha baada ya hapo, kwa sababu kuacha tabia ni katika mambo magumu isipokuwa kwa kutegemea uchamungu ambao ndio kusanyiko la kila kheri. Kama ilivyopokewa kutoka kwa Nabii (saww).¹⁵²

Mtume (saww) ameuhesabu uchamungu ni kiungo muhimu cha kuepukana na madhambi na ni dawa yenye kuponya maradhi ya kin-

¹⁵¹ *Man laa yahudhuruhul-Faqiyhi* cha Sheikh Suduuq chapa ya Muasasati Nashiril-Islamiy Qum Jz: 4 uk: 402 Hadith namba 5868

¹⁵² Inasemekana kwamba mwanaume alikuja kwa Nabii (saww) akasema: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu niusie. Akasema: ni juu yako kuwa mchamungu, hakika inakusanya kila kheri. Sharhu Nahjul-Balaghah Jz: 11, uk: 185, Bayaanu Ahwaalul-aarifiyna.

afsi. Uchamungu ni mwanga wanyoyo na ponyo la miili na ni rekebishi la yaliyoharibika katika nyoyo, na ni utakaso wa nafsi na safisho la uoni, nao ni tulizo la mkanganyiko wa ndani na huangazia giza.

Hivyo kwa ajili ya kufika kwenye usafi wa moyo na mwanga wake na kuwaweka mbali mashetani na uzio wa moyo ambaeo ndio arshi ya Mwenyezi Mungu fanyeni tawasuli kwa kumswalia Muhammad na Aali Muhammad na rejeeni kwenye utajo huu wa baraka, mtukufu uliobora kwa ajili ya kutakasa nyoyo zenu kutokana na kila uchafu. Imepokewa kutoka kwa Imam Amirul-Muuminina (as) vilevile amesema:

“Ambaye uchamungu wake nimchache basi moyo wake unakufa na ambaye moyo wake umekufa anaingia motoni.”¹⁵³ Na kutoka kwake (as) vile vile: “Enyi waja wa Mwenyezi Mungu! Tambueni kwamba uchamungu ni ngome imara.”¹⁵⁴

Uchamungu ni ngome ya mwanadamu kutokana na madhambi na maasi. Hivyo mcheni Mwenyezi Mungu Mtukufu na jihadharini kuyasogelea madhambi na jiepusheni kuamiliana na waovu na mafisadi; Hakika Imam Amirul-Muuminina (as) anasema:

“Rafiki muovu ni kipande cha moto.”¹⁵⁵ Na Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

فَادْكُرُوا آلَاءَ اللَّهِ وَلَا تَعْنُوا فِي الْأَرْضِ مُفْسِدِينَ

“.....Basi zikumbukeni neema za Mwenyezi Mungu na wala msifanye ufisadi katika ardhi.”¹⁵⁶

¹⁵³ Wasailu Shi'ah cha Hurrul-Aamly chapa ya Muasasati Aalil-Bayt Qum 1409H Jz: 12, uk: 187 mlango 117 wa Istihaab swamti wa sukuti illa anil – khair Hadith ya 16032

¹⁵⁴ Nahjul-Balaghah khutuba ya 198, Ghurarul-Hikam, uk: 147

¹⁵⁵ Ghurarul-Hikam, uk: 431 Dham Qariyn suui Hadith ya 9819

¹⁵⁶ Suratul-Aaraaf: 74

KUONDOA MASIKITIKO KWA KUMSWALIA MTUME (SAWW)

Sufiani Thauriy aliulizwa: Ni siku ipi ni siku ya masikitiko? Ambapo Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema: “**Na waonye juu ya siku ya masikitiko.**”? Akasema:

“Ni Siku ya Kiyama kwa sababu masikitiko yataenea kwa vi-umbe vyote, kwani wema watasikitika kwa yaliyowapita kwa kutofanya ziada ya mema na vitendo vyema, ama waovu watasikitika kwa kutofua kwa njia ya kheri duniani.” Akaam-biwa: Je, kunapatikana katika siku hiyo ambaye hatosikitika? Akasema: “Ndio, hakika aliyekuwa anadumu katika kumswalia Muhammad na Aali zake (a.s.) hatosikitika Siku ya Kiyama.”¹⁵⁷

KUJIKINGA NA MOTO WA JAHANNAM KWA KUMSWALIA MTUME (SAWW)

Katika fiqhi ya Imam Ridhaa (as) imeandikwa:

“Mwenye kumswalia Muhammad na Aali zake mara mia moja baina ya rakaa mbili za Alfajri na rakaa mbili za Dhuhri Mwenyezi Mungu ataukinga uso wake na moto wa Jahannam.”¹⁵⁸

VITENDO BORA ZAIDI KATIKA KAABA

Abdu Salaam bin Nuayim amesema:

“Nilimwambia Imamas-Sadiq (as): ‘Hakika mimi niliingia katika nyumba tukufu na hakikunijia kitu chochote katika dua

¹⁵⁷ *Sharhu Swalawati*, uk; 95

¹⁵⁸ *Fiqihi Ridhaa*, uk: 139 mlango wa 11 *Swalatu Layli*

isipokuwa kumswalia Muhammad na Aali Muhammad! Imam akasema: ‘Ama hakika hajatoka yeyote na kilichobora zaidi kuliiko ulichotoka nacho wewe kwa Swala hiyo.’¹⁵⁹

UTAJO WA MOYONI NA ULIMINI

Kati ya adabu za kumswalia Muhammad na Aali zake (a.s.) ni moyo kuafikiana na ulimi, yaani usiwe utajo wa mwanadamu katika Swala ya kumswalia Mtume (saww) ni katika hali ya kughafilika moyoni.¹⁶⁰

KUMHUDHURISHA NABII (SAWW)

Kati ya adabu zingine za kumswalia Muhammad (s.a.w.w.) na Aali zake (a.s.) ni mwenye kufanya uradi kumuona Nabii (saww) yuko mbele yake na anahisi kana kwamba anaongea pamoja naye.¹⁶¹

RIWAYA KUTOKA KWA SALMAN AL-FARISIY

Imepokewa kutoka kwa Salman al-Farisiy (r.a) kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufuamesema katika Hadithi al-Qudusiy:

“Viumbe watukufu zaidi kwangu ni Muhammad, Ali na Maimam kutoka katika kizazi chao, basi mwenye haja na akitakakukidhiwa au akishukiwa na msiba na akataka kuondolewa msiba wake basi na aniombe kwa haki ya Muhammad na Aali zake (a.s) watoharifu ili nimkidhie haja yake.”¹⁶²

¹⁵⁹ *Al-Kafiy cha Kullainiy chapa ya Muasasatil-Kutubil-Islamiyyati*, Tehran 1365H Jz: 2, uk 494 mlango wa Swalatu alaa Nabiyi wa Ahli baitihi, Hadith 17

¹⁶⁰ *Sharhu Swalawaati*, uk: 116

¹⁶¹ *Sharhu Swalawaati*, uk: 116

¹⁶² *Sharhu Swalawaati*, uk: 116

RIWAYA KUTOKA KWA MASHEIKH WANAOZINGATIWA

Amepokea Sheikh Mufid, Sheikh Suduq na Sheikh Tusiy kwa sanadi mbali mbali na kwa ibara tofauti riwaya kutoka kwa Imam al-Baqir (as) kwamba amesema:

“Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww): ‘Hakika itakapokuwa Siku ya Kiyama na watu wapeponi wakakaa peponi, na watu wa motoni wakakaa motoni, mja atakaa motoni kwa vipupwe sabini, nayo ni miaka sabini kisha atamuuliza Mwenyezi Mungu na atamwitikia. Atasema: Ewe Mola Wangu nakuomba kwa haki ya Muhammad na Ahlul-Baiti wake unihu-rumie. Mwenyezi Mungu atamfunulia Jibril (as) teremka kwa mja wangu mtoe. Jibril atasema: ‘Namna gani mimi nitateremka motoni.’ Mwenyezi Mungu Mtukufu atasema: ‘Hakika mimi nimeshauamuru uwe baridi na salama kwako.’ Jibril atasema: ‘Ewe Mola Wangu nitajua je sehemu yake.’ Mwenyezi Mungu atasema: ‘Hakika yeye yuko katika shimo la Sijiyn.’ Jibril atateremka motoni na kumkuta amefungwa uso wake atamtoa na atasimama mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Hapo Mwenyezi Mungu atasema: ‘Ewe mja Wangu muda gani umekaa motoni ukiniomba?’ Atasema. ‘Ewe Mola Wangu mimi sijui.’ Mwenyezi Mungu atasema: ‘Ama kwa mamlaka Yangu na utukufu Wangu kama si kwa ajili ya wale ulioniomba kwa haki yao Kwangu ningerefusha udhalili wako motoni lakini nimehukumu katika nafsi Yangu kwamba hatoniomba mja kwa haki ya Muhammad na Ahalul-Baiti wake isipokuwa nitamsamehe yale yaliyopo baina Yangu na yake, na nimesha kusamehe leo.’ Kisha ataamuriwa kwenda peponi.”¹⁶³

¹⁶³ *Mustadrakul-Wasail* cha Nuriy chapa ya Muasasati Aalil-Bayt, Jz: 5. uk: 228 mlango wa 35 *Istihbaab tawasaul fi Duaai bi Muhammad wa Aali Muhammad*, Hadith namba 5759

SWALA INAYOLINGANA NA KUKHITIMISHA QUR’ANI MARA 12,000

Kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) amesema:

“Mwenye kuswali rakaa mbili siku ya Ijumaa kwa kusoma Sura Ikhlasi mara hamsini na akasema mwisho wa Swala yake:

اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى النَّبِيِّ الْأَمِيِّ.

Mwenyezi Mungu atamsamehe yaliyotangulia katika dhambi zake na yajayo na kana kwamba amesoma Qur’ani yote mara kumi na mbili elfu.”¹⁶⁴

SHUFAA YA MANABII ELFU MOJA

Kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) amesema:

“Rakaa mbili anazoswali mtu katika usiku wa Ijumaa kwa kusoma katika kila rakaa Alhamdu na Ayatul-Kursiyyi mara moja na Sura Ikhlasi mara kumi natano, na kusema mwisho wa Swala yake mara elfu moja:

اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى النَّبِيِّ الْأَمِيِّ.

Mwenyezi Mungu atampa Shufaa ya Manabii elfu moja na atamwandikia Hija kumi na Umra, na Mwenyezi Mungu atampa kasiri peponi pana kama vile mji mpana duniani.¹⁶⁵

¹⁶⁴ Rejea iliyotangulia Jz: 6, uk: 81 mlango (*Istihbaab Swalatil-Maghribati laylatil-Juma ’ati*)

¹⁶⁵ *Mustadrakul-Wasail* cha Nurii chapa ya Muasasati Aalil-Bayt Qum 1408 A. H. Jz: 6, uk: 82 mlango wa 34 Hadith ya 37 na ya 6486 katika mtirirko

KUJIBIWA DUA

Amesema Imam as-Sadiq (as):

“Anapoomba mmoja wenu basi na aanze kwa kumswalia Muhammad na Aali zake kisha aseme: ‘Nifanyie kadha wakadhaa’ hakika mja anaposema: *‘Allahumma Swali Alaa Muhammad Wa Alaa Ahli Baitihi’* anakubaliwa. Na anaposema: ‘Nifanyie kadhaa wakadhaa’ Mkarimu hawezi kumkatilia baadhi na kumkubalia baadhi.”¹⁶⁶

KWA NINI MAHARI YA SUNNAH YAMEKUWA NI DIRHAMU 500?

Kutoka kwa Husein bin Khalid amesema: Nilimuuliza Hasan (as) kuhusu mahari ya Sunnah imekuwaje yamekuwa ni mia tano? Akasema:

“Hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu amewajibisha katika nafsi yake kwamba muumini hatotoa takbira mia moja na kumsabih mara mia moja na kumhimidi mara mia moja na kufanya tahlili mara mia moja na kumswalia Muhammad na Aali zake mara mia moja na kisha kusema: ‘Ewe Mwenyezi Mungu niozeshe Hurulaini’ isipokuwa Mwenyezi Mungu atamuozesha Hurulaini na atajaalia kuwa hayo ni mahari. Kisha Mwenyezi Mungu al-imfunulia Nabii Wake (saww) kwamba mahari ya Sunnah kwa waumini wa kike ni dirihamu mia tano. Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akafanya hivyo, na muumini yejote akiposa kwa ndugu yake binti yake na mwenye kuposa akataja mahari yake kuwa ni dirihamu mia tano lakini akakataa kumuza basi ajue amevunja heshima na haki ya muumini na anastahili kwa Mwenyezi Mungu kutokuoza Hurulaini.”¹⁶⁷

¹⁶⁶ Rejea iliyotangulia Jz: 5, uk: 225 mlango wa 34 Hadith na: 8 ya 5751 katika mtiririko

¹⁶⁷ *Al-Kafiy* cha Kullainiy cha Darul-Kutubil-Islamiyati, Teheran 1365 A. H. Jz: 5, uk: 376 Hadith na: 7 mlango wa *Sunnatu fityl-muhuri*.

KISA CHA NG'OMBE WA BANI ISRAIL

Lilitokea tukio katika Bani Israil na hakujulika na muuwaji; Mwenyezi Mungu akamfunulia Musa (as): “Waambie Bani Israil hakika Mwenyezi Mungu atawabainishia hilo, anawaamuru mumchinje ng’ombe na mumpige kwa baadhi yake, aliyeuliwa atafufuka na kuwaambia ni nani aliyemuwa.” Hayo ni yale aliyoyaeleza Mwenyezi Mungu Mtukufu: “**Na aliposema Musa kwa watu wake hakika Mwenyezi Mungu anawaamuru kuchinja ng’ombe,**” mkitaka kumjua muuwaji na kumpiga kwa baadhi yake atafufuka na kumtaja muuwaji. Wakasema: “**Ewe Musa unatufanyia mzaha**” na shere, unadai kuwa Mwenyezi Mungu anaamuru tuchinje ngo’mbe na kuchukua kipande cha mfu na kumpiga nacho maiti na hatimaye atafufuka mmoja kati ya wafu wawili kwa kuguswa na sehemu ya maiti mwingine, itakuwaje hiyo? Musa akasema: “**Najikinga na Mwenyezi Mungu kuwa kati ya majahili.**” Mwenye kunasibisha kwa Mwenyezi Mungu ambayo hajaniambia mimi.

Wakamwambia: “**Ewe Musa muombe Mola Wako atubainishie ni ng’ombe yupi**” yaani ni zippi sifa zake ili tumjue. Musa akamuuliza Mola Wake Mtukufu, na Mwenyezi Mungu akasema: “Hakika ni ng’ombe sio mkubwa wala si mdogo bali ni wa wastani baina ya hayo, yaani baina ya mdogo na mkubwa “**fanyeni mnay-oamrishwa.**” “**Wakasema ewe Musa muombe Mola Wako atubainishie rangi yake**” Musa akasema kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu baada ya swali na jibu: “**Hakika ni ng’ombe wa njano rangi imeiva sana inawapendezesha watazamaji**” kwa umbo lake na rangi yake na mng’aro wake. “**Wakasema muombe Mola Wako atubainishie ni yupi**” sifa zake? Akasema kutoka kwa Mwenyezi Mungu: “**Hakika anasema ni ng’ombe asiyetumikishwa kwa kilimo**” yaani ambaye hajatumikishwa kulima ardhi “**wala anay-**

enywesheleza mimea,” yaani na asiwe katika wale wanaobeba maji wala kuzungusha chombo kinachovuta maji, ambaye ameepukana na hayo yote, aliye safikutokana na kasoro zote, asiye na aibu na **“asiye nabaka humo,”** yaani asiye na rangi nyingine humo.

Waliposikia maelezo haya na jambo likatulizana kwao wakamtafuta huyu ng’ombe na hawakumpata isipokuwa kwa kijana wa Kibani Israil ambaye Mwenyezi Mungu alimuonyesha Muhammad, Ali na wema katika kizazi chao usingizini na wakamwambia: “Hakika wewe ni mwenye kutupenda mwenye fadhila na sisi tunataka kukupa baadhi ya malipo duniani, watakapotaka kununua ng’ombe wako usiwauzie ila kwa amri ya mama yako kwani Mwenyezi Mungu atamfunulia am-bayoyatakutajirisha wewe na kizazi chako.”

Kijana akafurahi na kaamu wakamjia wanataka ng’ombe wake wakasema: “Kiasi gani unamuza ng’ombe wako?” Akasema dinari mbili na maamuzi ni ya mama yangu. Wakasema: “Tumeridhika kwa bei ya dinari moja.” Alipomuuliza mama yake alisema: “Ni dinari nne.” Akawapa habari, wakasema: “Tunakupa dinari mbili.” Akamwambia mama yake, mama akasema: “Ni dinari mia moja.” Wakaendelea kuomba kwa thamani nusu ya ile anayosema mama, na mtoto akaendelea kurejea kwa mama yake, na mama akaende-lea kuongeza thamani hadi thamani yake ikafikia ujazo wa ngozi ya ng’ombe, ujazo mkubwa kabisa wa dinari. Ikawawajibikia kununua kisha wakamchinja wakachukua kipande, nacho ni shina la mkia ambalo kwalo mwanadamu kaumbwa, na kwalo atarejeshwa atakaporejeshwa katika umbo jipy. Wakampiga kwa kipande hicchona wakasema: “Eee Mwenyezi Mungu kwa jaha ya Muhammad na Aali zake watukufu watoharifu mhuishe maiti huyu ili atuambie ni nani muuwaji wake.” Akasimama akiwa salama mzima na akasema: “Ewe Nabii wa Mwenyezi Mungu wameniuwa hawa watoto wa ami yangu wamenionea husuda kwa binti wa ami yangu,

hivyo wakaniuwa na wakanitupia katika sehemu ya hawa ili wa-chukue fidia yangu.” Musa akawachukua wale wanaume wawili na akawauwa.

Na kabla ya kufufuka maiti alipigwa kwa kipande cha ng’ombe akawa hajafufuka, wakasema: “Ewe Nabii wa Mwenyezi Mungu yako wapi aliyotuahidi Mwenyezi Mungu?” Musa akasema: “Umesema kweli. Hayo ni juu ya Mwenyezi Mungu Mtukufu kuyatimiza.” Mwenyezi Mungu akamfunulia: “Ewe Musa mimi sikhali fu miadi lakini wampe kijana thamani ya ng’ombe wake, wajaze ujazo wa ngozi yake dinari kisha nitamfufua huyu.” Wakakusanya mali zao na Mwenyezi Mungu akatanua ngozi ya ng’ombe hadi uzani wa ujazo wa ngozi ukafikia dinari 500,000,000.

Baadhi ya Bani Israil wakamwambia Musa (as) na hiyo ni mbele ya aliyeuliwa aliyefufuliwa kwa kupigwa na sehemu ya ng’ombe: “Hatuju ni kipi cha ajabu zaidi, Mwenyezi Mungu kumhuisha huyu na kumtamkisha kwa aliyotamka au kumtajirisha huyu kijana kwa mali hizi nyingi?” Mwenyezi Mungu akamfunulia: “Ewe Musa waambie Bani Israil: Mwenyekutaka kati yenu niyaboreshe maisha yake duniani na kutkuza makazi yake peponi na kuondoa majuto yake kuititia Muhammad na Aali zake wema basi na afanye kama alivyofanya kijana huyu; Hakika ye ye alishasikia kutoka kwa Musa bin Imrani utajo wa Muhammad, Ali na Aali zao wema, na alikuwa ni mwenye kuwaswalia, na kuwafadhilisha wao zaidi ya viumbe vyote majini, wanadamu na malaika, kwa ajili hiyo nimempelekea mali nyingi ili aneemeke kwa uzuri na atukuke kwa zawadi, na apendeke kwa umaarufu wake kwa wenye mapenzi na awafedheheshe kwa pato lake wenye uadui.”

Kijana akasema: “Ewe Nabii wa Mwenyezi Mungu namna gani nitahifadhi mali hii au namna gani nitajikinga na uadui wa wenye

kunifanyia uadui na husuda ya mwenye kunihusudu kwa ajili yake ?” Akasema: “Isomee mali hiyo Swala uliyokuwa ukimswalia Muhammad na Aali zake wema, uliyokuwa ukimswalia kabla ya kupata mali kwani aliyekuruzuku mali kwa kauli hiyo pamoja na usahihi wa itikadi ataihifadhi vilevile kwa kauli hii pamoja na usahihi wa itikadi.”

Kijana akasema hivyo basi hakuna aliyemhusudu ili kufisidi, au mwizi aliyekusudia kumwibia au mnyang’anyi kumnyang’anya isipokuwa Mwenyezi Mungu alimlinda dhidi yake kwa upole wake hadi yeze mwenyewe akajizua kumdhulumu kwa hiyari au kwa ku-zuiliwa na balaa au hadaa au kwa madhara.

Musa (as) alipomwambia kijana kuhusu kumsalia Mtume Muhammad (saww) na Mwenyezi Mungu akawa ni mlinzi wa mali yake, aliyefufuliwa alisema: “Eee Mwenyezi Mungu nakuomba kwa yale aliyokuomba kwayo kijana huyu, kwa kumswalia Muhammad na Aali zake wema na kutawasali kwao ili unibakishe duniani hali ni mwenye kuneemeka katika umri wangu, mwenye kuburudika na binti wa ami yangu na kuwafedhehesha maadui zangu na wenyе kunihusudu na niruzuku humo kheri nyingi nzuri.”

Mwenyezi Mungu akamfunulia: “Ewe Musa, hakika kijana huyu aliyefufuliwa baada ya kuuliwa ana miaka sitini na nimeshampa kwa maombi yake na kwa kutawasali kwake kwa Muhammad na Aali zake wema miaka sabini ili atimize miaka 130 hali yakuwa ni mzima wa hisia zake, imara wa nguvu zake na shahawa zake, anaburudika kwa halali za dunia hii na ataishi wala hatotengana naye, wala yeze hatomwacha, itakapofika ajali yake pia itafika ajali ya mwenza wake vile vile na watakufa pamoja nakwenda katika Pepo Yangu pamoja, humo wataendelea kuwa mke na mume wenyе kuneemeka, na lau huyu muovu angeniomba, ewe Musa kwa mfano wa aliyotawasali kwayo huyu kijana pamoja na usahihi wa itikadi yake ili nimkinge

na husuda na nimkinahishe kwa niliyomruzuku, na huo ndio ufalme mtukufu ningefanya hivyo, na kama angeniomba hayo pamoja na toba ili nisimfedheheshe nisingemfedhehesha, na ningewaondolea hawa mapendekezo ya kumdhihirisha muuwaji na ningemtajirisha kijana huyu kwa njia isiyokuwa hii kwa kiasi hiki cha mali. Na lau akiniomba baada ya kufedheheshwa na akatubia Kwangu na akatasali kwa mfano wa wasila wa kijana huyu ili niwasahaulishe watu kitendo chake baada ya kuwatuliza mawalii wa maiti ili wamsamehe kisasi basi ningefanya hivyo na ingekuwa haabitshwi kwa kitendo chake na yejote na wala asingetajwa na yejote, lakini hiyo ni fadhillila nampa ninayemtaka na Mimi ni Mwenye fadhila kubwa na namnyima ninayemtaka na Mimi ni Mwenye enzi Mwenye hekima.”

Baada ya muda kabilia hilo likapiga kelele na kusema: “Tume-kuwa mafakiri tumetoa kwa kujikinga na tumefilisika kwa ukaidi wetu kwa kichache chetu na kingi chetu, Muombe Mwenyezi Mungu – Ewe Musa – atupanulie riziki.” Musa (as) akawaambia: “Ole wenu ni upofu ulioje wa nyoyo zenu! Je, hamjasikia dua ya kijana mwenye ng’ombe na aliyomrithisha Mwenyezi Mungu utajiri? Au hamjasikia dua ya kijana aliyeuliwa ambaye amefufuliwa na alicho-faidika katika umri mrefu na furaha na kuneemeka kwa hisia zake na mwili wake na akili yake? Kwa nini hamumuombi Mwenyezi Mungu Mtukufu mfano wa dua yake na kutawasali kwa Mwenyezi Mungu kwa mfano wa wasila wao ili aondoe ufakiri wenu na kuonda mvunjiko wenu na kuziba pengo lenu ?”

Wakasema: “Eee Mwenyezi Mungu tunakimbilia kwako na katika fadhila zako tumetegemea, ondoa ufakiri wetu na ziba pengo letu kwa jaha ya Muhammad, Ali, Fatima, Hasan, Husein na wema katika kizazi chao.” Mwenyezi Mungu akamfunulia: “Ewe Musa waambie viongozi wao waende kwenye gofu la Bani fulani na wafunue sehemu kadhaa katika sehemu hiyo hiyo, sehemu ya juu ya ardhi yake

kidogo, na watoeyaliyomo humo kwani ni dinari 10,000,000,000 ili wamrejeshee kila aliyelipa katika thamani ya ng'ombe huyu thamani aliyolipa ili zirejee hali zao, kisha wagawane baada ya hapo kitakachobaki, nazo ni dinari 500,000,000, apewe kila mmoja kwa kadiri alivyolipa katika balaa hili ili iongezeke mali yao, hayo ni malipo ya kutawasali kwao kwa Muhammad na Aali zake wema na itikadi yao juu ya ubora wao (as).”¹⁶⁸

ARSHI YANYANYUKA KWA KUMSWALIA MUHAMMADI (S.A.W.W.) NA AALI ZAKE (A.S.)

Katika tafsiri ya Imam al-Askariy (as), Imam amesema katika kauli yake (swt):

“Walipenda wengi wa Ahlul-Kitab lau wangewarejesheni baada ya kuamini kwenu kuwa makafiri,” kwa yale wanayoapokea dhidi yenu kati ya shubha **“kwa husuda ya nafsi zao”** kwenu, kwa kuwakirimu kwenu kwa Muhammad, Ali na Aali zao wema, **“baada ya kuthibiti haki kwao”** kwa muujiza unaoonyesha juu ya ukweli wa Muhammad (s.a.w.w.) na fadhilza za Ali na Aali zao (a.s.). **“Sameheni na kuweni wapole”** kutokana na ujahili wao na kabilaneni nao kwa hoja na ondoeni batili yao **“hadi Mwenyezi Mungu alete amri yake”** kwa kuperigana siku ya ufunguzi wa Makka, wakati huo mtawaondoa katika mji wa Makka na katika kisiwa cha kiarabu na wala havatamwacha kafiri, **“hakika Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kila kitu”** na kwa uwezo Wake juu ya vitu amekadiria ambayo yanamasilahi kwenu katika kumwabudu kwenu katika kuongoza na kukabiliana nao katika mjadala ambao ni mzuri.

¹⁶⁸ *Biharul-Anwar* cha al-Majlisiy chapa ya Muasasatil-Wafaai, Beirut 1404 A. H. Jz: 13, uk: 269 mlango wa 9 (*Qiswatu dhabihil-Baqarah*) Hadith ya 7

“Na hiyo ni kwamba Waislam walipopatwa na balaa siku ya Uhudikaumu katika mayahudi walimjia Ammar bin Yasir na Hudhaifa bin al-Yamani baada ya masiku wakawaambia: “Je, hamuoni yaliyowapata siku ya Uhudi? Hakika anapigana vita yake kama mmoja wa watafuta dunia, mara anashinda na mara inamgeuka, acheni dini yake.” Hudhaifa akasema: “Mwenyezi Mungu awalaani sitokaa nanyinyi wala sitosikiliza maneno yenu naiogopea nafsi yangu na dini yangu hivyo nakimbia nayo kutoka kwenu.” Akasimama akakimbia kutoka kwao. Ama Ammar bin Yasir hakusimama lakini alisema: “Enyi Wayahudi hakika Muhammad (saww) alishaahidi masahaba wake ushindi siku ya Badri kama watasubiri, hivyo walisubiri na wakashinda na alishaahidi ushindi siku ya Uhudi vilevile kama watasubiri, wakafeli na wakakhali na kwa sababu hiyo yaliwapata yaliyowapata, na lau wao wangetii na wakasubiri na wasingekhalifu wangeshinda.”

“Wayahudi wakamwaambia: “Ewe Ammar kama wewe utam-tii Muhammad atawashinda wakuu wa Kikuraishi pamoja na udhaifu wa miundi yako?” Akasema: “Ndio, naapa kwa Mwenyezi Mungu ambaye hakuna mungu isipokuwa Yeye, kwamba amemtuma kwa haki kuwa Nabii Muhammad alishaniahidi katika fadhila na hekima ambayo alinifahamisha katika utume wake na akanifahamisha katika fadhila za ndugu yake na wasii wake na wema watakaomfuata baada yake na akanitaka kujis-alimisha kwa kizazi chake chema na ameniamuru kuomba dua kupidia kwao katika matatizo na balaa na ameniahidi kwamba hatoniamuru jambo nikaliamini humo na nikatii isipokuwa nitalifikia hata kama angeniamuru kuiangusha mbingu au kuinyanya ardhi hadi mbinguni basi Mwenyezi Mungu angeupa mwili wangu nguvu kwa miundi yangu hii miembamba.”

Wayahudi wakasema: “Hapana Wallahi ewe Ammar, Muhammad ni mdogo mno mbele ya Mwenyezi Mungu kuliko hayo,

na wewe ni duni mno mbele ya Mwenyezi Mungu na mbele ya Muhammad kuliko hayo.” Na kulikuwa hapo na wanafiki arobaini, Ammar akasimama kwao na akasema: “Nimeshawafikishia hoja ya Mola Wangu na nimewapa nasaha lakini nyinyi ni wenye kuchukia nasaha.”

Akaja kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), Mtume wa Mwenyezi Mungu akamwambia: “Ewe Ammar imenifikia habari yenu, ama Hudhaifa alikimbia kwa kuichelea dini yake kwa shetani na marafiki zake, naye ni katika waja wa Mwenyezi Mungu wema, ama wewe ewe Ammar hakika wewe umepigana kwa ajili ya dini ya Mwenyezi Mungu na umetoa nasaha kwa ajili ya Muhammad Mtume wa Mwenyezi Mungu, wewe ni katika wapiganaji jihadi katika njia ya Mwenyezi Mungu wenye fadhila.”

Wakati Mtume wa Mwenyezi Mungu na Ammar wanazungumza wakaja Mayahudi ambao walizungumza nae, wakasema: “Ewe Muhammad huyu hapa sahaba wako anadai kama utamwamrisha kui-teremsha mbingu ardhini au kuinyanya ardhi mbinguni ataamini na atatii na ameazimia kutekeleza, na kwamba Mwenyezi Mungu angemsaidia juu ya hilo, na sisi tutatosheka kwake na kwako kwa kilicho duni ya hicho kama kweli weweni Nabii, tumetosheka Ammar pamoja na wembamba wa miundi yake abebe jiwe hili.” Na jiwe lilikuwa limetupwa mbele ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) nyuma ya Madina, na hukusanyika hapo watu mia mbili ili kulisogeza na kama angelibebeshwa miundi yake ingevunjika na kusambaratika mwili wake.

Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: “Msidharau miundi yake hakika ni mizito katika mizani ya mema yake kuliko Thaur, Thabiyr, Hiraai na Abi Quabais bali kuliko ardhi yote na vili-vyomo juu yake, na hakika Mwenyezi Mungu ameyafanya mepesi kwa kumswalia Muhammad na Aali zake yale yaliyomazito kuliko

milima hii, ameifanya arshi kuwa nyepesi kwa malaika nane baada ya kuwa hawawezi licha ya idadi yao kubwa na kundi lao kubwa.” Kisha akasema Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww): “Ewe Ammar amini utii wangu na sema: “Ewe Mwenyezi Mungu kwa jaha ya Muhammad na Aali zake wema nitie nguvu.” Mwenyezi Mungu ataku-sahilishia ninayokuamuru kama alivyofanya sahali kwa Kaalib bin Yohana pale alipoweza kuvuka bahari ya maji akiwa juu ya Farasi wake na kukimbia juu yake kwa kumuomba kwake Mwenyezi Mungu kwa jaha yetu Ahlul-Bait (as).” Ammar akasema: “Naamini.” Akabeba jiwe juu ya kichwa chake na akasema: “Kwa baba yangu na mama yangu ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, naapa kwa ambaye amekutuma kwa haki kuwa Nabii njepesi katika mikono yangu kuliiko kichokolea meno ninachokishika.”

Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: “Litupe angani litafika kilele cha mlima ule.” Na akaashiria kwa mkono wake kwenye mlima kwa umbali wa farsakh (kilometra) nne. Akalitupa likapaa angani hadi likatua juu ya kilele cha mlima. Kisha Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akawaambia wayahudi: “Je, mmeona?” Wakasema: “Ndio.” Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akamwambia Ammar simama juu ya kilele cha mlima utakuta huko jiwe kubwa zaidi libebe na ulirudishe kwangu. Ammar akapiga hatua moja ardhi ikafupishwa kwake na hatua ya pili ikawekwa juu kilele cha mlima, akachukua jiwe kubwa zaidi na akarejea kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu kwa hatua ya pili tu. Kisha Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akamwambia Ammar: “Lipige kwa nguvu sana ardhini.” Wayahudi wakaogopa na wakakimbia. Ammar akalipiga juu ya ardhi likasambaratika likawa kama vumbi lililopeperushwa na likamalizika.

Akasema Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww): “Aminini enyi-Wayahudi kwani mmeshashuhudia hoja ya Mwenyezi Mungu.” Baa-

dhi wakaamini na baadhi yao uovu ukawashinda. Kisha Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: “Enyi Waislamu je mnajua nini mfano wa jiwe hili?” Wakasema: “Hapani ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu.” Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: “Naapa kwa ambaye amenituma kwa haki kuwa Nabii, hakika mtu katika wafuasi wetu atakuwa na madhambi na makosa makubwa zaidi kuliko milima ya ardhini na ardhi yote na mbingu iongezwe maradufu zaidi, hana isipokuwa kutubu na kuirejesha upya nafsi yake katika mapenzi yetu Ahlul-Bayt, hapo atakuwa amezipiga dhambi zake ardhini kuliko kupiga Ammar jiwe juu ya ardhi, na kwamba mtu atakuwa na utii kama vile mbingu, ardhi, milima na bahari akikufuru tu uongoziwa Ahlul-Bayt hapo atakuwa ameupiga mno ardhini kuliko kupiga kwa Ammar jiwe hili ardhini na kumalizika kama vile kusambaratika kwa jiwe hili, na atakaporejea akhera hatokuta jema, na dhambi zake ni maradufu zaidi ya milima, ardhi na mbingu, na hisabu yake itakuwa kali na itadumu adhabu yake.”

Ammar alipoona katika nafsi yake ile nguvu ambayo alipiga kwayo jiwe lile ardhini na kusambaratika ikamchukua hali ya furaha akasema: “Je, unaniruhusu ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) nipigane na hawa Mayahudi ili niwauwe wote kwa yale niliyopewa mionganoni mwa nguvu hizi?” Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: “Ewe Ammar hakika Mwenyezi Mungu anasema: “Samehe na kuwa mpole hadi Mwenyezi Mungu alete amri yake” kwa adhabu yao na ataleta ufunguzi wa Makka na mengine yaliyoahidiwa.”¹⁶⁹

¹⁶⁹ Rejea iliyotangulia Jz: 91, uk: 17 na 18 mlango wa 28 *al-Istishifaa'u bi Muhammad wa Aalihi fiy Du'ai* Hadith ya 12.

KUONDOA HUZUNI NA KUTAKASIKA NA DHAMBI

Waislamu walikuwa wanakereka sana kwa ushawishi wa Mayahudi na wanafiki kwa kutia shubha katika dini, Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema:

“Je niwafahamishe yanayoondoa kero ya nyoyo zenu pale hawa maadui zenu wanapowashawishi?” Wakasema: “Ndio, ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww).” Hapo Mtume wa Mwenyezi Mungu akawaamuru kama alivyowaamuru wale waliokutwa pamoja naye katika shamba ambalo Makuraishi walimzingira humo na hapo nyoyo zao zikapatwa na dhiki na zikachafuka nguo zao, Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) aliwaambia: “Pulizeni nguo zenu na panguseni kwa mikono yenu zikiwa katika miili yenu, na hali nyinyi mnamswalia Muhammad na Aali zake wema, hakika zitasafika na kutoharika, zitakuwa nyeupe na zitakuwa nzuri, na itawaondolea kero katika nyoyo zenu.” Wakafanya hivyo na nguo zao zikawa kama alivyosema Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww).

Wakasema ajabu, ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu kwa sisi kukuswalia wewe na Aali zako namna gani zimetoharika nguo zetu? Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema:

“Hakika twahara inayopatikana katika nyoyo zenu kwa kumsawalia Muhammad na Aali zake, na inayoondoa mifundo na husuda, na inayotwaharisha miili yenu kutokana na madhambi, ni kali kuliko ile inayotwaharisha nguo zenu. Na hakika inafuta madhambi vizuri zaidi kutoka katika daftari zenu kuliko inavyoondoa uchafu wa nguo zenu, na hakika kuzitakasa nyoyo zenu ili yaandikwe mema yenu maradufu ni bora zaidi kuliko kuzitakasa nguo zenu.”¹⁷⁰

¹⁷⁰ Rejea iliyotangulia

SABABU YA KUSAHAU NA TIBA YAKE

Katika Hadith ni kwamba Hasan (as) alimjibu muulizaji ambaye al-imuuliza juu ya kukumbuka na kusahau, akasema:

“Hakika moyo wa mtu uko katika sehemu na katika sehemu kuna kifuniko, mtu anapomswalia Muhammad na Aali Muhammad Swala kamilifu kifuniko hicho kinafunguka na kuangazia moyo na mtu anakumbuka aliyokuwa ameyasahau, na kama hakumswalia Muhammad na Aali zake au akipunguza katika kuwaswalia kifuniko hicho kinajifunika sehemu hiyo na moyo unakuwa na giza na mtu anasahau aliyokuwa anayakumbuka.”¹⁷¹

KISA CHA MTU ANAYEMSWALIA MTUME (SAWW) DAIMA

Sufian Thauriy amesema: “Mwaka mmoja nilipokuwa natembea kwenda katika Ka’aba tukufu katika siku za Hija nilifika Madina tukufu, na katika kaburi tukufu la Mtume (saww) nilimuona kijana ambaye alikuwa anaonekana kuwa ni katika watu wema na athari za uchamungu zilikuwa zinaonekana katika uso wake, na alikuwa anazunguka Haram tukufu na alikuwa hakariri isipokuwa: “*Allahumma Swali Alaa Muhammad Wa Aali Muhammad.*” Nilitaka kumuuliza: Kwa nini husomi dua na nyuradizingine nyingi zilizopokewa? Lakin kundi likatenganisha baina yangu na baina yake na swali hili likabakia linanitatiza.

Nilikwenda Makka na nikamuona yule kijana katika hali ya tawafu na hapa pia sikumsikia anakariri isipokuwa kumswalia Muhammad na Aali zake (a.s.), nilikusudia kumsogelea na kumuuliza

¹⁷¹ Wasaili Shi’ah chapa ya Muasasati Aalil-Bayt Qum 1409H Jz: 7, uk: 198 mlango wa 37 (*Istihbaab Swalati alaa Muhammad wa Aalihi*) Hadith 9106

swali hili kwa mara nyingine, lakini msongamano ukazuia baina yangu na baina yake kwa mara nyingine, nikasikitika kwamba fursa imenipita tena na swali likabakia akilini mwangu.

Katika siku ya Arafah niliwaona watu wote wanashughulika na dhikri na nyuradi mbalimbali na nikamuona yule kijana mara nyingine naye anasema: “*Allahumma Swal Alaa Muhammad Wa Aali Muhammad.*” Alikuwa anakaa na kumswalia Nabii na Ahali zake na anasimama na kukariri: “*Allahumma Swal Alaa Muhammad Wa Aali Muhammad.*” na anatembea na huku anawaswalia. Nikamso-gelea nikamsalimia na nikazungumza pamoja naye nikamwambia: Nimekuftilia toka Madina hadi huku katika hali zako zote, unam-swalia Muhammad na Aali Muhammad (a.s.), na mimi nashangaa kushikamana kwako na utajo huu wakati watu wako katika hali ya kuswali na aina za dhikri na dua, kuomba, kufanya istighifari na unyenyekevu, ni nini hii ninayoiona kwako katika utajo huu kiasi kwamba hukuacha na kusoma uradi mwengine?

Akasema: ‘Hakika nimeona kwayo mambo mengi na kwa sababu hiyo unaniona nimeandama Swala hii ya kumswalia Mtume (saww) bila kusimama. Na kati ya mambo hayo ni kisa ambacho nitakusimulia ili ujue ni kitu gani inafanya Swala ya Muhammad na Aali Muhammad (a.s.).

‘Mwaka jana nilitoka pamoja na marehemu mzazi wangu kwenda Makka. Mzazi wangu akaugua katika moja ya nyumba na akajiengua na safari na nikalazimika kubaki pamoja naye na nikakodisha nyumba na nikamhamishia humo, ilipoingia jioni niliwashaa taa na nikaweka kichwa chake juu ya mto pembezoni mwangu, nikawa namwangalia ikawa ajali yake imekaribia na akaanza kupatwa na sakaratil-mauti. Uso wake ukaanza kuwa mweusi, nikafadhaika kwa mandhari haya nikasema *Innaa Lillahi Wainnaa Ilaihi Rajiuna*, nikajisemea kuiambia nafsi yangu vipi nitakabiliana na watu kutaka-

pokucha watakaposikia na kuja ili kumuosha mzazi wangu na kumkafini, watakapoona uso wake umeshakuwa mweusi? si watasema: Ni dhambi gani ameifanya huyu mzee hadi akawa katika mwisho huu?

‘Nikazindukana kisha nikasimama nakufunika uso wake, ni kaangua kilio kwa huzuni kwa kumkosa mzazi wangu, bali kibaya zaidi kuliko hayo dhiki nitakayokabili ana nayo kwa watu hususan kutokana na weusi wa uso, baada ya kuchoshwa na wingi wa kulia usingizi ulinipitia pembezoni mwa mzazi wangu, basi nikaona katika ulimwengu wa njozi mtu mwenye nuru angavu, mzuri wa mandhari sijawahi kuona yeyote mfano wake kabla yake, amevaa vazi sijaona mfano wake, amejivika kilemba cheupe angavu sijaona kilemba cheupe mfano wake, na kilikuwa kinanukia harufu ya manukato sijawahi kunusa katika maisha yangu mfano wake abadani, aliingia na akakaa karibu na kichwa cha baba yangu, na akafunua nguo niliyokuwa nimefunika uso wake kisha akapangusa juu yake kwa mkono wake mtukufu uso wa baba yangu ukawa mweupe ghafla.

‘Nikajitupia kwenye miguu ya huyu bwana mtukufu na nikasema kwa kustaajabu. Bwana wangu, ni nani wewe ambaye umeniokoa kutokana na shida hii kubwa? Akasema: Mimi nimwenye kushushiwa Qur’ani Muhammad bin Abdillahi (saww). Nikasema: Baba yangu amefanya nini hadi akastahili kufa mweusi wa uso? Akasema (saww): Alikuwa mwaasi lakini aliкуwa na jambo na nimekuja kumuokoa kwa ajili ya jambo hilo, nalo ni kwamba aliкуwa anadumu katika kuniswalia mimi na Ahlul-Bait wangu (a.s.), aliкуwa anankumbuka daima na sisi pia hatukumsahau na kwa ajili hiyo nimekuja hapa.’

Kijana anasema: Nikafadhaika katika usingizi wangu kwa hofu na baada ya kuondoa nguo nikakuta uso una mwanga unameremeta

kama mbalamwezi, na tangu wakati huo nikajua yale inayoyabeba Swala ya Muhammad na Aali zake (a.s.) katika sifa mahususi.”¹⁷²

BUSU LA NABII (SAWW)

Al-Marhum al-Haji Sheikh Ali Akbar An-Nahawandiy – kati ya Maulamaa wa Mashhad Tukufu - amesema: “Mmoja wa wachamungu mwanazuhud alikuwa anasema: ‘Nimeizoesha nafsi yangu kumswalia Muhammad na Aali zake kila siku kabla ya kulala kwa kiasi maalum. Siku moja katika moja ya nyusiku lilitembelea kundi la marafiki na chumba changu kilikuwa kimejaa, hadi usiku wa manane walipolala wote, nami nilihisi kuwa nimechoka sana lakini pamoja na hivyo sikuacha mazoea yangu nikatekeleza uradi wangu (kumswalia Muhammad na Aali zake) kisha nikalala. Usingizini nikaona kana kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) ameingia katika chumba changu na nuru ikazagaa sehemu zote za chumba wakati wa kuingia kwake, kisha akanisogelea na akasema: Uko wapi mdomo unaoniswalia mimi? Mimi nataka kuubusu. Nikaona aibu kusemani Mimi ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, kwa sababu sikuwa naona nafsi yangu inakusudiwa. Lakininikaona (saww) ananisogelea na anakaribia kwangu kisha busu lake likaupata mdomo wangu. Nikazinduka kutoka usingizini nikiwa na furaha kwa sauti yenye kusikika kutokana na wingi wa furaha, kiasi kwamba marafiki zangu wote waliokuwa wamelala pamoja na mimi chumbani walipiga kilele.”¹⁷³

¹⁷² *Qiswasu Swalawaat* uk: 30 – 33 cha Kifurusi

¹⁷³ *Qiswasu Swalawaat* uk: 30 – 33 cha Kifurusi

MIONGONI MWA BARAKA ZA KUMSWALIA MUHAMMADI (SAWW) NA AALI ZAKE (AS)

Kutoka kwa Zaidi bin Thabit amesema: “Tulitoka vitani katika moja ya vita tukiwa kikundi pamoja na Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) hadi tukafika katika njiapanda, akajitokeza bedui na hatamu za ngamia na akasimama mbele ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) na akasema: ‘Assalamu Alaika Ya Rasulallah Warahamatullahi Wabarakatuhu.’ Mtume wa Mwenyezi Mungu akamwambia ‘Waalaika Salam.’ Akasema: ‘Umeamkaje naapa kwa baba yangu na mama yangu ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu.’ Akamwambia: ‘Namshukuru Mwenyezi Mungu kwako. Nawe umeamkaje?’ Na nyuma ya ngamia ambaye alikuwa anamkokota bedui kulikuwa kuna mtu, akasema: ‘Ewe Muhammad hakika huyu bedui ameiba ngamia.’ Ngamia akalia kwa muda, na Mtume wa Mwenyezi Mungu akanyamaza akimsiliza kisha Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akamwendea yule mtu akasema: ‘Ondoka kwake kwani ngamia anashuhudia dhidi yako kwamba wewe ni muongo.’ Yule mtu akaondoka na Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akamwendea beduiakasema: ‘Ni kitu gani ulisema ulipokuwa unakuja kwangu?’ Akasema: ‘Nilisema:

اللَّهُمْ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَآلِ مُحَمَّدٍ حَتَّى لَا يَبْقَى صَلَاةُ اللَّهِ
بَارَكْ عَلَى مُحَمَّدٍ وَآلِ مُحَمَّدٍ حَتَّى لَا يَبْقَى بَرَكَةُ اللَّهِ سَلَّمَ عَلَى
مُحَمَّدٍ وَآلِ مُحَمَّدٍ حَتَّى لَا يَبْقَى سَلَامُ اللَّهِ ارْحَمْ مُحَمَّداً وَآلِ
مُحَمَّدٍ حَتَّى لَا يَبْقَى رَحْمَةً .

Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: ‘Hakika mimi nasema yale nionayo, namuona ngamia anatamka kwa mdomo wake na naona malaika wamefunika anga.¹⁷⁴

BAHARI YENYE MAWIMBI

Mmoja wa Maulamaa wa Kisuni anayeitwa Musa Dharir amesema: “Tulikuwa pamoja na marafiki na maswahiba wengi tukiwa ni wasafiri katika meli, punde tukahisi kwamba imetupwa na mawimbi kutokana na upopo mkali uliopiga baharini, kiasi kwamba tulikata tamaa na maisha na tukasameheana na tukaagana, kisha kila mmoja wetu akaanza kulia na kutawasali kwa Mwenyezi Mungu na kuweka nadhiri kama atanusurika kutokana na msiba huu atafanya kadhaa wa kadhaa, wakati tukiwa katika hali hiyo ukanipitia usingizi nikajikuta katika ulimwengu wa njozi nami nimebahatika kumuona Nabii (saww), nikatawasali kwake, naye akaniambia sema:

اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى سَيِّدِنَا مُحَمَّدٍ وَآلِهِ صَلْوَةً تُتْجِيْنَا مِنْ جَمِيعِ
الْأَخْوَالِ وَالْأَوْقَاتِ وَتُطَهِّرْنَا بِهَا مِنْ جَمِيعِ السَّيِّئَاتِ وَتَرْفَعْنَا
بِهَا عِنْدَكَ أَعْلَى الدَّرَجَاتِ وَتُبَلِّغُنَا بِهَا أَقْصَى الْغَایَاتِ مِنْ
جَمِيعِ الْخَيْرَاتِ فِي الْحَيَاةِ وَالْمَمَاتِ إِنَّكَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ

Nikazinduka kutoka katika usingizi wangu huku nikiwa nakariri Swala hii, nikawaambia marafiki zangu nao wakakariri pamoja na mimi na hatukifikisha mara (300) tufani ikawa imetulia.”¹⁷⁵

¹⁷⁴ Biharul-Anwar chapa ya Muasasati-Wafaai Beirut, 1404H Jz: 17, uk: 397 mlango wa 5 Madhhabara min I'jaazihi (saww) fiyl hayawan, Hadith 9

¹⁷⁵ Khaziynatul-Jawahir, uk: 587

NI KINGA YA USENGENYAJI

Mmoja wa mawalii wema alimlalamikia al-Khidhir (as) siku moja kutokana na kukithiri usengenyaji, na kwamba yeye kila anapowanasih i kuachana na tabia hiyo na kuwaambia kuwatabia hiyo ni katika madhambi makubwa hakika wao hawa jali maneno yake wala hawaachani na tabia hiyo mbaya. Khidhir (as) akamwambia utakapoingia katika baraza kati ya mabaraza yao naukawaona wanasegenya na unapenda wakome kumsengenya sema: “*Bismillahi Rahamani Rahiym Waswalallahu Alaa Muhammad*,” hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu atampeleka kwao malaika atakaye wakataza kufanya kitendo hiki kibaya na kuwazuia wao kila watakapotaka kusengenya, kisha al-Khidhir (a.s.) akasema: Mwanadamu anaposema wakati wa kutoka kwenye baraza lolote: “*Bismillahi Rahamani Rahiym Waswalallahu Alaa Muhammad Wa Aali Muhammad*” hakika Mwenyezi Mungu Mtukufuanamtuma kwake malaika atakayewazua wao kumsengenya.¹⁷⁶

TAJIRI NA MASIKINI

Masikini mmoja alitoka siku moja kutafuta riziki akapita katika msikiti ikiwa nikatika njia yake, na katika msikiti kulikuwa na mtu anatoa mawa idha amekaa juu ya mimbari na majilisi yake ime jaa watu, na alikuwa anawahimiza na kuwaraghibisha juu ya kumswalia Muhammad na Aali zake (a.s.). Masikini akasimama akimsikiliza, akasikia katika kauli yake: “Msizembee katika kumswalia Nabii na Aali zake kwani tajiri akimswalia Mtume Mwenyezi Mungu ana muongezea utajiri wake na masikini akimswalia Mtume Mwenyezi Mungu anamtumia riziki yake kutoka mbinguni.” Mtu huyu masikini baada ya kuondoka akawa anakariri Swala ya Nabii Muhammad na

¹⁷⁶ *Qiswasu Swalaawaat*, uk: 57

Aali zake (a.s.) bila kuacha. Zikapita siku tatu naye akiwa katika hali hii ya kumswalia Mtume, na alipotoka siku ya tatu nyumbani kwake, katika kutembea kwake alipita katikagofu moja na akajikwaa katika jiwe lililokuwa humo, alipolinyanyua akaona chini yake kifuko kimejaa dhahabu na vito vya thamani, akasema kuiambia nafsi yake: ‘Hakika mimi nimeahidiwa riziki kutoka mbinguni sitaki riziki ya ardhini.’ Kisha akarejesha jiwe juu ya kifuko na akarejea nyumbani.

Alipofika nyumbani alimsimulia mke wake yaliyomtokea, na jirani yake myahudi aliyekuwa juu ya nyumba aliquwa anasikiliza mazungumzo yake, hivyo myahudi akatoka nyumbani kwake na kukimbia haraka kwenda kwenye gofu, akaondoa jiwe na akabeba kifuko ambacho kilikuwa chini yake na akarejea nyumbani, alipofungua akaona kimejaa n’ge na nyoka, akamwambia mke wake: “Hakika jirani yetu Muislamu anatufanya uadui na amedhamiria shari kwetu, ye ye amejua kuwa mimi niko juu ya nyumba.....” na akamsimulia mke wake aliyoyasikia kutoka kwake; ili nilete ng’e na nyoka katika nyumba yangu ili atuuwe, na maadamu mambo yako hivyo basi hakika mimi nitakwenda na kichupa juu ya nyumba yake na nitakitupa toka huko kwenye nyumba yake ili ahiliki ye ye na mke wake, ili wapate waliyoyadhamiria dhidi yetu. Myahudi alipopanda juu ya nyumba akasikia yule Muislamu na mke wake wanajadiliana, mwanamke anasema: “Je, inasihi ewe mwanaume kuacha kichupa kilichojaa dhahabu na kurejea kwetu hivi hivi na sisi tunakabiliwa na ufakiri na dhiki kubwa?!” Naye mume anamwambia: “Hakika mimi natarajia riziki yetu itatuteremkia kutoka mbinguni.”

Wakati wakiwa katika hali hiyo myahudi akafungua kifuniko cha mfuko na akamimina yaliyomo humo juu yao, Muislamu aka-hisi kwamba kitu kinadondoka toka juu yao toka juu akanyanyua kichwa chake juu akaona vito vya thamani na dhahabu vinadondoka juu yake, akapiga kelele: “Tazama mbingu inanyesha dhahabu na

vitovya thamani.” Akafanya haraka kuzikusanyahuku akimswalia Muhammad na Aali Muhammaad.

Myahudi alipoona kwamba yanayotoka katika kifuko na kuteremka kwao nidhahabu akarejea na akafunga mlango wa kifuko lakinii akahisi kwamba yaliyomo yamerejea na kuwa ni nyoka na ng’e, akarejea tena na kumimina tena haraka hata haikubaki humo kitu na akajua kwamba katika jambo hili kuna siri mionganini mwa siri za ghaibu. Akakumbuka namna gani maji ya mto Nile kwa Waisrail yalikuwa maji na kwa Waqibti yalikuwa ni damu iliyoganda. Akamwita yule Muislamu toka juu ya nyumba na akasilimu haraka mbele yake bilaya kuchelewa. Vivyo hivyo masikini akawa tajiri kwa baraka za kumswalia Muhammad na Aali zake kama ambavyo myahudi alifafulu kwa neema ya Uislam na ni utukufu mkubwa ulioje kwa hawa wawili.¹⁷⁷

ADHABU YA KABURI

Mwanamke aliona usingizini mtoto wake aliye kufa anaadhibiwa kaburini, akafadhaika na akaamka analia na akaendelea katika hali ile kwa siku kadhaa, kisha akamuona mara yapili katika usingizi kuwa ni mwenye furaha na amelala pepo ya Firdausi, akamuuliza: “Mwanangu kuna nini nimekuona mara ya kwanza ni mwenye kuadhibiwa na nakuona leo katika Firdausi?”

Akasema: “Hakika adhabu hiyo ilikuwa kwa sababu ya dhambi zangu na kughafilika kwangu, ama unayoyaona katika hali yangu ya sasa ni kwa sababu mtu mwema amepita katika makaburi yetu kabla ya siku chache na akamswalia Muhammad na Aali zake mara kadhaa, kisha akatoa thawabu zake kwa watu wa makaburi yetu, Mwenyezi Mungu akatuondolea adhabu kwa baraka za Swala hiyo.”

¹⁷⁷ Rejea iliyotangulia uk: 59 - 62

Hivyo mwenye kuswali kila anapomswalia Muhammad na Aali zake katika makaburi yoyote na akatoa zawadi thawabu zake kwa watu wa makaburi hayo, hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu anawaon-dolea adhabu kwa utukufu wa Swala hiyo.¹⁷⁸

HARUFU NZURI

Amesimulia Hujatul-Islam wal-Muslimina al-Haji Muhaqiq (Mkwe wa Ayatullah al-Udhmaa al-Gulbayganiy) amesema: Amenisimulia marhum al-Akhundiyy Mullaa Ali al-Hamdaniy amesema: “Siku moja alinijia mzee mkubwa ili kulipa yaliyomuwajibikia katika khumsi, nikatambua kwamba harufu ya manukato inayotoka kwake sijawahi kuinusa kabla katu, nikamuuliza aina ya manukato am-bayo anayatumia, akasema: ‘Bwana wangu hakika harufu hii nzuri ina kisa sijamweleza yejote kabla yako, lakini kwa kuwa wewe ni bwana wangu na kiongozi wangu basi hakika nitakueleza. Niliona katika njozi katika usiku mmojawapo kwamba mimi nimebahatika kumzuru bwana wa viumbe Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), na alikuwa amekaa na pembezoni mwake kuna watu ishirini takrib-an na mimi nilikuwa katika majilisi hiyo vilevile, akasema (saww): Nani kati yenu ananiswalia kwa wingi? Nilitaka kumwambia: Bwa-na wangu hakika mimi ninakuswalia kwa wingi lakini nilinyamaza. Na katika mara yapili aliuliza (saww) swali lile lile, na hakumjibu yejote, na katika mara yatatu alipouliza (saww) ni nani kati yenu ananiswalia kwa wingi ? Niliazimia kujibu lakini nikaiambia nafisi yangu: Huenda katika majilisi kuna ambaye anamswalia zaidi kuliko mimi na hakujibu kwa kumuonea haya (saww), nikamuona anasi-mama na akaniambia: Wewe unaniswalia kwa wingi na akabusu mi-domo yangu.”¹⁷⁹

¹⁷⁸ Rejea iliyotangulia uk: 65

¹⁷⁹ Rejea iliyotangulia uk. 79

KUZUIA HATARI

Amesimulia Hujatul-Islam wal-Muslimima Mahdiy Pur katika mwakawa 1991– Mtarjumi wa kitabu cha *al-Jaziratul- Khadharau-* amesema: Mmoja wa watu wafamilia yetu kabla ya miaka minne aliona ndoto, naminikainukuu kwa Marhum Ayatullahi Swidiqiyna al-Isfahaaniy baada ya siku tatu katika mji wake. Naye akaifasiri ndoto hiyo kwa kusema: “Ilikuwa imekadiriwa katika familia yenu kufa mmoja wa watu wake katika siku ambayo ilionwa ndoto katika usingizi. Lakini hakika nyinyi mnamswalia kwa wingi Muhammad na Aali zake (a.s.) hivyo imeondolewa kwenu hatari na Mwenyezi Mungu amerefusha umri wa waliokuwa wanakabiliwa na mauti kwa baraka za kumswalia Muhammad na Aali Muhammad (s.a.w.w.).”

Nikampigia simu mmoja wa marafiki zangu Adharbaijani na baada ya kubadilishana salamu na kumuuliza juu ya hali yake akani-pa habari kwamba mtoto wangu amegongwa na lori baada ya kusafiri kwangu kwa siku tatu na akapelekwa hospitalini na bado angali katika hali ya kuzimia.

Hivi ndivyo ilivyonibainikia ukweli wa tafsiri ya ndoto hiyo na kwamba hatari imeondoka kwa mtoto wangu kwa baraka za kudumu katika kumswalia Muhammad na Aali Muhammad (a.s.).¹⁸⁰

KUMSWALIA MTUME NA PETE ILIYOPOTEA

Amesema al-Hujatul-Islam wal-Muslimima Sayyid Hasan As-Swahifiy: “Kabla ya miaka mingi nilifanya safari kwenda Tehran na wakati wakurejea kwangu Qum niligundua kwamba pete yangu ambayo najifakharisha nayo sana, nayo ni pete ya kito cha aqiqi ya Yemen ya njano iliyonakishiwa juu yake: “*Maa shaallah Laa Quw-*

¹⁸⁰ Athaaru wa Barakaati Swalawaati, uk: 93

wata Illa Biillahi Astaghfirullah” haipo pamoja na kwamba nilitafuta sana lakini sikuipata, na zikapita siku 17 na wakati wakurejea kwangu katika safari nyingine kwenda Tehran nilitumia fursa kabla ya basi kujaa wasafiri, kwa utajo wa kumswalia Mtume: “*Allahumma Swal Alaa Muhammad Wa Aali Muhammad Waa’jili Faraja Hum*” mara 1500, na nilipofikakwa mwenyeji wangu na nikalala usiku, nilisikia katika usingizi wangu mtu anasema: Pete iko mahali fulani. Na nilipoamka kwa ajili ya kuswali Swala ya Subhi nilimpa habari mwenyeji wangu juu ya ndoto yangu, alikwenda katika sehemu hiyo ambayo nimemwambia na akaja na pete.”¹⁸¹

SWALA YA MWISHO

Kutoka kwamtoto wa Marhum Ayatullah as-Shari’iy amesema: “Mzazi wangu alitoka Darab kwenda Laar ikiwa ni mwanzoni mwa masomo yake ya Kiislam, na katika siku hizo wanyama walikuwa ndio njia pekee ya usafiri, na safari ilikuwa inatimia kwa ugumu na taratibu. Na alipokuwa Laar mzazi wangu alivumilia na kukabiliana na taabu ya ugeni, lakini kuwa mbali na mama yake mchamungu na mpole haikuwa jambo rahisi kwake, hivyo aliazimia kurudi kwanza Darab hivyo alikwenda kwenye kituo cha misafara inayokwenda Darab na hakupata kipando cha kukodisha kwa sababu vilikuwa vyote vimeshakodishwa isipokuwa wanyama wawili, na wenyewe hawakodishi kwamsafiri mmoja, ambapo mzazi wangu alilazimika kulipa ujira wa kukodi wanyama wawili pamoja na kununua baadhi ya bidhaa zinazopatikana Laari zaidi kuliko Darab na kuzibeba kwenye mmoja wa wanyama wawili, na yeye kupanda mnyama mwiningine ili kuelekea Darab.

Alipowasili Darab na kuingia katika nyumba yake akamuona mzazi wake anashughulika na kufagia, na mzazi alipohisi kufika

¹⁸¹ *Qiswasu Swalaawaati*, uk: 78

kwake akamwambia kwa kusema: ‘Hee umefika mtoto wangu, nimeshamaliza sasa hivi kuhitimisha kumswalia Muhammad na Aali Muhammad.’ Ambapo inaonyesha kwamba huyu mama mchamungu alikuwa ametawasali kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kumswalia Muhammad ili mtoto wake arudi toka safarini na ali-kuwa ameshaanza kuhitimisha Swala kwa kutoa zawadi Swala mia moja kwa kila mmoja wa maasumina kumi na nne (as), na alipofika mwisho wa Swala hiyo Mwenyezi Mungu akamfikishia haja yake. Na hisia hiyo aliyokuwa nayo huko Laari ambayo ilikuwa imemtawala mtoto huyu haikuwa isipokuwa kwa amri kutoka kwa Mwenyezi Mungu ili aharakishe kuelekea katika mji wake wa Darab.”¹⁸²

KUPOTEZA KITU MUHIMU

Siku moja nilipoteza kitu muhimu nilichokuwa nakihitajia sana, nani kabaki nimeshikwa na bumbuwazi sijui cha kufanya! Nikakumbuka kumswalia Muhamamad na Aali Muhammad mara kumi, nikaweka nadhiri kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu ya kumswalia Muhammad na Aali Muhammad mara kumi kwa nia ya usalama wa Imam Swahib Zamani (as) iwapo nitakipata kitu hicho, na katika punde ileile nikakipata kitu hicho.¹⁸³

Na alikwisha jaribu mwandishi wa kitabu hiki jambo hili mara nyingi.

KARAMA ZA MTUME WA MWENYEZI MUNGU (SAWW) KABURINI

Shabliy alitoka pamoja na kundi la wanamuridi wake, walikwenda jangwani hali wameazimia Hija, na walipokuwa njiani mmoja wa

¹⁸² *Qiswasu Swalaawaati*, uk : 79

¹⁸³ Rejea iliyotangulia uk: 101

wanamuridi alipatwa na mauti, Shabliy akashikwa na bumbuwazi katika jambo lake wakati akiwa anaangalia mwili wake na anatafakari kumuosha, kumvisha sanda na kumzika, ghafla akaona mwili wake wote ni mweusi na ukawa giza kwa muda mchache kuliko kasi ya kupepesa jicho, kisha haukudumu na kabla haijapita saa weusi huo ukabadilika na kuwa weupe. Shabliy akastaajabishwa na hali ya mtu huyu, na baada ya kupata wepesi wa kumzika alimzika. Ndipo akamuona katika usingizi wake akiwa anarukaruka katika mapambo ya peponi na kichwani mwake kuna taji limepambwa kwa vito vya thamani na katika kidole chake kuna pete ya nuru imeandikwa: “Haya ni malipo ya mwenye kumswalia Muhammad na Aali zake (saww).” Akamuuliza ni sababu ipi iliyosababisha weusi wake kisha weupe? Akamwambia: “Ama weusi ulikuwa ni kwa sababu ya dhambi zangu, ilipotoka roho yangu tu katika mwili wake mwili wangu ukawa mweusi wote kwa sababu ya dhambi zangu, na ghafla nikaona mbalamwezi ya uwepo na bwana wa kizazi cha Adam (saww) ananijia na mkononi mwake anakikombe cha maji akanimwigia na akaosha kwa mikono yake mitukufu weusi wa madhambi yangu na akanivulia pambo la utukufu na akanivalisha pete ya wema. Nikamwambia: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu kwa amali gani nastahiki utukufu huu? Akasema: Kwa kuniswalia kwako daima.”¹⁸⁴ Shabliy anasema: Ikanipambanukia kwamba giza la dhambi linaondoka kwa kumswalia kipenzi cha Mwenyezi Mungu al-Mustafaa (saww).¹⁸⁴

SWALA YA MTUME (SAWW) INAOKOA DHIDI YA ADHABU YA KABURI

Kutoka kwa Shabliy vilevile amesema: Nilikuwa na jirani aliywishaa fariki, nikamuona katika usingizi na nikamuuliza: Mwenyezi Mungu amekufanyaje? Akasema: “Ewe mzee nimeshaona adhabu

¹⁸⁴ *Athaaru wa barakaatu Swalawaati*, uk: 129

kubwa na nimeteseka sana na nilishindwa kusema nilipomuona Munkar na Nakir, nikasema. Ole wangu! adhabu hii imenikuta, na nilikuwa Muislamu na nimefariki katika mila ya Uislam, ndipo Malaika wawili wakaanza kuniuliza kwa ukali, na ghafla mtu mzuri wa sura mwenye harufu nzuri akazuia baina yangu na baina yao na akanisomea majibu yao kwa njia nzuri. Nikamuuliza wewe ni nani Mwenyezi Mungu akuhurumie? Akasema: Mimi niSwala ambazo ulikuwa unamswalia Muhammad na Aali zake (a.s.) na hakika mimi nimeamriwa na nimekalifishwa kukusaidia wakati wowote unaohitaji msaada na nusura.”¹⁸⁵

AMANI KUTOKANA NA UCHUNGU, WAKATI WA KUTOKA ROHO

Mmoja wa watu wema alikwenda kumtembelea rafiki yake akamuona yuko katika hali ya *sakaratil-mauti*, akamuuliza: “Unaonaje (uchungu wa) kutoka roho ewe rafiki yangu?” Mwenye kukata roho akasema: “Sioni isipokuwa utamu na kheri na sihisi uchungu wowote.” Yule aliymzuru akastaajabu kwa sababu alikuwa anajua uchungu wa kutoka roho ya mwanadamu! Rafiki yake anayekata roho akamwambia alipoona mshangao wake: “Usistaajabu ewe rafiki yangu; kwa sababu mimi nimesoma Hadith kutoka kwa Nabii (saww) humo anasema: ‘Mwenye kuniswalia kwa wingi anasalimika kutokana na uchungu wa kutoka roho.’ Hivyo tangu wakati huo nimedumu katika kumswalia Mtume (saww) na nikazidisha zaidi na kwa sababu hiyo unaniona ninaraha wakati wa kutoka roho yangu.”¹⁸⁶

¹⁸⁵ *Athaaru wa barakaatu Swalawaati*, uk: 131

¹⁸⁶ *Qiswasu Swalawaatu*, uk: 73

SWALA YA USIKU WA KUAMKIA IJUMAA NA YA MCHANA WA IJUMAA:

Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww):

“Niswalieni kwa wingi katika Lailatul-Gharai na katika Yaumul-Azhar. Lailatul-Gharau ni usiku wa kuamkia Ijumaa na Yaumul-Azhar ni mchana wa Ijumaa, humo Mwenyezi Mungu huwaacha huru wenye madhambi, nayo ni siku ya sikukuu kwa umma wangu, natoeni sadaka kwa wingi humo.”¹⁸⁷

MTU ATAKAYEKUWA KARIBU MNO NA NABII (SAWW) SIKU YA KIYAMA

Imepokewa kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) kwamba amesema:

“Hakika atakayekuwa sehemu iliyokaribu mno na mimi kati yenu Siku ya Kiyama ni mwangi wenu wa kuniswalia duniani.”¹⁸⁸

KUPITA KATIKA SIRAT

Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww):

“Nilimuona mtu usingizini katika umma wangu anatetemeka katika Sirat na wakati mwingine anajivuta kwa tumbo na wakati mwingine ananig’inia, zikamjia Swala alizokuwa akinswalia zikamsimamisha kwa miguu yake hadi akatembea katika Sirat.”¹⁸⁹

¹⁸⁷ *Mustadrakul-Wasaail*, Jz: 6, uk: 71 mlango wa 35 Hadith ya 4

¹⁸⁸ *Jaamiul-Akhbaar*, Taaju Diyn ashaiyri chapa ya Daru Ridhaa Qum 1405 A. H uk: 59 fasil ya 28

¹⁸⁹ *Raudhatul-Waaidhiyna*, Juz: 2, Uk: 322

NURU SIKU YA KIYAMA

Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww):

“Mwenye kuniswalia mara moja Mwenyezi Mungu Siku ya Kiyama atamuumbia nuru katika kichwa chake, kuliani mwake, kushotoni mwake, juu yake, chini yake na nuru katika viungo vyake vyote.”¹⁹⁰

CHINI YA KIVULI CHA ARSHI YA MWENYEZI MUNGU MTUKUFU

Imepokewa kutoka kwa Nabii (saww) kwamba:

“Watu watatu Mwenyezi Mungu atawafunika kwa kivuli chini ya Arshi yake siku ambayo hakutakuwa na kivuli isipokuwa kivuli cha Mwenyezi Mungu.” Akaulizwa na ni akina nani hao ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu? Mtume (saww) akawataja: “Mwenye kuondoa matatizo katika ummah wangu, mwenye kuhuisha Sunnah yangu katika ummah wangu na mwenye kuniswalia kwa wingi.”¹⁹¹

KUMFUKUZA SHETANI KWA SWALA YA MTUME (SAWW)

Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww):

“Eeee wakumbukeni enyi ummah wa Muhammad, Muhammadi na Aali zake wakati wa shida zenu na matatizo yenu ili

¹⁹⁰ *Al-Mawaaidhul-Adadiyatu*, Uk: 413

¹⁹¹ Rejea iliyotangulia Uk: 313

malaika wenu wakuwezesheni kuwashinda mashetani ambao wanakukusudieni, hakika kila mmoja kati yenu ana malaika kuliani mwake anaandika mema yake na ana malaika kushotoni mwake anaandika mabaya yake, na anamashetani wawili kutoka kwa Ibilisi wanaompotosha, hivyo wanapomshawishi katika moyo wake naye akamtaja Mwenyezi Mungu na kusema:

وَلَا حَوْلَ وَلَا قُوَّةَ إِلَّا بِاللهِ الْعَلِيِّ الْعَظِيمِ وَصَلَّى اللهُ عَلَى مُحَمَّدٍ وَآلِهِ

mashetani wawili wanazuiliwa, kisha wanakwenda kwa Ibilisi wanamshitakia na kumwambia: ‘Tumechoshwa na jambo lake tuongezee waasi.’ Hatoacha kuwaongezea hadi atawaongezea waasi elfu moja, wanamwendea lakini kila wanapomtupia ushawishi anamtaja Mwenyezi Mungu na Muhammad na Aali zake wema (a.s.), na hivyo hawapati mwanya kwake wala muokozzi, wanarudi na kwenda kumwambia Ibilisi: ‘Hatutomuweza isipokuwa wewe umwendee kwa askari wako ili umshinde na kumpotosha.’

Ibilisi atamwendea na askari wake, Mwenyezi Mungu atawaambia malaika wake: ‘Huyu Ibilisi amemkusudia mja wangu - fulani au kijakazi wangu fulani – kwa askari wake, eee wa-pigeni vita.’ Watampiga vita kila shetani muovu malaika laki moja wakiwa juu ya farasi wa moto na mikononi mwao kuna panga za moto na mikuki ya moto, panga na mishale,¹⁹² visu na silaha zao ni za moto, na hawataaacha kuwatoa na kuwapiga vita kwavyo na kumteka Ibilisi na kumuwekea silaha hizo, naye atasema: ‘Mola wangu ahadi yako ahadi yako umenahirishia

¹⁹² *Nashaashiyb*: Ja’u Nnashaab kwa dhama na shada nayo ni nabal (Manati)

hadi wakati maalum.’ Mwenyezi Mungu Mtukufu atawaambia malaika wake: ‘Nimemwaahidi kwamba sitomuuwa lakini sikumwahidi kwamba sitomwadhibu kwa uchungu na silaha, mpatieni kipigo kwa silaha zenu kwani sitomfisha.’ Basi watamwadhibu kwa majeraha kisha watamwaacha basi hataacha kuwa ni mwenye kulia¹⁹³ kwa ajili ya nafsi yake na watoto wake walopigwa vita na kuuliwa,¹⁹⁴ na haliponi jeraha isipokuwa kwa kusikia sauti za washirikina zikitamka kufuru zao.

Na ikiwa muumini huyu atabakia katika utii wa Mwenyezi Mungu, kumtaja na kumswalia Muhammad na Aali zake (a.s.) Ibilisi atabakia katika majeraha hayo, na ikiwa mja ataacha hayona akajiingiza katika kumkhali Mwenyezi Mungu na maasi yake basi majeraha ya Ibilisi yatapona kisha atapata nguvu kwa muumini huyo hadi atamshawishi na atapanda mgongoni mwake na atateremka kwake, na mashetani wata-panda mgongo wake na shetani mmoja atawaambia rafiki zake: Je hamkumbuki yaliyotupata juu ya jambo la huyu mtu na sasa hivi amekuwa dhalili kwetu na ametufuata hadi amekuwa ana-pandwa na sisi.”

Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww): “Mkitaka kudumisha kilio cha Ibilisi na uchungu wa majeraha yake basi dumisheni utifufu kwa Mwenyezi Mungu na utajo wake na kumswalia Muhammad na Aali zake, na mkiacha hayo basi mtakuwa mateka, vitapandwa visogo vya baadhi yenu na baadhi ya waasi wake.”¹⁹⁵

¹⁹³ *Sakhanatul.*

¹⁹⁴ *Al-Mugattaliyna alaa binail-maf'uul min baab al-if'aali.*

¹⁹⁵ *Bahrul-Anuwar*, Jz: 60, uk: 272 namba 158

NURU KATIKA SIRAT

Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww):

“Niswalieni kwa wingi hakika kuniswalia ni nuru katika kaburi na ni nuru katika Sirat na ni nuru katika pepo.”¹⁹⁶

ANAWAJIBIKA KUPATA UWOMBEZI

Amesema Nabii (saww) katika wasia wake kwa Ali (as):

“Ewe Ali mwenye kuniswalia kila siku au kila usiku anawajibika kupata uombezi wangu hata kama atakuwa ni kati ya watu wenye madhambi makubwa.”¹⁹⁷

MAANA YA SWALA YA MWENYEZI MUNGU, YA MALAIKA, NA YA WAUMINI KWA MTUME (SAWW)

Kutoka kwa Abil-Mughirah amesema:

“Nilimuuliza Abu Hasan al-Kadhim (sa) nini maana ya Swala ya Mwenyezi Mungu na Swala ya malaika wake na Swala ya waumini kwa Muhammad na Aali zake? Akasema: ‘Swala ya Mwenyezi Mungu ni rehema na Swala ya malaika wake ni kumtakasa kwa ajili yake na Swala ya waumini ni kumuombea.’”¹⁹⁸

¹⁹⁶ *Mustadrakul-Wasail*, Jz. 5, Uk. 332, Mlango wa 31.

¹⁹⁷ *Bahrul-Anuwar*, Juz. 5, Uk. 334, Mlango wa 31 (*Istihbaab al-ikthaar min Swalaati alaa Muhammad wa Aalihi (saww)*)

¹⁹⁸ *Wasailu Shi'ah*, Jz: 6, uk: 375 mlango wa 22 *Taaqiyib swalaatl-maghrib*

KINGA DHIDI YA MOTO WA JAHANNAM

Kutoka kwa Swabaha bin Siyabah, kutoka kwa Abi Abdillah (as) amesema:

“Je nikufundishe kitu kitakachokukinga na moto wa Jahanam?”
Akasema: ndio, akasema (as): “Sema baada ya Alfajir: *Allahumma Swalilaa Muhammad Wa Aali Muhammad* mara mia moja, Mwenyezi Mungu ataukinga uso wako na moto wa Jahannam.¹⁹⁹

KUOZESHWA HURULAINI

Kutoka kwa Imam Abi Abdillah as-Sadiq (as) amesema:

“Vitu vinne vimepewa usikivu wa viumbe: Nabii, Hurulain, pepo na moto. Mja hamswalii Nabii (saww) au kumsalimia isipokuwa hayo yanamfikiana kuyasikia, na hakuna yeyote anayesema: ‘Eee Mwenyezi Mungu niozeshe Hurulain’ isipokuwa wanamsikia na wanasema: ‘Ewe Mola wetu hakika fulani ametuposa tuozeshe kwake.’ Na hakuna yeyote anayesema: ‘Eee Mwenyezi Mungu niingize peponi,’ isipokuwa pepo inasema: ‘Eee Mwenyezi Mungu mpe makazi kwangu.’ Na hakuna yeyote anayejikinga na moto kwa Mwenyezi Mungu isipokuwa moto unasema: ‘Eee Mola Wangu mwepushe na mimi.’”²⁰⁰

¹⁹⁹ Wasailu Shi’ah Jz: 6, uk: 479 mlango wa 25 *nubdhatu mimmaa yustahabu an yuzaada fiy taaqiyyib asubhi* Hadith 8941

²⁰⁰ Wasailu Shi’ah Jz: 6, uk: 465 mlango wa *istihbaabil-mauidhati baada kulli swalaati*

KUMSWALIA MUHAMMADI NA AALI ZAKE (A.S.) KILA WANAPOTAJWA MANABII (AS)

Kutoka kwa Muawiya bin Ammar amesema:

“Nilimtaja kwa Abi Abdillahas-Sadiq (as) mmoja kati ya Manabii na nikamswalia, as-Sadiq (as) akasema: ‘Ukitaja mmoja kati ya Manabii anza kumswalia Muhammad kisha kutohana naye Mwenyezi Mungu atamrehemu Muhammad, Aali zake na Manabii wote.”²⁰¹

RAFIKI WA MUHAMMAD (S.A.W.W.) KATIKA PEPO ZA JUU

Imepokewa kutoka kwa Imam Ridhaa (as) kwamba amesema: “Kati ya siri za Aali Muhammad (saww) katika kumswalia Nabii na Aali zake (as) ni kusema:

اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَآلِهِ فِي الْأَوَّلِينَ وَصَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَآلِهِ فِي الْآخِرِينَ وَصَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَآلِهِ فِي الْمَلَائِكَةِ الْأَعْلَى وَصَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَآلِهِ فِي النَّبِيِّنَ وَالْمُرْسَلِينَ اللَّهُمَّ اعْطِ مُحَمَّدًا وَآلَهُ الْوَسِيلَةَ وَالْفَضِيلَةَ وَالشَّرْفَ وَالرِّفْعَةَ وَالدَّرَجَةَ الْكَبِيرَةَ اللَّهُمَّ إِنِّي آمَنْتُ بِمُحَمَّدٍ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَلَمْ أَرَهُ فَلَا تَحْرِمنِي فِي

²⁰¹ Reja iliyotangulia Juz.7, Uk. 208 *Istihbaab Taqidiyam Swalaati Alaa Muhammad wa Aali Muhammad kullamaa dhukra ahdu minal-Anbiyaai*, Hadith ya 9129

الْقِيمَةِ رُؤْيَتُهُ وَارْزُقْنِي صُحْبَتُهُ وَتَوَفَّنِي عَلَى مِلْتَهُ وَاسْقَنِي مِنْ حَوْضِهِ مَشْرَبًا رَوِيًّا سَائِغاً هَنَي়ًا لَا أَظْمَاءُ بَعْدَهُ أَبَدًا إِنَّكَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ اللَّهُمَّ كَمَا آمَنْتُ بِمُحَمَّدٍ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَلَمْ أَرَهُ فَعَرَفْنِي فِي الْجَنَانِ وَجْهُهُ اللَّهُمَّ أَبْلِغْ رُوحَ مُحَمَّدٍ عَنِي صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ تَحِيَّةً كَثِيرًا وَسَلَامًا²⁰²

Hakika mwenye kumswalia Nabii (saww) kwa Swala hii dhambi zake zinavunjwa na anasamehewa makosa yake na inadumu furaha yake na dua yake inakubaliwa na anapewa maombi yake na anakunjiliwa riziki yake na anasaidiwa dhidi ya adui yake na anatayarishiwa sababu za aina mbalimbali za kheri na ana jaaliwa kuwa kati ya marafiki wa Nabii Wake katika pepo za juu.”²⁰³

AMALI YA MKESHA WA MWEZI SABA RAJABU

Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww):

“Mwenye kuswali katika usiku wa mwezi saba Rajab rakaan nne kwa kusoma Alhamdu mara moja na *Qul Huwallahu Ahdi* mara tatu na *Qul Audhu Bi Rabbil-Falaq* na *Qul Audhu Bi Rabbi Naasi*, na akamswalia Nabii (saww) mara kumi baada ya kumaliza,

²⁰² *Tahdhiybul-Ahkaami* cha Sheikh Tusiy, Khurasan 460H, Najaf al-Ashraf chapa ya Darul-Kutubil- Islamiyyati Teheran 1365H, Sharhi ya Juz. 3, Uk. 86, Hadith ya 15, *Dua Fiy Ziyaadati-Tamaamil –Miati Rakaati*

²⁰³ *Tahdhiybul-Ahkaami* cha Sheikh Tusiy chapa ya Darul Kutubil-Islamiyyati Teheran 1365, Sharhi Juz 3 Uk.86 *Dua fiyl ziyaadati tamaam miati rakaati* Hadith ya 15.

kisha akasema: *Subhaanallah Walhamdulillah Walaa Ilaahe Illallahu Wallahu Akbar* mara kumi, Mwenyezi Mungu atam-funika kwa kivuli cha Arshi yake na kumpa thawabu za mwenye kufunga mwezi wa Ramadhani na malaika watamuombea maghfira hadi amalize Swala hii, na atamfanya wepesi wakati wa kutoka roho na katika mbinyo wa kaburi na wala hatotoka duniani hadi aone makazi yake peponi na Mwenyezi Mungu atamsalimisha kutokana na fazaa za Kiyama.”²⁰⁴

AMALI YA USIKU WA NUSU YA SHABAN

Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww):

“Mwenye kujitwaharisha usiku wa nusu ya Shabani akajitakasa vizuri akavaa nguo mbili nadhifu kisha akatoka kwenda kwenye mswala wake kisha akaswali Isha, kisha baada yake akaswali rakaa mbili, katika rakaa ya kwanza atasoma Alhamdu na Aya tatu za mwanzo wa Sura al-Baqarah, Ayatul-Kursiyi, na Aya tatu za mwisho wa Sura al-Baqarah, kisha atasoma katika rakaa ya pili Alhamdu na *Qul Audh Bi Rabbi Naasi* mara saba na *Qul Audhu Bi Rabbil-Falaq* mara saba na *Qul Huwallahu Ahdi* mara saba, kisha atatoa salam na baada yake ataswali rakaa nne, atasoma katika rakaa ya kwanza Suratu Yaasin na katika rakaa ya pili atasoma *Haamiyim Dukhan* na katika rakaa ya tatu *Alif laam Miym Sajdah* na katika rakaa ya nne atasoma *Tabaarakalladhi Biyadihil-Mulk*, kisha ataswali baada yake rakaa mia moja atasoma katika kila rakaa *Qul Huwallahu* mara kumi na Alhamdu mara moja, Mwenyezi Mungu atamkidhia haja tatu hapa duniani au kesho Akhera, kisha akiomba kuniona katika usiku wake huo ataniona.”²⁰⁵

²⁰⁴ *Iqbaalul-Aamaali* cha Sayid Ibnu Tausi chapa ya Darul-Kutubil- Islamiayati, Teheran 1367 A. H

²⁰⁵ *Wasailus-Shi'ah* Juz. 8, Uk. 108, mlangano wa 8 *Istihbaab Swalaati Laylati Niswif Shaaban.*

FADHILA ZA SWALA YA MTUME NA AALI ZAKE (A.S.)

Kila kitu katika ulimwengu huu kinahukumu mbili, *Taklif* na *Wadhi’iy*, Swala ya kumswalia Muhammad na Aali Muhammad hukumu yake ni *Taklif ya istihbab*, na katika upande huo inathawabu nyingi kutoka kwa Mwenyezi Mungu, lakini – katika upande mwingine – inaathari za *Wadhi’iy* zisizohesabikana sisi tumeghafili na wingi wake. Kutohana na tunayojifunza kutoka katika Hadith tukufu tunaweza kutaja fadhila na baraka arobaini za kumswalia Muhammad na Aali wa Muhammad (s.a.w.w.):

1. Ni kujipamba kwa adabu ya Mwenyezi Mungu Mtukufu.
2. Ni kutii amri ya Mwenyezi Mungu Mtukufu.
3. Ni kupata utukufu wa Swala ya Mwenyezi Mungu.
4. Ni kuafikiwa na kuimba pamoja na malaika.
5. Ni kupata Swala ya malaika.
6. Ni sababu ya kupata ukuruba wa Mwenyezi Mungu.
7. Inapelekea kupata radhi za Mwenyezi Mungu.
8. Ni kuwa karibu na Mtume (saww).
9. Inapelekea kupata uombezi wa Nabii (saww).
10. Inapelekea kupata zawadi ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww).
11. Inawajibisha mwenye kuswali kuwa maarufu kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww).
12. Swala zinaandikwa katika kitabu cha mtu chenye nuru.

13. Ni kupata radhi za Mtume (saww).
14. Inapelekea kupata malipo na thawabu kwa mwenye kufanya uradi.
15. Ni ibada.
16. Ni kafara ya madhambi.
17. Inapelekea furaha ya Maimam wote (a.s).
18. Dua ambayo katikati yake kuna kumswalia Nabii (saww) inajibiwa.
19. Inapelekea kupata ufaulu duniani na Akhera.
20. Inapelekea kuwa mbali na moto.
21. Inatia nuru kaburini.
22. Inaondoaa hali ya kubanwa na kaburi.
23. Inaleta radhi za malaika wa mauti.
24. Inaleta radhi za Ridhiwani mwangalizi wa pepo.
25. Hakika ni kutimiza ahadi ya (Je mimi si ndio Mola Wenu).
26. Inaondoaa unafiki.
27. Inawajibisha kuombewa na viumbwe vyote.
28. Ni amali bora zaidi huko Akhera.
29. Inatakasa amali.
30. Inaleta afya.
31. Inapelekea kupata huruma.
32. Ni sababu ya kukubali utii.
33. Ni sababu ya kufanya majilisi ziwe nzuri.

34. Ni sababu ya kuepukana na kusengenywa.
35. Ni sababu ya kupata nguvu.
36. Ni sababu ya kukumbuka vitu.
37. Ni sababu ya kuwa na nuru nyigi siku ya Kiyama.
38. Inapelekea mizani kuwa nzito.
39. Inapelekea kuvuka katika Sirat.
40. Inapelekea kuridhiwa na Manabii wote.²⁰⁶

MALIPO YA MWENYE KUACHA KUMSWALIA MTUME (SAWW)

Kama ambavyo kumswalia Muhammad na Aali zake (a.s.) kuna athari kubwa na nyingi vile vile atapata balaa yule mwenye kudharau na kukusudia kuiacha kwa athari ovu na mbaya, na kati ya mambo ambayo humpata mwenye kuacha Swala ya Mtume (saww) ni:-

1. Atapigwa muhuri wa waovu katika paji lake kama ilivyokuja katika kitabu cha *Udatud-Daa'iy* cha Ibnu Fahdi al-Hilliyy.
2. Anakuwa dhalili mwenye kupuuzwa kama ilivyokuja katika Hadith ya Musa bin Ja'far (as).
3. Ni alama ya ubakhili kama ilivyopokelewa kutoka kwa maasumina.
4. Hiyo inahesabiwa kuwa ni katika dharau kama ilivyopokelewa kutoka kwa Nabii (saww).

²⁰⁶ Athaaru wabarakaatu swalaati uk: 155

5. Majilisi ambayo hatajwi humo Nabii wala haswaliwi ni balaa na majuto kwa wenye majilisi hiyo, kama alivyopokea mwenye kitabu cha *Udatud-Da'iy*.
6. Mwenye kuiacha anakosea njia ya peponi kama ilivyopokewa kutoka kwa Nabii (saww).²⁰⁷
7. Inampelekea mwenye kuacha kumswalia Muhammad na Aali zake (a.s.) kuwa mbali na Mwenyezi Mungu Mtukufu kama ilivyopolewa katika Hadith aliyoinukuu Ibnu Babawaihi kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww).
8. Inasababisha kuingia motoni kama ilivyopokelewa katika Hadith aliyoinukuu Ibnu Babawaihi kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww).
9. Na inapelekea kuwa mbali na waliokaribu (na moto).

BAHATI NZURI

Mwenyezi Mungu kwa utukufu Wake amenijaalia na kuniwafikisha mwishoni mwa maisha yangu ya kutunga kitabu hiki kuwa mgeni wa bwana wa Mashahidi Imam Husein (a.s) na Sayid Abdul-Adhim al-Hasaniy (ra), ambapo nilikwenda katika usiku wa kufa Shahidi Imam al-Baqir (a.s) na siku za Muslim – yaani usiku wa mwezi kumi na saba Dhilhija 1422 A. H – pamoja na mmoja wa wahudumu wa Imam Husein (a.s) kwenye raudha ya Sayid Abdul-Adhim al-Huseiniy huko Tehran. Na ni ada ya tangu miaka mingi kwamba misafara na vikundi vingi vya ziara ya Imam Husein huenda Tehran katika siku kama hizi kwa ajili ya kumzuru Sayid Abdul-Adhim al-Huseiniy.

²⁰⁷ *Al-Kaafiy* cha Thiqatul-Islaam al- Kullainiy chapa yaDarul- Kutubil- Islamiyat, Teheran 1365 A. H Juz. 2, uk. 495, Mlango waSwalatu Alaa Nabiyyi wa Ahli Baitihi, Hadith 19.

Mimi pia nilikwenda pamoja na mtoto wangu Sayid Muhammad bin Khamsaiy na watukufu wengine waliokuwa pamoja nami katika kikundi chetu maalum kwenye raudha yake ili kuungana na safu za misafara ya maombolezo ambayo inafika huko. Baada ya kumsalimia Imam al-Muntadhar (a.s) nilisoma ziara ya Ashuraa na dua ya tawasuli kwa Maimam watukufu (a.s) pamoja na Sayid Kazaruniy, na baada ya ma'atam na azaa kikundi kilijiandaa kuelekea kwenye raudha tukufu ya Sayid Abdul-Adhim, na wakati wakuondoka kwetu macho yangu yaliwaona marafiki wawili watukufu kati ya vipenzi wa Ahlul-Bait (a.s) waliokuja kutoka katika msikiti wa raudha katika sehemu ya Kasri la Dashti Tehran, nao ni Aswghar Nuru Bakhshity na Said Sha'abaniy, na baada ya kuzungumza kidogo katika baadhi ya mambo mazungumzo yalielekea katika kumswalia Muhammad na Aali Muhammad na nikawajulisha kuwa kitabu changu ni juu ya kumswalia Muhamad na Aali zake (a.s.), Saidi Shaabaniy akanipa habari juu ya majilisi itakayohudhuriwa na wapenzi wa Ahlul-Bait (a.s) na kuwa katika majilisi hiyo hakitowashughulisha tangu mwanzo wa majilisi hadi mwisho wake isipokuwa uradi wa kumswalia Muhammad na Aali Muhammad (a.s.).

Nilikuwa kama mwenye kiu ambaye anatafuta maji, nikachukua kwake anuani nanikaelekea kwake siku iliyofuatia, ndipo nikakutana na kijana mwenye kujaa hamasa na uchangamfu na ari na mwenye dini, mwenye adabu, mnyenyeketu mno na mchamungu, mpenzi wa Muhammad na kizazi cha Muhammad kwa kila maana ya neno hilo, kiasi kwamba dhahiri yake inaakisi undani wake mzuri, anameremeta huku nuru ya wilaya ikiwa dhahiri katika uso wake.

Baada ya kumsalimu, kumwamkia na kumuuliza hali nilimwambia hakika mimi namtafuta ndugu anayeitwa Majid al-Karbalai, akasema: "Ndio mimi karibu." Nikamwambia je, kwa ihsani yako unaweza kunieleza juu ya sababu ya kuasiisi kikundi chenu cha Darud-

Dhikir? Akasema: "Tulikuwa watu 15 tuliokusudia katika moja ya usiku na kuahidiana kuhuisha Sunnah ya Nabii (saww) na hususan Sunnah iliyosahauliwa, na ambayo kati ya hizo ni kumswalia Muhammad na kizazi cha Muhammad (s.a.w.w.), na kwa kuongezea nyuradi zingine zinazoingiza furaha kwa Maimam maasumini (a.s)." Baada ya hapo nilimuuliza: Tangu lini mlanza kikao cha majilisi yenu ya kwanza? Akasema: "Mwaka 1415 A. H." Nikasema: Na ni zipi haja zenu mlizozipata? Akasema: "Hatukuanzisha majilisi hii kwa ajili ya kukidhiwa haja zetu maalum bali ni kwa ajili ya mapenzi yetu kwa Ahlul-Bait (a.s) na kutaka kuharakishwa kudhihiri kwa Imam al-Mahdi anayesubiriwa (a.s), lakini kuna mtu mmoja kati ya ndugu zetu waliohudhuria pamoja na sisi ameweke nadhiri kwamba kama akikidhiwa haja yake ataita kikundi cha Darud-Dhikir na atafanya majilisi nyumbani kwake."

Nikasema: Maelfu mangapi ya Swala za kumswalia Mtume (saww) mmeshaswali hadi sasa? Akasema: "Bali sema ni milioni ngapi, mwenye kuhesabu ni ndugu yetu Shamsi kwa mfano:

- Alihesabu Swala kuanzia mwezi wa Ramadhani mtukufu katika mwaka uliopita hadi mwanzo wa mwezi wa Ramadhani wa mwaka huu ikafikia milioni tatu, elfu hamsini mia moja na thelethini na tisa (350,139).
- Idadi ya Swala katika siku ya kuzaliwa Imam Hasan (as) imefikia 91,817.
- Katika usiku wa 21 katika mwezi mtukufu wa Ramadhani imefikia 7000.
- Katika usiku wa 27 katika mwezi wa Ramadhani imefikia 76500.
- Idadi ya Swala katika siku ya Idil-Fitr imefikia 79,000.

- Katika siku ya kufa shahidi Imam as-Sadiq (a.s) imefikia 218,627.
- Katika siku ya kufa shahidi Fatma al-Maasuma (as) imefikia 112,818.
- Idadi ya Swala katika uzao wa Imam Ridhaa (a.s) imefikia 314,200.
- Idadi ya Swala katika siku ya kufa shahidi Imam al-Jawad (a.s) imefikia 216,401.
- Idadi ya Swala katika siku za kufa shahidi Muslim imefikia 100,000.
- Na hivyo jumla yake kwa muda wa miezi kumi na tano ni milioni nne mia nne na kumi na tano elfu na mbili (4,415,002)."

Kama ambavyo ndugu wanaopenda kuiga majilisi za kikundi cha Darud-Dhikir cha Tehran na ambacho kinakusanyika katika mnasaba wa sikukuu za Kiislam basi wanaweza kupiga simu kupitianamba zifuatazo kwa maelezo ya ziada: 06871139 na 0912099667.

Cha muhimu ni kwamba ndugu wapendwa ambao wana majilisi kama hizi ni sawa iwe Tehran au sehemu nyingine wanaweza kupiga simu kwa kuwasiliana na mwandishi wa kitabu hiki kwa simu kupitia namba: 0912109667, na kutuma shughuli zao pamoja na kueleza shida zao ambazo zimetatuliwa kwa baraka za majlisi hizi ili kuwashajiisha Waislamu wengine kuhuisha Sunnah hii na ili wale ambao hawajapata taufiki ya kujaribu na kuzifanya kazi majilisi hizi wajaribu majilisi hizi na washuhudie wigo wa athari zake.

WASIA WA AWALI KATIKA VIKAO VYA KIDINI

Nawausia viongozi wa misafara ya maombolezo, vikundi vya Husseiniya na vikundi vya ziara za kidini vinavyokwenda Qum, Jamkaran, Mashhad, Syria, Karbalaa na kwingineko, na washiriki wa majilisi za dua za Nudubah, Kumail, na majlisi za sikukuu za Kiislam, watenge wakati mahususi kwa ajili ya kumswalia Muhammad na Kizazi chake na katika kuhitimisha majilisi hizo waombe kwa Mwenyezi Mungu aharakishe kudhihiri kwa Swahibu Zaman, na vile vile watoe zawadi thawabu za Swala hizo kwa Maasumina kumi na nne na wafu wa waasisi wa majilisi hizo.

Kwa mfano katika Mashhad tukufu katika raudha ya Imam Ridha (a.s) katika uwanja wa Huriyah baada ya Swala ya Maghribi na Isha hufanywa uradi wa kumswalia Muhammad na Aali zake (a.s.) baada ya wenye kufanya uradi huu kuleta kiasi cha maji ya mimea na ambayo kwa kiajemi yanaitwa *Aab Nabaati*. Nayo ni sukari iliyotengenezwa kama vidonge maalum kisha wanakisomea Swala kwa kila kidonge mara mia moja, kisha mmoja wa washairi wenye kuwasifu Ahlul-Bait (a.s) husoma ziara ya Ashura na kutaja masaibu yao kisha wasimamizi wa majilisi hii hugawa sukari hiyo kwa wahudhuriaji wa uradi, na jambo muhimu na lakuzingatia ni kwamba mwenye kupata sukari hiyo anapata ponyo la kimwili na kiroho.

Mfano mwingine: Msafara wa Hujjatullah kwa ajili ya kuzuru sehemu ya Kasri la Dashiti Tehran, huwa wanakwenda Qum huko Jamkarankila wiki, na katika msafara huanza kwa kumswalia Muhammad na Aali zake (a.s.) hadi zifike Swala 50,000 kwa ajili ya kuharakisha kudhihiri kwa Imam al-Mahdi, kisha wanasoma uradi huu: “*Naad Aliyyan Madhharul-Ajaabi, Tajiduhu Aunan Laka Fiyn-*

nawaaib” Baada yake wanasoma ziara ya Ashura na Hadithual-Kisai tukufu.

Kama ambavyo hatusahau kumshukuru mwasisi wa msafara wa Hujjatullah kwa ajili ya kufanya ziara Tehran, naye akiwa ni kijana wa miaka 12, kijana huyu mcheshi aliweka nafsi yake nadhiri ili iwe ni askari kati ya maaskari wa Imam al-Hujjah (a.s) na utamuona ame-jaa ucheshi na uchangamfu na kumpenda kwake. Jina lake ni Sajjad Khamsayi, na baada ya hapo ndugu yake Muhammad mwenye umri wa miaka 16 alijiunga naye ili kumpa nguvu katika jambo hili.

Nimeshuhudia kwa karibu huduma mbalimbali zenyenikilishi za msafara huu, kama ambavyo hali ya kiroho iliyokuwa inatawala msafara huu iliandaa kwa wenyewe kuzuru mazingira ya kupata katika kila wiki haja muhimu kutoka kwa Imam Swahibu Zaman (a.s) kwa baraka za tawasul ya dhikiri tukufu. Mwenyezi Mungu aidumishe njia yao na aineemeshe kwa dua ya Imam Zaman Insha-Allah.

اللَّهُمَّ كُنْ لِوَالِيِّكَ الْحُجَّةُ بْنُ الْحَسَنِ صَلَوَاتُكَ عَلَيْهِ وَعَلَى آبَائِهِ
فِي هَذِهِ السَّاعَةِ وَفِي كُلِّ سَاعَةٍ وَلَيْاً وَحَافِظَاً وَقَائِدًا وَنَاصِرًا
وَدَلِيلًا وَعَيْنًا حَتَّى تُسْكِنَهُ أَرْضَكَ طَوْعًا وَتُمْتَعَهُ فِيهَا طَوِيلًا
بِرَحْمَتِكَ يَا أَرْحَمَ الرَّاحِمِينَ

ORODHA YA VITABU VILIVYO CHAPISHWA NA AL-ITRAH FOUNDATION

1. Qur'an Al-Kariim - Tafsir Al-Kashif Juzuuy ya kwanza mpaka Thelathini
2. Uharamisho wa Riba
3. Uharamisho wa uwongo Juzuuy ya Kwanza
4. Uharamisho wa uwongo Juzuuy ya Pili
5. Hekaya za Bahlul
6. Muhangaa wa Imamu Husein (A.S.)
7. Mikingamo iliyomzunguka Imamu Ali (A.S.)
8. Hijab vazi Bora
9. Ukweli wa Shia Ithnaashari
10. Madhambi Makuu
11. Mbingu imenikirimu
12. Abdallah Ibn Saba
13. Khadijatul Kubra
14. Utumwa
15. Umakini katika Swala
16. Misingi ya Maarifa
17. Kanuni za Ndoa na maadili ya Familia

18. Bilal wa Afrika
19. Abudharr
20. Usahihi wa Historia ya Uislamu na Waislamu
21. Salman Farsi
22. Ammar Yasir
23. Qur'an na Hadithi
24. Elimu ya Nafsi
25. Yajue Madhehebu ya Shia
26. Ukusanyaji na Uhifadhi wa Qur'an Tukufu
27. Al-Wahda
28. Ponyo kutoka katika Qur'an
29. Uislamu mfumo kamili wa maisha ya kijamii
30. Mashukio ya Akhera
31. Al Amali
32. Dua Indal Ahlul Bayt
33. Udhuu kwa mujibu wa Kitabu na Sunna.
34. Haki za wanawake katika Uislamu
35. Mwenyezi Mungu na sifa zake
36. Kumswalia Mtume (s)
37. Nafasi za Ahlul Bayt (a.s)
38. Adhana
39. Upendo katika Ukristo na Uislamu

40. Tiba ya Maradhi ya Kimaadili
41. Maana ya laana na kutukana katika Qur'an Tukufu
42. Kupaka juu ya khofu
43. Kukusanya swala mbili
44. Bismillah ni sehemu ya Qur'an na husomwa kwa Jahara
45. Kuwaongoza vijana wa kizazi kipyta
46. Kusujudu juu ya udongo
47. Kusheherekeea Maulidi Ya Mtume (s)
48. Tarawehe
49. Malumbano baina ya Sunni na Shia
50. Kupunguza Swala safarini
51. Kufungua safarini
52. Umaasumu wa Manabii
53. Qur'an inatoa changamoto
54. as-Salaatu Khayrun Mina -'n Nawm
55. Uadilifu wa Masahaba
56. Dua e Kumayl
57. Sauti Ya Uadilifu wa Binadamu
58. Umaasumu wa Mitume - Faida Zake Na Lengo Lake
59. Umaasumu wa Mitume - Majibu Ya Aya Zenye Utata
60. Umaasumu wa Mitume - Umaasumu wa Mtume Muhammad (s)
61. Nahju'l-Balaghah - Juzuu ya Kwanza

62. Nahju'l-Balaghah - Juzuu ya Pili
63. Kuzuru Makaburi
64. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Kwanza
65. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Pili
66. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tatu
67. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Nne
68. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tano
69. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Sita
70. Tujifunze Misingi Ya Dini
71. Sala ni Nguzo ya Dini
72. Mikesha Ya Peshawar
73. Malezi Ya Mtoto Katika Uislamu
74. Ubora wa Imam 'Ali Juu ya Maswahaba Na Ushia ndio njia iliyonyooka
75. Hukumu za Kifikihi zinazowahusu Wanawake
76. Liqaa-u-llaah
77. Muhammad (s) Mtume wa Allah
78. Amani na Jihadi Katika Uislamu
79. Uislamu Ulienea Vipi?
80. Uadilifu, Amani na Mtume Muhammad (s)
81. Mitala na Ndoa za Mtume Muhammad (s)
82. Urejeo (al-Raja'a)

83. Mazingira
84. Utokezo (al - Badau)
85. Hukumu ya kujenga juu ya makaburi
86. Swala ya maiti na kumlilia maiti
87. Uislamu na Uwingi wa Dini
88. Mtoto mwema
89. Adabu za Sokoni
90. Johari za hekima kwa vijana
91. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Kwanza
92. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Pili
93. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Tatu
94. Tawasali
95. Imam Mahdi katika Usunni na Ushia
96. Hukumu za Mgonjwa
97. Sadaka yenyе kuendelea
98. Msahafu wa Imam Ali
99. Ngano ya kwamba Qur'ani imebadilishwa
100. Idil Ghadiri
101. Kusoma sura zenyе Sijda ya wajibu
102. Hukumu zinazomuhusu mkuu wa kazi na Mfanyakazi
103. Huduma ya Afya katika Uislamu
104. Sunan an-Nabii

105. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Kwanza)
106. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Pili)
107. Shahiid Mfiadini
108. Kumsalia Nabii (s.a.w)
109. Ujumbe -Sehemu ya Kwanza
110. Ujumbe - Sehemu ya Pili
111. Ujumbe - Sehemu ya Tatu
112. Ujumbe - Sehemu ya Nne
113. Mariamu, Yesu na Ukristo kwa mtazamo wa Kiislamu
114. Hadithi ya Thaqalain
115. Maarifa ya Kiislamu
116. Ukweli uliopotea sehemu ya Kwanza
117. Ukweli uliopotea sehemu ya Pili
118. Ukweli uliopotea sehemu ya Tatu
119. Ukweli uliopotea sehemu ya Nne
120. Ukweli uliopotea sehemu ya Tano
121. Mkutano wa Maulamaa wa Baghdad
122. Safari ya kuifuata Nuru
123. Fatima al-Zahra
124. Myahudi wa Kimataifa
125. Kuanzia ndoa hadi kuwa Wazazi
126. Visa vya kweli sehemu ya Kwanza

127. Visa vya kweli sehemu ya Pili
128. Elimu ya Ghaibu ya Maimamu
129. Mwanadamu na Mustakabali wake
130. Imam Ali ('a) Ndugu wa Mtume Muhammad (s)
(Sehemu ya Kwanza)
131. Imam Ali ('a) Ndugu wa Mtume Muhammad (s) (Sehemu ya Pili)
132. Khairul Bariyyah
133. Uislamu na mafunzo ya kimalezi
134. Vijana ni Hazina ya Uislamu.
135. Yafaayo kijamii
136. Tabaruku
137. Taqiyya
138. Vikao vya furaha
139. Shia asema haya Sunni asema haya Wewe wasemaje?
140. Visa vya wachamungu
141. Falsafa ya Dini
142. Azadari-Kuhuzuni na Kuomboleza
143. Sunna katika Kitabu Fiqhi al-Sunnah
144. Mtazamo Mpya - Wanawake katika Uislamu
145. Kuonekana kwa Allah
146. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Kwanza)
147. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Pili)

148. Ndugu na Jirani
149. Ushia ndani ya Usunni
150. Maswali na Majibu
151. Mafunzo ya hukmu za ibada
152. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 1
- 153 Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 2
154. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 3
155. Abu Huraira
156. Vipengee kadhaa katika Swala ya Jamaa na Msikiti.
157. Mazingatio kutoka katika Qur'an - Sehemu ya Kwanza
158. Mazingatio kutoka kaitka Qur'an - Sehemu ya Pili
159. Mazingatio kutoka katika Uislamu - Sehemu ya kwanza
160. Mazingatio kutoka katika Uislamu - Sehemu ya Pili
161. Qur'ani Tukufu – Pamoja na Tarjuma ya Kiswahili
162. Falsafa ya Mageuzi ya Imam Husein (a.s)
163. Amali za Mwezi Mtukufu wa Ramadhani
164. Elimu ya Tiba za Kiislamu - Matibabu ya Maimamu
165. Uislamu Safi
166. Majlisi za Imam Husein Majumbani
167. Je, Kufunga Mikono
168. Uislam wa Shia
169. Amali za Makka

170. Amali za Madina
171. Asili ya Madhehebu katika Uislamu
172. Sira ya Imam Ali kuhusu Waasi
173. Ukweli uliofichika katika neno la Allah
174. Uislamu na Mifumo ya Uchumi
175. Umoja wa Kiislamu na Furaha
176. Mas'ala ya Kifiqhi
177. Jifunze kusoma Qur'ani
178. As-Sahifatul Kamilah as-Sajjadiyyah
179. Hayya 'Alaa Khayri'l-'Amal Katika Adhana
180. Ukweli kuhusu Funga ya Siku ya Ashura
181. Dua za Miezi Mitatu Mitukufu (Rajabu, Shaabani na Ramadhan)
182. Uadilifu katika Uislamu
183. Mahdi katika Sunna
184. Maswali Ya Uchunguzi Kuhusu Uislam
185. Kazi na Bidii ni njia ya maendeleo
186. Abu Talib – Jabali Imara la Imani
187. Ujenzi na Utakaso wa Nafsi
188. Vijana na Matarajio ya Baadaye
189. Usalafi – Historia yake, maana yake na lengo lake
190. Ushia – Hoja na Majibu
191. Mateso ya Dhuria wa Mtume (saww)

192. Maombolezo – Msiba wa Bwana wa Mashahidi (a.s.)
193. Shahidi kwa Ajili ya Ubinadamu
194. Takwa
195. Mwonekano wa Upotoshaji katika Hazina ya Kiislamu
196. Amirul Muuminina ('as) na Makhalfa
197. Uongozi na Utawala katika Mwenendo wa Imam 'Ali ('a)
198. Kuvunja hoja iliyotumika kutetea Uimamu wa AbuBakr
199. Adabu za vikao na mazungumzo
200. Hija ya Kuaga
201. Uwazi baina ya Maslahi na Vikwazo
202. Fadhila za watukufu watano katika Sahih Sita
203. Mdahalo baina ya Mwanachuoni wa Kisunni na Mwanachuoni wa Kishia (*Al-Muraja 'aat*)
204. Utawala na Uendeshaji katika Sera ya Imam Ali (as)
205. Upotoshaji dhahiri katika Turathi (Hazina) ya Kiislamu
206. Mtazamo kuhusu msuguano wa Kimadhehebu
207. Nchi na Uraia – Haki na wajibu kwa Taifa
208. Mtazamo wa Ibn Taymiyyah juu ya Imam Ali (as)
209. Uongozi wa Kidini – Maelekezo na Utekelezaji wa Kijamii
210. Maadili ya Ashura
211. Mshumaa – Shahidi na Kifo cha Kishahidi
212. Mizani ya Hekima – Hadithi za Ahlul Bait (as) – Sehemu ya Kwanza

213. Imam Ali na Mambo ya Umma
214. Imam Ali na Mfumo wa Usawa
215. Kuvunja Hoja Iliyotumika Kutetea Uimamu wa Abu Bakr
216. Mfumo wa Wilaya
217. Ndoa ya Mutaa
218. Vipi Tutaishinda Hofu?

**KOPI NNE ZIFUATAZO
ZIMETAFSIRIWA
KWA LUGHA KINYARWANDA**

1. Amateka Na Aba' Khalifa
2. Nyuma yaho naje kuyoboka
3. Amavu n'amavuko by'ubushiya
4. Shiya na Hadithi

**ORODHA YA VITABU VILIVYO
CHAPISHWA NA
AL-ITRAH FOUNDATION KWA LUGHA YA
KIFARANSA**

1. Livre Islamique